

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

## **BUNGE LA TANZANIA**

---

### **MKUTANO WA PILI**

---

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 08 Februari, 2011**

*(Mkutano Ulianza saa Tatu Asubuhi)*

### **WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wimbo wa Taifa uliimbwa)*

### **D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na taratibu zetu za kibunge, hili ni Bunge la Pili na ni Bunge ambalo tutafanya kazi zinazohusika. Kwanza kabisa nawakaribisheni katika Bunge letu. Kwakuwa tumepata nafasi ya kufanya Semina elekezi, ninaamini kila Mbunge atazingatia na kuendelea kusoma Kanuni zetu ili tuendeshe Bunge letu kwa utaratibu na amani.

Pia ninaamini utaratibu wa kukaa utawasumbua leo tu, lakini baada ya hapo mtakuwa mmetulia vizuri. Kama tulivyosema, vibandiko hivi ni vya muda, kama kuna marekebisho yoyote yale yaweze kufanyika bila ya kuwa na tatizo kubwa. Kwa hiyo, mvumilie matatizo mtakayoyapata kwa siku ya leo. Tunaendelea na ratiba yetu.

### **KIAPO CHA UTII**

Wajumbe wafuatao waliapa kiapo cha utii na kukaa katika nafasi zao ndani ya Bunge:-

- (1) Mhe. Amina Abdallah Amour
- (2) Mhe. Magdalena Hamis Sakaya
- (3) Mhe. Rebecca Michael Mngodo
- (4) Mhe. Sabreena Hamza Sungura
- (5) Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini
- (6) Mhe. Mariam Nassoro Kisangi

**SPIKA:** Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameapishwa leo na ninawatakia kazi njema ya kuliongoza Bunge letu kwa miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

## **HATI ZILIZOWASILISHWA**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake vilivyochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

### **Changamoto za Uchaguzi Mkuu**

**MHE. SALIM HEMED HAMIS (CHAMBANI)** aliuliza:-

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 kumalizika na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kutangazwa mshindi wa Kiti cha Urais:-

- (a) Serikali inatathimini vipi mafanikio ya changamoto zilizojitokeza wakati huo wa Uchaguzi Mkuu?
- (b) Je, ni hatua zipi zinapaswa kuchukuliwa ili uchaguzi ujao uwe bora zaidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Hamisi, Mbunge wa Chambani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya Uchaguzi Mkuu kukamilika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeendelea kufanya tathmini kuangalia namna uchaguzi huo ulivyofanyika pamoja na changamoto zilizojitokeza. Kwa ujumla, Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 ulifanyika vizuri kwa amani na utulivu na ambao ulikipa Chama Cha Mapinduzi ushindi kwa upande wa Rais 61.6%, kwa upande wa Wabunge leo hii ni 260 kati ya Wabunge waliopo humu ndani 350, kwa upande wa Madiwani 2,802 kati ya Madiwani 3,337 nchi nzima, na kwa upande wa Madiwani, Viti Maalum 969 kati ya Madiwani 1181.

Pamoja na mafanikio haya, tathmini inaonesha kwamba zipo changamoto Zilizojitokeza, na miongoni mwake ni hizi zifuatazo:-

- (i) Wapiga kura kujiandikisha au kwenda kurekebisha taarifa zao siku za mwisho na hivyo kusababisha msongamano vituoni na kuonekana kama siku za kuboresha daftari zilizopangwa na Tume hazitoshi;
- (ii) Baadhi ya vituo vya kupigia kura kuwa mbali na maeneo wanayoishi Wapigakura, hususan maeneo ya vijijini. Hali hii ilisababisha watembe mwendo mrefu kukagua orodha ya majina na siku ya kupiga kura;
- (iii) Mwitiko mdogo wa wananchi ambapo zaidi ya asilimia 57 ya Watanzania wenye sifa hawakujitokeza kupiga kura;
- (iv) Baadhi ya Vyama vya Siasa kutozingatia Maadili ya Uchaguzi wakati wa kampeni za za Uchaguzi;
- (v) Kutokuwepo chombo cha kuratibu na kusimamia elimu kwa Wapigakura; na
- (vi) Tatizo la teknolojia, ambapo mfumo wa kujumlisha matokeo ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge majimboni kufanya kazi polepole kiasi cha kuzua mashaka.

Mheshimiwa Spika, changamoto nilizotaja hapa ni baadhi tu, tathmini rasmi ya Uchaguzi inafanywa na Tume na itatangazwa baadaye.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kurekebisha kasoro zilizojitokeza kwa manufaa ya chaguzi zijazo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- (i) Kuzifanyia marekebisho Sheria zinazohusu masuala ya uchaguzi kwa kuzihusisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 na Sheria za Uchaguzi Na.1 ya mwaka 1985. Haya ni mambo ambayo wanafikiria katika tathmini yao wanayoandaa.
- (ii) Kuweka mkakati wa kutoa Elimu ya Uraia na Elimu ya Mpigakura kwa utaratibu endelevu pamoja na kuwa na chombo kitakachoratibu utaratibu huo.
- (iii) Kuendelea kuboresha daftari la Kudumu la Mpira kura pamoja na kuangalia upya vituo vya kuandikisha Wapigakura ili kuvisogeza karibu na wananchi.
- (iv) Kutumia teknolojia rahisi na sahihi katika mchakato wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na kuboresha mchakato mzima katika hatua mbalimbali za uchaguzi.

- (v) Nia njema ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, ya kutaka Katiba yetu iangaliwe upya pengine nayo itatoa majibu kwa baadhi ya changamoto zilizojitokeza. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED HAMIS:** Nakushukuru kwa majibu yako, lakini napenda niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, 50% na kwa maneno mengine nusu ya Watanzania, milioni 20 waliojiandikisha katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 hawakwenda kupiga kura katika vituo vya kura siku ya uchaguzi tarehe 31 Oktoba, amedai kwamba CCM kwa vyovyote vile itarekebisha matokeo ili ishinde kwa maana itachakachua na haya yakitokea, basi wananchi wanaamini kwamba hapatakuwa na mabadiliko yoyote ya maana ya maendeleo kwa Mtanzania wa kawaida: Je, Serikali itarekebisha tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, baada ya uchaguzi tarehe 31 Oktoba, 2010 nchi yetu imekumbwa na shindikizo na taharuki za maandamano na migomo mbalimbali kiasi cha kuhatarisha amani, lakini vilevile imeonekana kwamba baada ya uchaguzi nchi imekabiliwa na hali ngumu sana ya maisha: Je, vielelezo hivi na tathmini hii haitoshi kwa Serikali kuona kwamba Watanzania wamechoshwa na utawala wa Serikali ya CCM na kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuachia ngazi ili yasitokee mabaya zaidi?

**SPIKA:** Naomba wanaouliza maswali ya nyongeza wawe *direct*, wasitupigie hotuba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwenyewe kwamba zaidi ya 57% ya waliojiandikisha hawakwenda kupiga kura, hiyo ni taarifa ambayo wote tunajua na hivi sasa Tume ya Uchaguzi inafanya tathmini, lakini inaandika taarifa nzima ya uchaguzi na itakuwa wazi kwa Wanatanzania wote, lakini hili jambo haliwezi kuhusishwa na Chama cha Mapinduzi kwa sababu pengine lingehusishwa ingekuwa ni *advantage* kwa Vyama vya Upinzani kuchukua hii asilimia zaidi ya hamsini ili wawapigie kura wao. Lakini baadhi ya sababu zilizotolewa ni hizi zilizotolewa.

Kwa hiyo, wote sisi Vyama vya Siasa tunao wajibu wa kueleemisha wanachama wetu ili wajitokeze kwa wingi kupiga kura kama tulivyofanya wakati wa kujiandikisha, kila chama kilijaribu kwa uwezo wake kutafuta makada wake wajiandikishe, lakini katika upigaji wa kura lazima wote tushirikiane. Hili haliwezi kuwa la Chama cha Mapinduzi, na hakuna chochote kilichochakachuliwa, huo ni msemo wa kwenye majukwaa. Watanzania wametoa ridhaa yao kwa Chama cha Mapinduzi kwa matokeo niliyoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninajua katika mchezo wowote wa mpira, mtu atakayeshindwa ni lazima hakosi visingizio hasa makocha. Makocha wa Vyama vya Siasa ndio wanaotoa visingizio vya kuchakachua, lakini ushindi ni wazi kwa takwimu na ndiyo maana hata *European Union* wametoa taarifa rasmi kwamba uchaguzi ulikuwa huru na haki. CCM imeshinda kihalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya uchaguzi Mheshimiwa Salim Hemed Salim anasema hali ni ngumu na CCM iachie ngazi. Kama tunafuata mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi na utawala wa Sheria, Watanzania wameipa ridha ya kutawala CCM na kwa sababu uchaguzi huu tulikuwa tunashindanisha sera, kwa hiyo, ndugu zangu nataka hizo sera zenu ambazo Watanzania wamezikataa mztie kabatini msubiri miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa sababu Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni mojawapo ya walalamikiwa wakubwa katika sakata zima la uchaguzi, na kwa sababu katika maeneo kadhaa ya nchi yetu Tume ilikiuka utaratibu halali wa uendeshaji wa uchaguzi, na kwa sababu chama chetu kiliomba na kikaitaka Serikali iunde Tume huru ambayo ikiangalia matatizo kadhaa ambayo yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi na Tume hiyo isitoke kwenye chama chochote cha siasa:

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu uwezekano wa kuunda Tume huru ambayo itaweza kujua mapungufu kadhaa yaliyojitokeza kwenye uchaguzi na sio kuiachia Tume ya Uchaguzi kwa sababu nayo ni mdau? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Freeman Mbowe - Mbunge wa Hai na Kiongozi Rasmi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba walilalamikia Tume, lakini kama nilivyosema, haya machache niliyoyasema ni sehemu tu ya taarifa ambayo Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria itaitoa na itafanya tathmini. Kwa hiyo, Watanzania wote ningependa na kuwasihii wasubiri hiyo Taarifa Rasmi ya Tume itakayoonesha namna uchaguzi ulivyofanyika vizuri. Lakini pia hivi leo Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa kauli itakayohusiana kwa kiasi fulani na mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa kuwa wao wanaamini kabisa kwamba Tume ya Uchaguzi haifai na Mheshimiwa Rais ametoa ridhaa ya kufanya mabadiliko ya Katiba, hata ikibidi kuandika Katiba mpya, ninafikiri *solution* hapa, tujipe muda ili wote tushirikiane, vyama vyote vya siasa, akiwepo Mheshimiwa Freeman Mbowe na chama chake, tutoe mawazo yatakayojenga msingi mzuri zaidi wa marekebisha ya Katiba ili haya mambo mengine ambayo Mheshimiwa Freeman Mbowe anayaona, yasitokee kwa baadaye. Kwa hiyo, nafikiri tujenge msingi na mawazo ndani ya Katiba ambayo sisi Wabunge tutahusishwa.

**SPIKA:** Nadhani tumechukua muda mwingi kwa swali hili, dakika 10. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 2

### **Kuligawa Jiji la Dar es Salaam Kwenye Mikoa Mitatu**

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU** aliuliza:-

Serikali iliamua kuunda Wilaya tatu, Ilala, Temeke na Kinondoni kwenye Jiji la Dar es Salaam na kufanya huduma nyingi kugawanywa Kimkoa katika Wilaya hizo tatu kama vile Polisi Mkoa, Wanausalama wa Mikoa, Hospitali za Mikoa na kadhalika kutokana na wingi wa watu na mahitaji:-

Je, Serikali haioni kuwa, sasa ni wakati muafaka wa kuligawa Jiji la Dar es Salaam katika Mikoa Mitatu kulingana na Wilaya ambazo tayari zimeshaundwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uundwaji au ugawajii wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na.7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na. 8 (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria ya taratibu za uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imejiwekea vigezo maalum vya kuzingatia wakati wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala kwa mujibu wa taratibu na sheria. *“The Region and Districts Establishment Procedure Act, cap. 397, R.E. 2002.”* Aidha, ongezeko la idadi ya watu na mahitaji sio vigezo pekee vinavyozingatiwa katika ugawaji wa maeneo mapya ya utawala. Eneo la utawala linaloanzishwa lazima likidhi vigezo vyote vilivyowekwa kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotakiwa kukidhi ili Mkoa mpya uanzishwe ni vifuatavyo:-

- (1) Ukubwa wa eneo lenye kilometa za mraba 20,000;
- (2) Idadi ya Wilaya zisizopungua 4;
- (3) Asilimia tatu (3%) ya idadi ya watu kitaifa;
- (4) Idadi ya Tarafa zisizopungua 15;

- (5) Idadi ya Kata zisizopungua 45;
- (6) Idadi ya Vijiji visivyopungua 150;
- (7) Idadi ya watu wasiopungua 100,000;
- (8) Eneo lenye jiografia inayozuia huduma kuwafikia wananchi kwa urahisi kama vile milima, mito, misitu mikubwa, visima na kadhalika;
- (9) Miundombinu ya uhakika;
- (10) Uwezo wa Serikali kuanzisha Mkoa mpya; na
- (11) Wananchi kuwa tayari kuchangia gharama za kuanzisha mkoa mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi kufanyika kuhusu vigezo vinavyotumika kuanzisha maeneo mapya ya utawala katika Mikoa, Wilaya zote tatu za Mkoa wa Dar es Salaam hazikidhi kupandishwa hadhi na kuwa Mikoa pamoja na kuwa na idadi kubwa ya watu. Kwa mantiki hiyo, hatua nyingine muhimu zinatakiwa kufanywa kabla ya kufikiria kuunda Mikoa mipya itakayotokana na Wilaya tatu za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Mkoa wa utendaji katika Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa, Hospitali za Mikoa inayotokana na Wilaya za Ilala, Temeke, Kinondoni, ni kwa lengo la kurahisisha utoaji huduma na kurahisisha usimamizi wa utekelezaji ambao haumaanishi uundwaji wa maeneo mapya ya utawala. Utaratibu huu uliamuliwa na Serikali kwa lengo la kuboresha huduma na kuongeza ufanisi kiutendaji katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuzingatia changamoto za Jiji la Dar es Salaam katika maeneo ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao na utoaji wa huduma za afya zinazotokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kutokana na uhalisi na uhalisia wa suala hili na ukweli wa suala hili: Je, Serikali ipo tayari kulipitia tena upya suala hili na kulipatia ufumbuzi wa kudumu katika Mkoa huu wa Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naielewa *concern* ya Wabunge wa Dar es Salaam kuhusu tatizo hili linalozungumzwa hapa. Sitaki tufike Serikali ione kane kwamba hatuzioni *complications* ambazo zinatokea katika Jiji la Dar es Salaam na kufikiri kwamba hakuna haja ya kuanzisha eneo hili.

Mheshimiwa Zungu anazungumza habari ya kuanza tena upya, labda ni vizuri pia nikatoa picha hapa kwamba maana yake nini unapozungumza kwamba unataka kuanzisha Mkoa mpya kwa maana ya fedha.

Hapo unazungumza habari ya mikoa mitatu ambayo kama nilivyosema, unazungumzia habari ya Wilaya nne katika kila Mkoa, maana yake unazungumzia hapa Wilaya 12. Kwa maana ya kwamba utachukua wastani wa chini kabisa wa shilingi bilioni tano unazungumza habari ya shilingi bilioni 60. Kwa hiyo, wakati tunapozungumza haya, nilitaka nitoe picha hiyo pamoja na kwamba takwimu hizo sitaki kuzitumia kwa ajili ya kupinga jambo linalozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia habari ya kulirudia tena upya, hakuna *problem* ya kurudiwa tena upya, lakini vigezo hivi nilivyoviweka hapa, ndivyo vitakavyotumika hata kurudia upya zoezi zima linalozungumzwa hapa. Kwa hiyo, nakaribisha mawazo haya kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nikielekezwa kwamba nikarudie upya, nitarudia, lakini tutatumia vigezo hivi tulivyovizungumza hapa. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo la Wilaya ya Manyoni linafanana kabisa na tatizo la Mkoa wa Dar es Salaam kwa maana Wilaya ya Manyoni ni asilimia 58 ukubwa wake kwa Mkoa wa Singida, na kwa kuwa Wilaya hiyo ni kubwa sana na jiografia yake ni ngumu sana na hata utoaji huduma ni kazi sana na lengo la Serikali ni kusogeza huduma kwa Watanzania walio wengi: Je, Serikali itachukua hatua ya kufuatilia ugawaji wa Wilaya ya Manyoni ili huduma ziweze kwenda vizuri kwa Watanzania wa Manyoni? (*Makofi*)

**SPIKA:** Kweli haifanani hata kidogo tena ni kinyume chake. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwamba umenisaidia kuonyesha hiyo tofauti. Lakini sitaki tusione *concern*. Yapo maombi mengi sana ambayo yameletwa ambayo yanapitia katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kuomba kupata Wilaya mpya, kwa maana ya kuimarisha huduma.

Hivi karibuni kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge, kuna Wilaya ambazo tayari zimeshatamkwa na sasa tunategemea kwamba tutaanza. Kuna mambo mengi ya kufanyika, miundombinu na mambo mengine na kuteua wale watakaohusika katika kuziendesha hizi Wilaya.

Sasa hizi Wilaya nyingine anazozungumza Mheshimiwa ziko katika maombi yale ambayo yameletwa mengi tu ambayo sasa tunapitia kwa vigezo vile nilivyovieleza hapa, tunajaribu kuchambua moja moja. Hizi Wilaya alizozitaja Mheshimiwa kama zitaonekana zinakidhi, *no problem*. Sisi tutaona kwamba tunampelekea Mheshimiwa, kazi ni kupeleka tu hapa wala usiwe na wasiwasi Mheshimiwa Mbunge wewe hata kama kuna kijiji unataka kiwe Wilaya, wewe lete sisi tutakwenda kuangalia kwamba hiki kijiji kimekwenda kwa maana huku kuna mto, huku kuna mto, sasa kijiji kimebaki kinaletwa, mzee sasa si unaona hapa hawawezi kukatisha? Kwa hiyo, tunaomba wawe Wilaya. Kwa hiyo, nataka niseme hapa kwamba Serikali haizuii kabisa *as long as* Serikali hii inakusudia kuhudumia wananchi ndicho inachotaka kufanya.



**Benki ya Wanawake**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE** aliuliza:-

Ingawa Serikali ilikubali kuanzisha Benki ya Wanawake hapa nchini, lakini Benki hiyo ambayo ina Makao Makuu yake Dar es Salaam, haina Matawi sehemu nyingine za nchi:-

(a) Je, ni lini sasa uanzishwaji wa Matawi mengine ya Benki hiyo utafanywa kwenye Mikoani?

(b) Je, ni chombo gani cha kifedha kitakachohakikisha utekelezaji wa hatua iliyotajwa kwenye swali hili mapema iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ni kweli kuwa Serikali imewezesha uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Aidha, Benki hiyo yenye Makao Makuu yake Jijini Dar es Salaam inayo Tawi moja tu lililopo katika Mtaa wa Mkwepu na haina Matawi mengine Mikoani. Hata hivyo, mipango ya baadaye ya Benki hiyo ni kufungua Matawi mengine Mikoani ili wananchi wengi zaidi waweze kufikiwa na huduma za Benki hii. Baada ya maelezo hayo mafupi napenda kumjibu Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Ngoye kuwa, Benki hii kwa hivi sasa haina mtaji wa kutosha utakaoiwezesha kufungua matawi mengine Mikoani. Pamoja na kuwa Serikali imewezesha Benki hiyo kwa kuipatia mtaji shilingi bilioni 4.8, bado mtaji huo hautoshi kuweza kufungua matawi mengine.

Hata hivyo, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa Benki imeshaandaa mpango endelevu wa kufungua matawi mengine Mikoani kwa awamu kwa jinsi mtaji utakavyokua.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Wanawake, Tanzania inaendelea kuwahamasisha wadau mbalimbali kama vile Halmashauri mbalimbali, Mifuko mbalimbali ya Pensheni, Makampuni mbalimbali na watu binafsi kununua hisa za Benki ya Wanawake kwa lengo la kukuza mtaji wake ambao utawezesha Benki hiyo kufungua matawi mengine.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa vipo vyombo viwili vitakavyohakikisha utekelezaji wa hatua hii ambavyo ni Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya utoaji wa vibali na Wizara ya Fedha na Uchumi ambayo inahusika na ununuzi wa Hisa.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilishatoa mtaji wa shilingi bilioni 4.5 kwa Benki hii ili iweze kujiendesha na sasa inaonekana kwamba mtaji huo ni mdogo: Je, Serikali iko tayari sasa kuweza kufikiria kuongeza kiwango cha mtaji ili kuimarisha Benki hii ukizingatia umuhimu wa ukombozi wa mwanamke kiuchumi?

Swali la pili, kwa kuwa inaelekea uanzishaji wa matawi huko Mikoani itachukua muda mrefu kidogo. Je, Benki hii haioni sasa umuhimu wa kuanzisha dirisha maalum ambalo litahusika moja kwa moja na mikopo ya wanawake kupitia *SACCOS* zao ambazo zimeanzishwa huko Mikoani na kwamba wanawake ni wazuri sana katika kukopa na kurudisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mtaji wa Benki hautoshi, lakini Serikali tayari imeshachukua hatua za kuongeza mtaji. Ili kuhakikisha kuwa mtaji wa Benki unakuwa na hivyo kufungua matawi Mikoani, Serikali imeahidi kutoa shilingi bilioni mbili kila mwaka kuanzia mwaka 2010 hadi 2015.

Mheshimiwa Spika, ahadi hii ilitolewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2010 katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mwaka 2010 tayari Serikali imeshatoa shilingi bilioni mbili kwa Benki ya Wanawake Tanzania ili iweze kuimarisha mtaji wake.

Swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge ni jinsi gani Benki inaweza kufungua dirisha dogo ambalo litahusisha au litakuwa na mahusiano ya karibu na *SACCOS* au vikundi vingine vya wanawake kama *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, tayari hilo tumeshaliona. Katika mkakati endelevu wa Benki tuna maeneo makuu mawili ambapo tunahusiana au tunashirikiana kwa karibu sana na *SACCOS* na *VICOBA*. Eneo la kwanza ni kwamba *SACCOS* na *VICOBA* ni wateja wakubwa wa Benki ya Wanawake ya Tanzania. Kwa hiyo, tunahamasisha *SACCOS* au *VICOBA* zifungue akaunti katika Benki ya Wanawake na wakishafungua akaunti wachukue mkopo kutoka kwa Benki ya Wanawake na wao wanakwenda kuwagawia wateja wao au wanachama wao. Hilo ndio eneo la kwanza ambalo tumeliona.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili tumeamua kufungua vituo katika sehemu mbalimbali ambapo kuna *SACCOS*. Sio Benki, lakini ni vituo, na tunatoa mafunzo,

tumeanza na Mkoa wa Dar es Salaam, tumefungua vituo Kigamboni, Tabata, Segerea na Kibaha Mjini na nina uhakika pia tumefungua vituo kwa ajili ya kushirikiana ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi ambao wamejiunga katika *SACCOS*.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba niulize tu kwa sababu suala la mtaji ndilo ambalo tunaona ni kikwazo katika Benki hii kutoa mikopo mingi katika mikoa yetu. Kwa hiyo, ninapenda kujua ni mtaji wa kiasi gani unahitajika ili Benki hii iweze kutoa matawi yake kwa Mikoa mbalimbali na wanawake wengi waweze kunufaika ikiwemo na wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ambao kwa kweli wana hamu kubwa ya kuwa na Tawi la Benki ya Wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mujibu wa taratibu za Kibenki hapa Tanzania mtaji ambao utaiwezesha Benki kufungua matawi mengine katika Mkoa mmoja au Mikoa mingine ni shilingi bilioni 17. Kama tulivyosema, sasa hivi mtaji wetu ni shilingi bilioni 4.8, lakini tuna shilingi bilioni mbili ambazo tunazipata kutoka Serikalini, kwa hiyo, kwa miaka mitano itakuwa shilingi bilioni 10. Naomba nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mkahamasishe Halmashauri zenu, wanawake waliopo katika Majimbo yenu wanunue hisa ili kuweza kukuza mitaji haraka ya Benki ya Wanawake wa Tanzania.

**SPIKA:** Ahsante kwa sababu changamoto ni kuongeza mtaji, basi tunaendelea.

Na. 4

### **Utaratibu wa Kupatiwa Matibabu Nje ya Nchi**

**MHE. MCH. DR. GETRUDE P. RWAKATARE** aliuliza:-

Taratibu za kwenda kupatiwa matibabu nje ya nchi haziko wazi kwa watu wote kwa sababu hazijaweka wazi vigezo vinavyotumika kwa wale wanaohitaji matibabu hayo:-

Je, ni vigezo gani vinavyotumika kubainisha wagonjwa wanaotakiwa kupatiwa matibabu nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo ambavyo hutumika ili kuwaongoza Madaktari wanaohudumia wagonjwa katika Hospitali za ngazi ya Kitaifa katika kuamua mgonjwa apelekwe nje ya nchi kwa matibabu ni pamoja na:-

- (a) Kutokuwepo kwa utaalum unaohitajika kumtibu au kumfanyia uchunguzi mgonjwa hapa nchini;
- (b) Kutokuwepo kwa vifaa vinavyohitajika kumtibu/kumchunguza mgonjwa hapa nchini; na
- (c) Mgonjwa kuugua au kugunduliwa kuwa ana ugonjwa unaohitaji matibabu ya haraka ili kuokoa maisha yake, wakati akiwa nje ya nchi.

Hospitali zinazokubalika kutoa rufaa kwa mgonjwa kwenda kutibiwa au kufanyiwa uchunguzi nje ya nchi ni zile zilizoko katika ngazi ya rufaa ya kitaifa ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Taasisi ya Saratani - *Ocean Road*, Hospitali ya Rufaa ya Bugando, Hospitali ya Rufaa KCMC, Mbeya Rufaa, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto.

Daktari Bingwa katika fani yake akiridhika kwamba mgonjwa anayemhudumia anahitaji kutibiwa nje ya nchi, humwomba Mkuu wake wa Idara kuundwa kwa jopo la Madaktari Bingwa wasiopungua watatu, ambao hujadili hali ya mgonjwa na kutoa mapendekezo kama mgonjwa anatakiwa kwenda kutibiwa nje ya nchi. Endapo wataridhia, taarifa ya jopo hilo huwasilishwa kwa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ambaye ndiye mwenye mamlaka ya rufaa. Mtendaji Mkuu wa Hospitali akiridhia, taarifa ya rufaa mhusika huwasilishwa Wizarani ambako hujadiliwa na Kamati ya Wagonjwa wa nje. Baada ya ridhaa ya Kamati hiyo, ndipo taratibu za kumsafirisha mgonjwa kwenda nje ya nchi kwa matatibu au uchunguzi hufanyika. Aidha, katika mazingira ya udharura ili kuokoa maisha ya mgonjwa, Katibu Mkuu anaweza kutoa kibali kabla ya taarifa ya rufaa ya mgonjwa kujadiliwa na Kamati ya Wagonjwa wa nje. Hata hivyo, baada ya mgonjwa kusafirishwa, rufaa yake hujadiliwa na Kamati kwa madhumuni ya kuwa na kumbukumbu sahihi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tayari Serikali imeanzisha huduma za upasuaji mkubwa wa moyo (*Open Heart Surgery*) na tiba ya kusafisha figo (*Renal Dialysis*) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, uwekaji wa viungo bandia vya nyonga na goti (*Total hip and knee replacement*), upasuaji wa ubongo na mgongo na uchunguzi kwa kutumia mashine ya kisasa inayotumia nguvu za sumaku (*Magnetic Resonance Imaging – MRI*) na *CT Scan*.

Kuanzishwa kwa huduma hizi kumepunguza gharama za kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi na wagonjwa wengi zaidi watanufaika kwa huduma hizi kwa kupatikana hapa nchini.

**MHE. MCH. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Je, Serikali inaweza kuweka vigezo hivi wazi zaidi kwa watu wengi hasa wananchi wa kawaida waweze kujua kwa sababu suala hili limegubikwa na malalamiko na manung'uniko mengi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wengi hasa katika maeneo ya vijijini hawaelewi vigezo ambavyo vinatumika katika kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo ninasema, naomba Waheshimiwa Wabunge katika mikutano yao ya hadhara waweze kutoa hizi taarifa kwa wananchi wao kwamba unapoumwa, unatakiwa kwenda hospitalini katika Wilaya, na kwenye Wilaya wakishindwa kukutibu wanakupeleka kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, kama wanashindwa kukutibu ndipo wanakupeleka sasa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili; kama uko kwenye Kanda ya Kaskazini, Hospitali ya Rufaa ya KCMC; Hospitali ya Bungando au Mbeya katika Kanda zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wasaidiane na Wizara katika kuhamasisha wananchi waelewe haki zao za kuweza kupata matibabu ya rufaa. Lakini pia naomba mwajulishe kwamba katika Hospitali yetu ya Muhimbili kuna huduma za kufanyiwa operesheni za moyo bure, operesheni na kusafishwa mafigo pamoja na huduma nyingine ambazo Serikali yetu imetoa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na vigezo, nilikuwa napenda kuuliza: Ni kwa nini Serikali ya Tanzania imekuwa inawapeleka baadhi ya wagonjwa nje ya nchi wakiwa mahututi kabisa matokeo yake wakifika ama wanafikia ICU na baada ya siku moja au mbili wanafariki? Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanalishughulikia suala hilo ili kupunguza gharama ya kuwahudumia wagonjwa wale?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, wagonjwa wanaopelekwa nje wanakwenda wakiwa wamezidiwa, wanafariki, napenda kusema kwamba kama Daktari hawezi kusema kwamba huyu mgonjwa asitibiwe kama ameweza kukidhi vigezo vya kupelekwa nje. Kwa hiyo, sisi tunampeleka kumtibu, matokeo ya ugonjwa yanategemeana na mtu alivyopangiwa na Mwenyezi Mungu kuishi au kuondoka katika ulimwengu huu. Lakini sisi kama Madaktari ni wajibu wetu kuzuia kifo pale ambapo inawezekana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wapo wananchi wengi ambao wanakuwa na vigezo na wanapata ridhaa ya kwenda kupata huduma nje kutokana na huduma hizo kukosekana hapa, lakini wananchi hao wanakuwa hawana uwezo kifedha wa kuweza kusafirishwa nje na hivyo

wanalazimika kutembea mitaani kuomba msaada na wakati mwingine wanafariki wakiwa hawajaweza kupelekwa nje: Je, kwa kuwa ni haki ya Kikatiba ya kila mwananchi kupata huduma zote muhimu ikiwepo huduma ya afya, Serikali sasa iko tayari kuweka utaratibu mzuri utakaowawezesha kila mwananchi kuweza kupata huduma ya afya pale anapolazimika kupata?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna wagonjwa wanaozunguka mitaani wakiomba kuchangiwa fedha za kwenda kutibiwa nje. Mimi nimezungumzia kwenye jibu langu la msingi kwamba kuna vigezo ambavyo vinahitajika vifuatiliwe. Sasa kama mgonjwa hajaweza kukidhi hivyo vigezo inabidi aambiwe kwamba anatibiwa hapa nchini kwa sababu uwezo upo. Lakini wagonjwa wengine wanakataa, wanaamua kuzunguka wakiomba kwa sababu wanaamini kwamba wakipelekwa nje watatibiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba Madaktari wanapoamua kwamba unatibiwa hapa, ni kweli kuna uwezo wa kutibu na ndio sababu Serikali imejitoa kwa kiwango kikubwa kuanzisha hizo *Centre* mbili tatu, *Centre* ya Moyo, Mifupa pamoja na kusafisha figo.

Na. 5

### **Dawa za Kutibu Ugonjwa wa Kisukari**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa Kisukari umekuwa ni tatizo na unawapata watu wa rika zote, na kwa kuwa kumejitokeza wimbi kubwa la Waganga Asilia wanaojitangaza kuwa wanazo dawa zinazotibu ugonjwa huo:

Je, Serikali inawaeleza nini wananchi juu ya dawa hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo wa tiba asili, kuna dawa nyingi zinazotumika kudhibiti ugonjwa wa kisukari mwilini, kama ilivyo katika mfumo wa tiba ya kisasa.

Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) na Taasisi ya Tiba Asili iliyo chini ya Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya ya Jamii Muhimbili, hufanya utafiti wa kubaini aina mbalimbali za dawa za asili zinazosadikiwa kutibu magonjwa mbalimbali, ukiwemo ugonjwa wa kisukari. Matokeo ya tafiti zilizokwishafanyika, hayajaonyesha kuwa kuna dawa yoyote ya asili, yenye uwezo wa kutibu ugonjwa na kisukari, isipokuwa kudhibiti ugonjwa huo, kama ilivyo kwa dawa za kisasa.

Hivyo, wananchi wanashauriwa kuwa na tabia ya kwenda hospitali kupimwa afya zao ili kufahamu hali (*Status*) ya afya zao. Kisukari ni ugonjwa hatari sana usipodhibitiwa. Hivyo, mara wanapohisi kuwa na dalili za kisukari wanashauriwa kwenda kupima kabla ya kuanza matibabu ya kisukari.

Mheshimiwa Spika, Waganga wa Tiba Asilia wanashauriwa kuwasiliana na Taasisi za Utafiti ili kupata maelekezo yanayohusu ufanisi na usalama wa dawa wanazitumia kudhibiti ugonjwa wa Kisukari na dawa za magonjwa mengine. Dawa inapotangazwa kwenye vyombo vya habari, inatakiwa iwe imefanyiwa utafiti na kuthibitishwa kuwa ina uwezo wa kutibu ugonjwa husika na salama kwa mtumiaji. Kwa Waganga walio katika maeneo ya vijijini, wanashauriwa kuwasiliana na Waratibu wa Tiba Asili, waliopo katika Ofisi za Waganga Wakuu wa Wilaya, na katika kila Halmashauri. Waratibu hao wataweza kuwashauri namna ya kufanya mawasiliano na Taasisi za Utafiti kwa lengo la kufanyiwa utafiti dawa zao ili kuona kama zina uwezo wa kutibu na ni salama kwa mtumiaji.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kusisitiza kuwa, Waganga wa Tiba Asili nchini kote, watoe huduma hiyo kwa kuzingatia Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala, Na. 23 ya mwaka 2002, na kanuni zake. Waganga wa Tiba Asili, wawe na mawasiliano na Waganga Wakuu wa Mkoa na Wilaya, kupitia Waratibu waliopo ili kurahisisha uelewa wa mambo yanayohitaji ufafanuzi na miongozo katika ufanyaji kazi wao.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na kufanya utafiti wa dawa za kisukari, lakini kwa siku za hivi karibuni ongezeko la ugonjwa wa kisukari limekuwa zaidi kwa watoto ukilinganisha na miaka ya 1970. Napenda kujua: Je, Serikali imeshafanya tafiti yoyote kuhusiana na ugonjwa huu kwanini unawapata watoto wakati huu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwa kipindi cha sasa hivi magonjwa mengi yanaonekana kwamba yameongezeka kwa sababu kumekuwepo na uwezo wa kuweza kuyatambua *diagnosis facilities*. Lakini nashukuru kusikia kwamba haya maradhi yanaongezeka kwa watoto ambayo anasema ni hatari kwa afya ya mtoto. Naomba nimhakikishie kwamba kwa sababu Serikali tuna vitengo mbalimbali vinavyofanya uchunguzi na utafiti na sisi tuna taasisi yetu ya *NIMR*, basi nitakwenda kuwapa taarifa watogeneze mkakati wa kufuatilia

tuweze kuona ni kwanini watoto wadogo wanapata kisukari ambao ni ugonjwa hatari. Tufanye uchunguzi tujue chanzo chake, tujipange kuzuia watoto wasipate kisukari.

Na. 6

### **Kuhamishwa kwa Karakana ya Reli Tabora**

**MHE. ISMAIL A. RAGE** aliuliza:-

Kwanini Karakana ya Reli iliamishwa Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) ina Karakana kuu nne sehemu ya Makao Makuu Dar es Salaam (Gerezani), Morogoro na Tabora. Karakana ya Makao Makuu Dar es Salaam kazi yake ni kutengeneza, kuimarisha na kukarabati mabehewa ya abiria na mizigo. Karakana ya Gerezani kazi yake ni kutoa huduma ndogondogo na matengenezo ya kila siku, Karakana ya Morogoro kazi yake ni kutengeneza, kuimarisha na kufufua injini za treni zilizoharibika kwa njia ya kawaida au kwa kupata ajali. Karakana ya Tabora kazi yake ni kufanyia matengenezo injini zinazohitaji utaalum maalum (*required speciality*) ambazo ni za tabaka la 37xx 64xx na 65xx.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatayo:-

Karakana ya Tabora haijhamishwa na bado inaendelea na kazi zake zilizoelzwa hapo awali. Isipokuwa mwaka 2007 kulikuwa na zoezi la upunguzaji wa wafanyakazi kutoka wafanyakazi 6,500 na kubakiza wafanyakazi 3,320. Waliopunguzwa ni 3,180 katika kampuni ya *TRC* kabla ya kuvunjwa na kuundwa kwa *TRL*.

Hii imetokana na nafasi kisheria aliyopewa mwekezaji *RLTES* na kuchagua wafanyakazi ambao aliona wanafaa kuendelea na mkataba wa kazi kulingana na mahitaji ya wakati huo. Hivyo kulikuwa na upunguzwaji wa wafanyakazi katika karakana hiyo kwenye zoezi la ubinafsishaji.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini nataka kufahamu Serikali inachukua hatua gani kuimarisha Karakana ya Tabora kwa sababu pale Tabora ndiyo katikati ya kwenda reli zote kwa maana ya kwenda Mwanza, Kigoma, Mpanda anakotoka Mheshimiwa Waziri Mkuu?



**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mahitaji ya karakana yanahitajika na hivi sasa Serikali inafanya utaratibu wa kuongeza ufanisi wa kazi wa karakana hizi ili kukidhi mahitaji ya reli zinazokwenda Mikoa ya Kigoma, Katavi, Mwanza, Shinyanga na Dodoma.

Na. 7

### **Usafiri na Usafirishaji wa Treni**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. SAID AMOUR ARFI)** aliuliza:-

Kutokuwepo kwa usafiri wa kueleweka wa garimoshi kumezidi kuwa tatizo na kero kubwa kwa safari za kwenda Dar es Salaam:-

(a) Je, ni lini usafiri na usafirishaji wa garimoshi utarudishwa kwenye utaratibu wake wa awali?

(b) Je, ni lini usafiri watokeo Mpanda kwenda Dar es Salaam watapatiwa behewa lao maalum la daraja la tatu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kampuni ya *TRL* inakabiliwa na upungufu mkubwa wa mapato na vitendea kazi vikiwemo vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo na abiria na mitambo ya mawasiliano kutokana na uwezo mdogo wa kampuni. Hivyo kuathiri uwezo wake kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, ili kurudisha hali ya usafiri na usafirishaji wa garimoshi kwenye utaratibu wake wa awali, Wizara kwa kushirikiana na *RAHCO* na Menejimenti ya Mpito ya *TRL* imeandaa Mpango Biashara (*Business Plan*) ambao pamoja na mambo mengine unahusisha uboreshaji wa miundombinu ya reli, ununuzi na ukarabati wa injini na mabehewa, ununuzi wa mitambo na mashine za uendeshaji. Aidha, katika mpango huo kiasi cha Dola za Marekani milioni 335.95 sawa na shilingi bilioni 503.94 zitahitajika katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zitaiwezesha kampuni kununua injini mpya, kukarabati injini zilizopo, kuimarisha njia na kununua mitambo mpya ya mawasiliano na hatimaye kurudisha hali ya usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria kwenye utaratibu wake wa awali.

(b) Mheshimiwa Spika, treni za abiria kutoka Mpanda hufanya safari tatu kwa wiki na kwamba mabehewa ya abiria hufungwa kwenye treni za mizigo *mixed trains* hadi Tabora na kurudi tena baadaye. Hivi sasa *TRL* inafanya safari chache kwa wiki kati ya

Dar es Salaam na Kigoma kutokana na ukosefu wa fedha, vichwa vya treni na mabehewa pamoja na matatizo ya kiutendaji. Hii inamaanisha kwamba kwa zile treni mbili kati ya tatu za Mpanda wasafiri hawataweza kuunganisha safari kwenye kwenye treni ya Dar es Salaam kwa kuwa treni ya Dar es Salaam kwenda Kigoma hufanya safari chache kwa wiki.

Utaratibu uliopo ni kwamba abiria wa daraja la tatu kutoka Dar es Salaam kwenda Mpanga hukata tiketi za moja kwa moja ambapo wakifika Tabora wanaingia kwenye mabehewa ya treni ya Mpanda. Utaratibu huu pia hutumika kwa abiria wa daraja la tatu kutoka Mpanda kwenda Dar es Salaam. Abiria mwenye tiketi ya moja kwa moja anahakikishiwa nafasi ya kiti kwenye treni husika. Aidha, abiria kuhamia kwenye treni nyingine inaokoa muda mrefu unaohitajika kuhamisha mabehewa (*Shunting*). Hivyo utaratibu wa sasa wa abiria kuhamia kwenye mabehewa mengine utaendelea mpaka hapo Kampuni itakapoweza kununua injini na mabehewa ya kutosha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Je, Serikali inaweza kuwaambia Watanzania ni kwanini sasa hivi wafanyakazi wa Shirika la Reli wamegoma hivyo kuufanya usafiri kwa watu wa Kanda ya Magharibi kuwa mgumu ukizingatia barabara za lami?

Swali la pili: Je, kwanini Serikali ya Chama cha Mapinduzi siku zote imeshindwa kusimamia na kuendeleza mashirika yake mengi likiwemo Shirika la Reli na Shirika la Ndege Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, mgomo wa *TRL* tulikuwa na menejimenti ambayo viongozi wa mgomo ni *TRAWU*. Tulifanya mazungumzo nao kwa sababu walikuwa na maelezo kwamba Serikali iharakishe kuvunja mkataba na *RITES*. Lakini sisi Serikali tuliona tufuate taratibu za kisheria ili kuondokana na mkataba ule bila madhara yoyote.

Kuhusu swali la pili, tunafanya kila taratibu kufuata kanuni, taratibu na sheria ili migogoro isiendele.

**MHE. JOHN. M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Reli ndiyo uhai wa karibu zaidi ya watu milioni 10 ambao wanaunganishwa na reli mpaka Mwanza na Kigoma na ni zaidi ya biashara, ni huduma ya uchumi na huduma ya jamii. Je, Serikali ina mkakati gani wa sasa hivi na wa mbali kuhakikisha kwamba huduma hii inarudishwa na ili watu waweze wakaitumia kwa shughuli zao zi kiuchumi na Tanzania iweze kuendelea?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa muda mrefu Serikali ilikuwa inajaribu kuboresha Shirika letu la Reli. Katika jitihada hizo, tulikwenda mpaka tukafikia kutafuta mwekezaji tuwe nae katika kuliboresha Shirika hili. Mwaka 2007 tukaingia kwenye ubia na wenzetu wa *RITES* na tukavunja Shirika la Reli lililokuwepo *TRC* tukaanzisha *TRL* tukawa tuna hisa 49 na wawekezaji wakawa na hisa

51. Tulitegemea kwa kuingia katika ubia huo na kuwaleta wenzetu tushughulike nao, tushamiliane nao shirika hili litakwenda mbele, halikwenda mbele. Hivi tusemapo Serikali imechachukua hatua ya kukatisha mkataba wetu na *RITES* tunabaki sasa kumaliza zile taratibu za kutia saini mkataba ule uondoke. Baada ya hapo kazi kubwa tuliyonayo ni kuliboresha Shirika hilo.

Tunayo menejimenti ya mpito ambayo tunadhamiria kuwakabidhi shirika hilo waliendeshe. Kuna gharama za kufanya hivyo, sasa hivi tunahitaji bilioni 63 ili tufufue shirika. Katika kipindi kilichokwenda mpaka Desemba, wale tuliwakabidhi kuliendesha shirika hilo nikimaanisha menejimenti ya *RITES* walilifikisha shirika mpaka tukawa na usafiri wa garimoshi moja tu kwa wiki kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora na Kigoma na usafiri huo ulikuwa hauendi Mwanza. Mwezi Desemba tumeongeza sasa, tuna safari mbili na nia yetu ni kuwa ikifika Juni ziwe safari tatu na ikifika mwisho wa mwaka tuwe na safari angalau tano.

Na. 8

### **Matatizo Makubwa ya Maji Kawe**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Jimbo la Kawe ni miongoni mwa Majimbo yanayokabiliwa na matatizo makubwa ya ukosefu wa maji:-

- (a) Je, Serikali ina mipango gani ya muda mrefu na ya muda mfupi na wa kati ya kutatua tatizo hilo sugu?
- (b) Kama mipango husika ipo, utekelezaji wake utanza na kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Jimbo la Kawe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza tatizo la ukosefu wa maji katika Jimbo la Kawe, Serikali imeandaa mipango ya muda mfupi, wakati na muda mrefu. Mpango wa muda mfupi unahusu kuimarisha mfumo wa usambazaji, kupunguza uvujaji wa maji pamoja na kufunga dira kwa wateja wote wanaopata maji ili maji yanayozalishwa yawafikie watu wengi zaidi.

Kazi hii inaendelea, lengo ni kupunguza kiwango cha maji yanayopotea kutoka asilimia 50 ya sasa hadi asilimia 35. Pia Serikali kupitia *DAWASA* imepanga kutekeleza mradi huu kujenga mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 300 na kuunganisha wateja katika maeneo ya Tegeta, Ununio, Mbweni, *Bahari Beach*, Mivumoni, Boko, Bunju na Mpiji. Kazi hii itatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*).

Kazi ya usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni imekamilika. Ujenzi wa mradi utanza Julai, 2011 na kukamilika Julai, 2012. Serikali inatekeleza upanuzi wa mitambo ya Ruvu Chini kwa lengo la kuongeza uzalishaji maji kutoka lita milioni 180 hadi lita milioni 270 kwa siku. Kazi hii inagharimiwa na Shirika la *Millennium Challenge Corporation* ya Marekani kwa kiasi cha shilingi bilioni 31.5. Kazi inaanza mwezi Februari, 2011 na itakamilika mwezi Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda wa kati unahusisha pia ujenzi wa bwawa la Kidunda ili kuongeza uhakika na uendelevu wa upatikanaji maji katika vituo vya Ruvu Chini na Ruvu Juu. Kazi ya usanifu inandelea na itakamilika mwezi Juni, 2011. Mpango huo pia unahusisha upanuzi wa kituo cha Ruvu Juu. Ujenzi utanza baada ya kukamilika kazi ya usanifu wa miradi yote miwili.

Serikali kupitia *DAWASA* inatekeleza mradi wa maji ya visima katika eneo la Kimbiji na Mpera, katika Wilaya ya Temeke. Uchimbaji wa visima unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2011. Utakapokamilika mradi huu utaongeza upatikanaji wa maji Jijini Dar es Salaam kwa lita milioni 260 kwa siku. Kwa kuwa maeneo ya kusini mwa Dar es Salaam yatapata maji kutoka Mpera na Kimbiji, hali hiyo itaboresha upatikanaji wa maji Kaskazini mwa Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na Jimbo la Kawe maeneo ambayo yatahudumiwa na mitambo ya Ruvu Chini na Ruvu Juu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake. Kama yakitekelezeka mwaka 2015 watakaotaka kuja Kawe inabidi wakimbie. Swali la kwanza, kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea juu ya upanuzi wa bwawa la Ruvu Chini ambapo vilevile amesema kwamba mradi unatarajia kuanza Februari. Hii ndiyo Februari: Je, mradi umekwishanza?

Swali la pili, *DAWASCO* imekuwa na utaratibu katika maeneo mbalimbali ya kuingia makubaliano na watu ambao wanawavutia maji na hao watu wanafanya biashara ya maji ama kwa kutumia vioski au kwa njia nyingine zozote wakati watu ambao wamewazunguka hawapati huduma ya maji, hivyo kuuziwa maji kwa gharama kubwa sana. Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri anipatie majibu: Je, Serikali haidhani kwamba utaratibu huu ni kandamizi kwa Watanzania wa kipato cha chini na haioni kama imeweza kusogeza huduma ya maji kwa yule mtu mmoja anayefanya biashara? Ni busara yale maji kusambazwa kwa watu wanaozunguka hilo eneo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa Ruvu Chini, tunasema kwamba utanza Februari, lakini mpaka sasa Mkandarasi amekwishakabidhiwa *site* na mkataba umeshasainiwa. Kwa hiyo, utanza Februari, maana Februari hatujaamaliza. Kuhusu usambazaji wa maji ya *DAWASCO*, ikifika mwaka 2013 tatizo la maji Dar es Salaam litakuwa limekwisha kwa kiasi kikubwa kutokana na mipango ambayo tumeweka.

Mheshimiwa Spika, katika uhaba lazima kutakuwa na matatizo ya usambazaji. Lakini tukishakuwa na maji ya uhakika, hilo tatizo litakuwa limekwisha.

**Upatikanaji wa Maji Safi na Salama –Vunjo**

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA** aliuliza:-

Maji safi na salama ni uhai kwa wananchi na Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kupata ufumbuzi wa tatizo hilo kwenye Jimbo la Vunjo na kwingineko nchini:-

- (a) Je, ni Kata zipi na vijiji vipi kwenye Jimbo la Vunjo mpaka sasa vimepatiwa maji safi na salama?
- (b) Je, huo mradi wa maji utanza lini? Utakamilika lini? Utagarimu shilingi ngapi na mpaka sasa zimeshatumika shilingi ngapi?
- (c) Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni aliahidi kuchangia Sh. 150,000,000/- kwenye Mradi wa Maji Himo. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kata na vijiji vilivyopatiwa maji safi na salama katika Jimbo la Vunjo ni kama ifuatavyo:-

Kata ya Kirua Vunjo Mashariki, vijiji vinne (Mero, Kileo, Mrumeni na Nganjoni), Kata ya Kirua Vunjo Kusini vijiji vitano (Yamu Makaa, Yamu, Uparo, Uchira na Mabungo), Kata ya Kirua Vunjo Magharibi vijiji saba (Nduoni, Maruwa, Kanango, Kanji, Kwamare, Manu na Iwa), Kata ya Kahe Mashariki vijiji vitano (Ghona, Kyomu, Kochakindo, Kiterini na Soko), Kata ya Kahe vijiji vitano (Oria, Kisangesangeni, Ngasinyi, Mwangaria na Mawala) Kata ya Kilema Kaskazini vijiji sita (Makami juu, makami chini, Kyou, Rosho, Kimaroroni na Mkyashi), Kata ya Kilema Kusini vijiji sita (Legho Mulo, Marawe Kyaru, Masaera, Kilema Pofu, Kilema Mandaka na Kilototoni), Kata ya Mwika Kaskazini vijiji vitano (Lole, Marera, Msae Kinyamvuo, Mrimbo Uuwo, Maringa na Msae Nganyeni), Kata ya Mwika Kusini vijiji vitano (Kimangato, Kiriweni, Kondeni, Mawanjeni na Matala), Kata ya Makuyuni vijiji vitatu (Lotima, Kilimo na Makuyuni), Kata ya Mamba Kaskazini vijiji vinne (Mboni, Komakundi, Kokirie na Kotela) Kata ya Mamba Kusini vijiji vinne (Kiria, Mkolowonyi, Kimangara na Kimbogho) Kata ya Marangu Mashariki vijiji saba (Sembeti, Lyanrakana, Arisi, Lyasomboro, Samanga, Rauya na Mshiri), Kata ya Marangu Magharibi vijiji saba (Nduweni, Kyala, Mbahe, Komela, Komalyangoe Kitowo na Kiraracha) Orodha ya majina ya vijiji ipo na kwa sababu ya muda naomba viorodheshwe kwenye Hansard.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya maji katika vijiji upo katika viwango tofauti. Vijiji nilivyovitaja vya Kata za Kahe Mashariki na Kilema Kusini vitapata kikamilifu huduma ya maji safi na salama ifikapo mwezi Desemba, 2011 kupitia Mradi wa Maji wa Kirua Kahe unaoendelea kutekelezwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya Moshi Vijijini imeteua vijiji 12 katika utekelezaji wa mpango wa maji na usafi mazingira vijijini ambavyo ni Matala, Mawanjeni, Kilimo Makuyuni, Makame Juu, Makame Chini, Boro, Mwasi Kaskazini, Mwasi Kusini, Korini Kusini, Mande, Njari na Ongoma. Kati ya hivyo 12, vijiji vitano ambavyo ni Matala, Mawanjeni, Kilimo Makuyuni, Makame juu na Makame chini viko katika Jimbo la Vunjo.

Fedha ambazo Serikali imetoa kwa Halmashauri ya Moshi Vijijini kuanzia Julai, 2009 hadi Juni, 2010 ni Sh. 323,340,850/- kwa ajili kazi ya upimaji na usanifu wa miradi katika vijiji husika. Zabuni kwa ajili kupata wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji yameandaliwa. Gharama za ujenzi vitafahamika baada ya kupata mshindi. Ujenzi wa miundombinu unatarajiwa kuanza mwaka huu 2011.

(c) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji katika mji mdogo wa Himo unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Maji chini ya programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Ujenzi wa chanzo cha maji Mananga umefanyika kwa asilimia 60 na maji yameshafika kwenye mantenzi ya Merisini. Ununuzi wa mabomba ya kusambaza maji kilomita tano kati ya kilomita 16.5 umefanyika. Mpaka sasa mradi umegharimu Sh. 253,190,610/-.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni ameahidi kuchangia shilingi milioni 150 kwa ajili ya mradi wa Himo. Fedha hizo zitatumika kukamilisha kazi zifuatazo:- Kununua mabomba makubwa yenye urefu wa kilomita sita kwa ajili ya mtandao wa maji, mita za maji na vituo vya kuchotea maji.

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu yake mazuri, naomba kuuliza maswali mawili nyongeza.

Wakati wa kusimamia mradi wa Kirua Vunjo Kahe, wananchi walihamasishwa wachimbe mitaro, walaze mabomba na wakaahidiwa kwamba kila mita moja ambao walifanya kazi watalipwa Sh. 6,000/- lakini mpaka sasa sijui umefikia wapi na kama hizo fedha walizoahidiwa ni za kweli na watalipwa lini?

Swali la pili, wakati mradi huo wa Kirua Vunjo Kahe, tulikuwa na mradi wetu wa maji asili. Tulikuwa tunatumia bomba za zamani lakini bomba hizo ziling'olewa, wananchi walikuwa wanapata maji bure, sasa bomba hizi mpya maji wanauziwa. Wanataka kujua zile bomba zao ziko wapi na kama watapewa fidia kwa ajili ya zile bomba.

**NIABU WAZIRI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa maji ambao tunaendeleza kule Kahe utaratibu ni kwamba miradi yote hii tumeifanya iwe shirikishi. Ni lazima wananchi watoe mchango aidha, kwa kuchangia fedha au kwa kufanya nguvu kazi. Kwa hiyo, mchango wa kuchimba mitaro na kulaza mabomba ndiyo mchango wa wananchi katika mradi ule. Kwa hiyo, hakuna fidia ya Sh. 6,000/- ambayo itatolewa. Tunawashukuru sana wananchi wa Vunjo Mashariki wameelewa hilo.

Mheshimiwa Spika, mabomba ambayo yameng'olewa ambayo ni ya zamani yametunzwa na mradi, sio kwamba yamepelekwa mahali pengine. Ni kwamba kuna maeneo mengine tunayatumia katika kuongeza kama maeneo ambayo unahitaji kuilinda lile bomba jipya unaweka lile la zamani katikati. Kwa hiyo, mambo yale yanaendelea kutumika kwa faida ya mradi na kuhusu na kuhusu kuuziwa maji ndiyo Sera ya Maji kwamba maji lazima yachangiwe kidogo ili kuwe na Mfuko wa Maji ili ule mradi uendelee hata kama *cork* imeharibika waweze kununua. Kwa hiyo, hilo ni jukumu ambalo wananchi ni lazima waone ule mradi ni wa kwao na waweze kuilinda.

Na. 10

### **Tishio la Mamba Katika Mto Ruvuma**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Wananchi wengi wa Jimbo la Lulindi hasa vijiji vinavyopakana na Mto Ruvuma katika Kata za Mnavira, Mchauru, Sindano na Chikoropola wamepoteza maisha na wengine kupoteza viungo kutokana na kushambuliwa na Mamba waliozaliana kwa wingi katika Mto Ruvuma:-

Je, Serikali inafanya juhudi gani za haraka kutafuta wawindaji wa kupunguza mamba hao ambao wamekuwa tishio kwa wananchi wanaotegemea mto huo kwa kupata maji ya kunywa, uvuvi na kilimo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo: Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali za Wilaya pamoja na sekta binafsi inafanya jitihada mbalimbali na za haraka katika kutafuta njia sahihi na muafaka za kuzuia tatizo la mamba ambao wamekuwa tishio kubwa kwa wananchi wanaotegemea Mto Ruvuma katika kukidhi mahitaji yao.

Kwa kawaida, Wizara hutuna watalaam katika maeneo yaliyoathiriwa na wanyama hao pamoja na kutoa leseni kwa kampuni binafsi kwa ajili ya kazi ya kuwinda mamba. Kampuni hizo za uwindaji zimekuwa zikipangiwa maeneo mbalimbali ya kuwinda kwa kuzingatia taarifa ambazo Wizara yangu inazipata kuhusu kuwepo kwa matukio ya watu kuuwawa au kujeruhiwa.

Mwaka 2010 Wizara ilipata taarifa ya matukio ya uharibifu unaofanywa na Mamba katika maeneo ya Kata za Jimbo la Lulindi zilizo kandokando ya Mto Ruvuma. Kwa kuzingatia uzito wa tatizo hilo, Wizara ilitoa kibali cha kuvuna Mamba kwa kampuni ya *New Sanje Sugar Estitate*. Kampuni hiyo ilifanikiwa kuvuna Mamba 41.

Hata hivyo, mwishoni mwa mwezi Januari na mwanzoni mwa mwezi Februari, Wizara ilifanya msako wa kukabiliana na madhara yanayosababishwa na mamba kwa wananchi wanaoishi katika vijiji vilivyoko kandokando ya Mto huo. Msako huo ulifanyika kwa kushirikiana kati ya Menejimenti ya Pori la Akiba la Lukwika, Lumesule, Msanjesi pamoja na Waheshimiwa Madiwani kutoka Kata za Mnavira, Mchauru, Sindano, Lipundulu na Chikoropola. Hata hivyo, kutokana na kina cha maji ya Mto huo kuwa kikubwa sana, hakuna Mamba ambaye ameuwa hadi sasa. Msako unaendelea.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, nikubaliane na shughuli inayofanywa hivi sasa ya Watalaam wa Maliasili na Waheshimiwa Madiwani ambayo ni kupata tathmini ya athari zilizotokana na mamba hawa ambao wamekuwa tishio kwa wananchi. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa haraka kuhakikisha kwamba mamba wale wanavuliwa ili wananchi waishio kandokando ya Mto Ruvuma waweze kuishi kwa amani na kuweza kufanya shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, la pili; nimuulize Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa suala hili ni tishio na wananchi wengi wanakufa na kupoteza viungo vyao: Je, Mheshimiwa Waziri atafanya ziara lini ya haraka ili kuja kuona hali halisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba ujibu kwa kifupi maana tuko nyuma kabisa ya ratiba.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tatizo lipo, lakini kwa upande wetu sisi tunaendelea na jitihada za kusaka hao mamba. Kwa sasa tumeongeza watalaam, mwanzo tulikuwa na watalaam wachache, lakini kwa kuwa bado hatujafanikiwa kutokana na kina cha maji kuwa kimeongezeka, tumeamua kuongeza watalaam wengine wakati huo tukiwaomba wananchi wawe wanatoa taarifa za mapema na wenyewe kuchukua tahadhari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufanya ziara kwenye eneo hilo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafanya ziara mapema iwezekanavyo ili kuona hali ilivyo na kuweza kuona hatua za kuchukua.

Na. 11

**Uvuvi Katika Mabwawa Yaliyoko Kwenye Mbuga ya Selous**



**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI** aliuliza:-

Hifadhi ya Taifa ya ya Selous iliyoko Rufiji ni maarufu kwa utalii na uvunaji wanyama walioko kwenye hifadhi hiyo, na pia ndani ya hifadhi hiyo yapo mabwawa yenye samaki ambapo zamani watu waliruhusiwa kuvua samaki, lakini kwa sasa wanazuiwa kuvua:-

Je, kwa nini Serikali imezuia watu kuvua samaki kwenye mabwawa hayo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Pori la Akiba la Selous lina mabwawa yaliyoko kandokando ya Mto Rufiji. Hata hivyo, umuhimu wa mabwawa haya unatokana na sababu kuwa maeneo hayo ndiyo kivutio kikubwa cha utalii wa picha ambao umekuwa ukiongezeka kwa kiwango cha kuridhisha na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

Vile vile mabwawa haya ni mazalia, makulio na maficho ya samaki ambayo husaidia uwepo samaki katika maeneo yaliyo nje ya Hifadhi ya Pori la Akiba la Selous. Aidha, mabwawa haya ndio tegemeo la wanyama kwa ajili ya kujipatia maji hasa kipindi cha kiangazi. Umuhimu wa mabwawa haya unafanana sana na umuhimu wa Hifadhi ya Mahale iliyoko Mkoani Kigoma ambayo pia ni mazalia na makuzio ya wanyama, samaki katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shughuli za utalii wa picha hufanyika wakati wa kiangazi ambapo vile vile ndicho kipindi muafaka cha uvuvi, ni dhahiri kuwa kutakuwa na mgongano wa shughuli za uvuvi na utalii zinazoweza kuleta athari kwa upande mmojawapo. Haiyumkini mabwawa hayo ni maarufu kwa kuwa na idadi kubwa ya mamba wanaopatikana katika huo Mto, hivyo pia kuruhusu uvuvi kwenye maeneo hayo ambayo sasa mamba wameongezeka kwa kiasi kikubwa sana kunaweza kuleta maafa. Wizara yangu imeona ni vizuri kutenga fedha katika bajeti yake ili kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuweza kuhamasisha wananchi wa vijiji jirani waweze kuchimba mabwawa na kufuga samaki nje ya Pori la Akiba.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mabwawa haya yalizuliwa kuvuliwa tangu miaka ya 1977, hadi leo Waziri ndio anatamka kwamba Wizara yake ina mpango wa kupanga bajeti kwa ajili ya kwenda kuchimba mabwawa mbadala ya uvuvi: Je, Waziri anayo habari kuwa watu wanapojaribu kwenda kuvua katika mabwawa haya huwa wanauwawa? Je, huu si ukiukwaji wa haki za binaadamu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri ametamka kwamba Selous inaingiza fedha za kigeni: Je, wananchi wanaozunguka maeneo yale huwa wananufaika vipi na fedha hizi katika huduma za kimsingi kama afya, elimu na maji? Naomba majibu Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba hakuna mtu yeyote ambaye anaruhusiwa kuuu binadamu mwenzake na matukio kama yamekuwa yakitokea labda yawe yanasababishwa na wanyama. Lakini, kama ni kuuwawa kwa maana ya kuuwawa na askari, jambo hilo haliruhusiwi, ni kinyume cha sheria na huwa tunachukua hatua mara moja pale panapotokea tukio la namna hiyo. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba pengine ni vizuri tukawasiliana anipe *specific cases* za watu ambao wameuwawa na kama wameuwawa na askari wa kwetu, tuweze kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu namna ya kusaidia wananchi ambao wako pembezoni mwa pori hili, kwa sasa, Wizara imekuwa ikitoa asilimia 25 ya mapato yanayotokana na Uwindaji wa kitalii. Kwa bahati mbaya sina takwimu hapa, lakini Wilaya ya Kilwa, Wilaya ya Rufiji na Wilaya zote ambazo ziko pembezoni mwa Pori la Akiba la Selous ni wanufaika wakubwa sana wa fedha hizo. Labda cha kuzungumzia ni kwamba labda tuongeze jitihada, lakini angalau kutoa tumekuwa tukifanya hivyo.

Na. 12

**Maamuzi ya Uuzwaji wa Kampuni ya Celtel  
kwa Zain na Baadaye Airtel**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Serikali iliingia ubia na Kampuni ya *MSI* ya Uholanzi kuunda Kampuni ya Simu za Mkononi ya *Celtel*, Kampuni hiyo ya *Celtel* imeuzwa kwa Kampuni ya Zain na baadaye Zain kuuzwa kwa Kampuni ya *Airtel*:-

- (a) Je, Serikali imekuwa na maamuzi yoyote katika uuzwaji huo?
- (b) Je, Serikali imefaidika na nini katika uuzwaji huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalasa, Mbunge wa Lupa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali iliingia ubia na Kampuni ya *Mobile Systems Cellular Investment (MSI)* ya Uholanzi ambayo ilijulikana kwa jina la *Celtel International* kama jina la kibiashara. Katika kuendesha Kampuni ya Simu za Mkononi ya *Celtel Tanzania Ltd.* kwa uwiano wa hisa wa asilimia 40 na 60 sawia. Mwaka 2005 Kampuni ya *Mobile Telecommunication Company – KSC (Zain Group)* ya Kuwait ilinunua hisa za *Celtel International BV* ambayo ilikuwa inamiliki *Celtel Africa BV* kwa asilimia 100. *Celtel Africa BV* nayo ilikuwa ikimiliki *Celtel Tanzania BV* kwa asilimia 100 ambayo nayo ilikuwa na hisa asilimia 60 katika Kampuni ya Simu ya *Celtel Tanzania*. Aidha, baada ya mauzo hayo, jina la *Celtel* likabadilika kuwa *Zain*. Kwa maana hiyo, *Celtel* ya Tanzania ikawa na ubia na *Zain Tanzania BV* ndani ya *Zain Tanzania Ltd.* ambayo sasa inaitwa *Airtel* kutokana na *Zain Africa BV* kununuliwa na *Airtel* ya India. Aidha, Serikali ilipewa taarifa juu ya mauzo hayo, lakini haikuwa na maamuzi juu ya mauzo hayo kutokana na makubaliano ya mkataba katika ubia hususan pale mauzo yanapofanyika kwa ngazi ya Kampuni Tanzu (*Parent Company*), kwani mauzo hayo hayakuathiri hisa za wabia katika nchi husika.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na mchakato wa uuzaji wa Kampuni ya Simu ya *Celtel* kwenda *Zain* kama nilivyosema katika kipengele (a), mwaka 2010, Kampuni ya Simu ya *Zain* ambayo ilikuwa ikimilikiwa kwa pamoja kati ya Kampuni ya *Zain Tanzania Ltd.* na Serikali ya Tanzania kwa uwiano wa hisa asilimia 60 na 40 sawia, iliuzwa na kubadili jina kuwa *Airtel* kutokana na Kampuni ya *Zain Africa* iliyokuwa ikimiliki makampuni mbalimbali Afrika ikiwemo *Zain Tanzania* kuuzwa kwa *Airtel Africa* ambayo nayo iliendelea kumiliki sehemu ya hisa ambazo ni asilimia 60 katika *Airtel Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa uuzaji baina ya Kampuni hizo ulihusisha makampuni husika katika Afrika yote. Serikali haikunufaika kutokana na uuzaji huo, bali kama mmiliki wa hisa kwa kiwango cha asilimia 40 katika iliyokuwa *Celtel Tanzania*, *Zain Tanzania* na sasa *Airtel Tanzania*, Serikali itaendelea kupata gawio lake la kila mwaka linalotokana na faida ya uendeshaji wa Kampuni ya *Airtel Tanzania*. Mpaka sasa Serikali imekwishapokea gawio la mwaka 2007, 2008 ambapo mchakato wa kupata gawio la mwaka 2009 bado unaendelea kutokana na Kampuni mpya ya *Airtel* kufanya tathmini ya mali ilizonunua. Aidha, Serikali pia inaendelea kunufaika na uwepo wa Kampuni hii kutokana na nafasi za ajira mbalimbali na misaada mbalimbali ya kijamii ambayo imekuwa ikitolewa na Kampuni hii iliyokuwa *Celtel*, *Zain* na sasa *Airtel*.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye Rais alituambia jina lake lingine ni “Mawe Matatu”, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, *Celtel Tanzania*, Serikali ilikuwa na asilimia 40, imekwenda *Zain* Serikali ina asilimia 40, *Zain* inauzwa inakwenda *Airtel* bado Serikali ina hisa asilimia 40. Pale ambapo mwenye 40 percent unakuwa huna usemi kwenye kuuzwa kwa kampuni hiyo, ina maana kwamba mkataba huo una matatizo. Je, Mheshimiwa Waziri analihakikishia Bunge hili kwamba Wizara yake itaangalia upya mkataba huo?

La pili, sheria zetu zilizopo hapa Tanzania, hisa ambazo zimesajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (*Dar es salaam Stock Exchange*) zimekuwa *exempted* kulipa kodi. Hizi hisa za *Celtel Tanzania* au *Zain Tanzania* hazikuwa *listed* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*. Je, walipouza hisa hizo walilipa kodi zinazopaswa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua hii ni biashara, huyu mtu ana hisa na mna mkataba naye ana asilimia 60 na wewe una asilimia 40 na amepata mtu atakayeweza kununua hizo hisa akapata faida, na wewe hachukui hisa zako akaziuza, unaendelea kubaki nazo. Kulingana na mkataba uliopo, anakupa taarifa na yeye anaweza kuuza hisa zake, lakini wewe unaendelea kubaki na hisa ulizo nazo. Ndivyo Serikali yetu ilivyoendelea na ndiyo sababu *Airtel* imekua zaidi na wananchi wengi wanapata ajira na inachangia zaidi kwenye pato la Taifa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hisa zilizosajiliwa kulipiwa kodi, kwa kawaida hisa zinazonunuliwa zinaendana na utaratibu wa kisheria, sheria zote zilifuatwa katika kuuza hisa hizi na kwamba hisa zetu sisi kama Serikali ya Tanzania zimeendelea kubaki kama zilivyo.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu wa kuuliza maswali, kifungu gani?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 46(1).

**SPIKA:** Eeh, soma!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** “Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa, isipokuwa kwamba kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi, Waziri atampa Mbunge mwuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza kabla ya muda wa kujibu swali hilo haujafikiwa.”

Mheshimiwa Spika, Waziri ameulizwa swali kama kodi zilizotakiwa kulipwa kisheria zimelipwa. Hajajibu hilo swali?

**SPIKA:** Aliyeuliza swali hajasema hivyo. Tunaendelea. Mheshimiwa David Kafulila, swali linalofuata.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu; ile ile, hapana, hatufanyi mara mbili.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Hapana.

**SPIKA:** Wewe, kuhusu nini sasa? Mheshimiwa Kafulila swali linalofuata!

Na. 13

### **Mawasiliano ya Simu Wilaya ya Uvinza**

**MHE. KAFULILA DAVID** aliuliza:-

Karibu nusu ya eneo la Wilaya mpya ya Uvinza halina mawasiliano ya simu: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mtandao wa simu za mikononi unafikishwa kwenye maeneo hayo ambayo yana Kata za Kalya, Bahingu, Igalula, Sigunga na Sunuka?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kafulila David, Mbunge wa Kigoma Kusini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, inatambua umuhimu wa kuwepo huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo yote nchini, hii ni kutokana na ukweli kwamba huduma za mawasiliano zenye ubora na uhakika hurahisisha mawasiliano katika maendeleo ya shughuli za kijamii na kiuchumi. Kwa mfano, hivi sasa wananchi wanaweza kutuma na kupokea pesa, kulipa ankara za huduma mbalimbali kwa kutumia simu za mikononi, kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba mawasiliano ni chachu ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kafulila David, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali imekuwa ikisisitiza makampuni ya simu nchini kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya mpya ya Uvinza.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Zantel* imeahidi kufanya utafiti wa kimasoko katika maeneo ya Kata ya Kalya, Buhingu, Igalula, Sigunga na Sunuka katika mwaka wa 2010 ili kuangalia uwezekano wa kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Airtel* tayari imeanza jitihada za dhati kabisa za kufikisha mawasiliano katika Kata ya Kalya, Buhingu, Igalula, Sigunga na Sunuka ambapo katika hatua za awali Kata ya Sunuka katika eneo la Kilando tayari limekwishafanyiwa ukaguzi wa kiufundi na limo katika mpango wa utekelezaji katika mwaka 2011. Aidha, Kata nyingine katika Wilaya ya Uvinza zinatarajiwa kufanyiwa ukaguzi wa kiufundi hivi karibuni ili ziweze kuboreshewa huduma ya mawasiliano katika mwaka wa 2011.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuwahakikisha huduma za mawasiliano zinawafikia wananchi wote nchini, Serikali tayari imeanzisha Mfuko wa Mawasiliano

kwa Wote (*Universal Communication Access Fund - UCAF*) ambapo kupitia mfuko huu Serikali itashirikiana na makampuni ya mawasiliano nchini ili kufikisha huduma za mawasilino hata katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa wawekezaji ili kila mwananchi popote alipo aweze kupata huduma ya mawasiliano.

**MHE. KAFULILA DAVID:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, ndani ya majibu yake, hajapata kueleza ni kwa nini eneo hilo ambalo ni takriban nusu ya Wilaya halina mawasiliano ya simu zaidi ya kueleza michakato mbalimbali ambayo Serikali au kupitia makampuni hayo wanashughulikia. Lakini, katika maelezo hayo hayo, amegusia tu kidogo kwamba kuna dhana ya soko kama kikwazo cha kufikisha mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo. Sasa, ningependa kufahamu pengine kama kigezo ni soko, ni kwa kiasi gani eneo hilo ambalo lina wakazi zaidi ya 200,000 ni soko dogo kiasi cha kuwezesha pengine makampuni hayo ama yenyewe au kwa ushirika na Serikali yashindwe kufikisha mawasiliano katika eneo hilo. Hilo moja.

Lakini la pili,...

**SPIKA:** Basi, umemaliza maswali mawili. Maswali mawili tu. La kwanza umesema kwa nini hamkuona na soko hilo na pili kwamba kuna watu wengi pale. Kwa hiyo, ni maswali mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kuweka mnara au kuweka mawasiliano unapitia katika sehemu tano:- Ya kwanza ni kuangalia hali ya kibiashara, watu walioko pale na uwezo wao wa kulipa. Pili, wakishaona kwamba ile inafaa, wanakwenda hatua ya pili kukagua eneo hilo kuona kama ni sehemu gani ambayo inaweza kuwekewa mnara ili mawasiliano yaweze kupatikana. Sehemu ya tatu inaangalia kama mnara unaweza kupatikana, *then* wanaanza kuangalia ni katika eneo gani ambapo wanaweza kununua eneo na kusimika huo mnara ili kuweza kusambaza mawasiliano katika eneo hilo. Baada ya hapo, ujenzi unaanza na ujenzi ukishafanyika, basi hapo ndipo mnara utakuwa *commissioned*. Kwa sababu hiyo, basi mchakato huo ulivyokuwa mrefu ndio sababu ilichukua muda katika eneo hili la Uvinza kuweza kupata mawasiliano.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Taarifa tena! Haya.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Ndiyo!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri wa Mawasiliano akijibu swali Na.12 la Mheshimiwa Mwambalasa, ametoa maelezo ya utaratibu ambao hisa za kampuni moja kwenda kampuni nyingine zinavyokwenda na

taratibu za kikodi zinavyotakiwa kuwa. Maelezo aliyoyatoa sio sahihi kwa sababu *Zain Tanzania Ltd* imesajiliwa Tanzania, ni kampuni ya ki-Tanzania yenye asilimia 60 za wageni.

Wakati hisa hizi zinazwa, inapaswa wale wageni wanao-*transfer* ile *ownership* walipe *Capital Gains Tax*. Mpaka tunapozungumza, *Zain Tanzania Ltd* ilipobadilisha *transfer* kwenda *Airtel* hatujalipwa *Capital Gains Tax* ya thamani ya *Zain Tanzania Ltd*. Wenzetui wa Nigeria, Gabon, Sudan wamelipwa *Capital Gains Tax*. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri asahihishe kauli yake kwamba utaratibu uliofanyika wa Tanzania ndio sahihi. Tatizo ni kwamba utaratibu wa Tanzania umekiuka mazingira ya kibiashara yanavyopaswa kuwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa utaratibu, taarifa inatolewa wakati ule anaposimama kusema suala lenyewe. Sasa hii taarifa aliyofanya Mheshimiwa Zitto, anaweza kuileta tena ikajibiwa vizuri zaidi kwa sababu unaweza kusema kwamba swali fulani lilipojibiwa, sikuridhika kwa sababu moja, mbili, tatu. Kwa hiyo, maelezo kama ulivyoeleza, halafu utajibiwa kwa utaratibu, siyo wakati huu.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona kwamba tulipaswa kumaliza maswali yetu saa 4.30, lakini mtakumbuka kwamba tulianza na kuapisha wenzetu. Kwa hiyo, tumechukua muda ule, tumelipia pale, lakini sasa tena muda umekwisha, maswali yamebakia ya Wizara ya Nishati na Madini, yatapangwa tena wakati mwingine. Kwa hiyo, tulichojifunza hapa ni kwamba asilimia kubwa sana maswali yaliulizwa vizuri na Wabunge, lakini maswali ya nyongeza ni marefu mno, hivyo hivyo na Mawaziri majibu ya nyongeza ni marefu mno, ndiyo yaliyokula muda wetu.

Kama nilivyowaelezeni, swali na maswali ya nyongeza yote ni dakika tano tu. Kwa hiyo, tuendeleo kujifunza na ndiyo maana nimewaacha wengi kuwaambia kwamba msimame kwa sababu tunajifunza. Kwa hiyo, tuendeleo kujifunza. Kwa hiyo, kipindi cha maswali tumemaliza lakini maswali yamebaki.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Kanuni gani?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7), lakini Kanuni ninayotaka kuomba mwongozo wako ni Kanuni ya 39(8). Kwamba “Bunge linapovunjwa, maswali yote ambayo hayakuwahi kujibiwa yatajibiwa kwa maandishi”. Mheshimiwa Spika, Bunge la Tisa lilipokuwa linavunjwa yalibaki maswali mengi sana. Naamini Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwepo Bunge hilo la Tisa pamoja na mimi tuliandika maswali mengi, hayakujibiwa na Bunge likatayarisha Kitabu cha Maswali ambayo hayakujibiwa. Sasa ninaomba mwongozo wako:-

Je, isingekuwa busara, badala ya Wabunge wale kuanza kurejea na kuuliza maswali yale upya, kwa sababu Serikali ni ile ile na maswali mengine bado yako *valid*,

kwa nini Serikali isiyajibu na kuwapatia Wabunge wale kama nilivyosema tusianze kuyarejea tena, tukaendelea na maswali mengine? Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, tungejifunza. Hata Miswada iliyosomwa Mara ya Kwanza Bunge lililopita inabidi isomwe Mara ya Kwanza tena, sembuse maswali! Kwanza, hatujui hata wanaotakiwa wajibiwe, wengine wameshaondoka. Asilimia 70 ya Wabunge walioko hapa ni wapya. Asilimia 70 ni wapya na wenyewe wana maswali yao mengi kabisa.

Kwa hiyo, maswali yote yaliyokuwa ya Bunge la Tisa kama waliohusika hawakupewa majibu, kwanza wengine hawapo, kwa hiyo, tunayafuta, tumeyafunga, wala hatuyagusi tena, wala Wizara msihusike nayo. Mtahusika na yale tu tuliyovaliteeni sasa.

Ila kama nilivyosema, ulizeni maswali kwa kifupi, Mawaziri jibuni kwa kifupi, tutapata muda mwingi sana wa kuuliza maswali mengi ya nyongeza na kipindi kinakuwa *live*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, yale maswali bahati mbaya, kama unataka uliza tena.

#### **KAULI ZA MAWAZIRI**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimwa Spika, katika hotuba ya Salaam za Mwaka Mpya za Rais tarehe 31 Desemba, 2010, Mheshimiwa Rais aliwafahamisha wananchi kwamba Serikali imedhamiria miongoni mwa mambo mengine kuanzisha mchakato wa kuitazama upya Katiba ili hatimaye tuwe na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoendana na Taifa lenye umri wa nusu karne.

Mheshimiwa Rais alibainisha juu ya umuhimu wa kuitazama upya Katiba ya nchi na nia yake ya kuunda Tume Maalum ya Katiba itakayokuwa na wajumbe kutoka pande zetu mbili za Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais alieleza kwamba jukumu la msingi la Tume hiyo litakuwa ni kuongoza na kuratibu mchakato utakaoshirikisha wananchi wote bila kubagua, Vyama vya Siasa, wanasiasa, wafanyabiashara, asasi za kiraia, mashirika ya dini, wanataaluma na makundi mbalimbali ya watu nchini kote katika kutoa maoni yao kuhusu Katiba ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, tarehe 5 Februari, 2011 wakati Mheshimiwa Rais akihutubia kwenye sherehe za Chama cha Mapinduzi za kutimiza miaka 34 alisema, miongoni mwa mambo ambayo tutayafanya mwaka huu kuelekea kwenye kilele cha maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa nchi yetu ni kuanzisha mchakato wa kuitazama upya Katiba ya nchi yetu kwa nia ya kuihuisha na hatimaye kuzaa Katiba mpya inayolingana na Taifa lenye umri wa miaka 50 na itakayotupeleka kwenye miaka mingine 50 ijayo.



Mheshimiwa Rais aliwahakikishia wananchi kuwa Serikali ya CCM ni miongoni wa wadau wakubwa wanaotaka Katiba ihuishwe ili kukidhi mahitaji ya wakati tulionao na matarajio ya Watanzania ya baadaye. Alisema kuwa sisi sote ni wadau wa mabadiliko ya Katiba yetu ya sasa.

Hata kama kusingekuwepo mapendekezo ya *CUF*, *CHADEMA* na vyama vingine vya siasa na wengineo wote, ilikuwa ni dhamira ya Serikali inayoongozwa na CCM kufanya mabadiliko ya Katiba ya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitumia nafasi hiyo kuwasihi wananchi kuwa na utulivu na subira. Vile vile aliwaomba Watanzania wote kuwa wakati huo ukifika, wajitokeze kwa wingi katika kutoa maoni na kupiga kura ya maoni itakayoidhinisha Katiba hiyo. Katiba ni mali ya wananchi, hivyo tunataka tuwashirikishe kwa ukamilifu katika hatua zote muhimu.

Mheshimiwa Spika, historia ya nchi yetu haitengani na ile ya Katiba ya nchi yetu, inatosha kwa sasa kusema tu kwamba Katiba hii tuliyonayo imetufikisha hapa tulipo salama, tumepita katika mambo mengi makubwa tangu uhuru wetu, Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, Mfumo wa Chama kimoja, Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, Muungano baina ya nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa na mambo hayo na mengine mengi yaliifanya nchi yetu kuheshimiwa na kuaminiwa ndani ya nchi na Jumuiya ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyoifanya nchi yetu kuwa tulivu ya amani na iliyokuwa kimbilio kwa wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika na watu wengine waliokimbilia hapa kwa sababu ya udhalimu au machafuko katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, Katiba hii ndiyo inayotuwezesha kuishi pamoja kwa udugu kwa kuheshimiana na kupiga hatua katika juhudi zetu za kujenga Taifa lenye umoja na maendeleo ya watu. Hivi sasa ni miaka hamsini tangu tulipopata uhuru, tulipopata Katiba mpya ya uhuru iliyotokana na mazungumzo baina ya Serikali ya Uingereza iliyokuwa na udhamini wa Utanganyika na viongozi Wazalendo waliokuwa wanadai uhuru wa nchi hii. Aidha, Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wetu yanatimiza miaka 34. Bila shaka wote tunatambua mabadiliko mengi yaliyotokana na matukio kadhaa katika nchi yetu, kwa msingi huo, Serikali imedhamiria kuanzisha mchakato wa kuitazama Katiba yetu upya ili hatimaye tuwe na Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoendana na mahitaji, mabadiliko na matarajio mapya ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari juu ya namna nzuri ya kuendesha mchakato huu, katika kuandika Katiba ya sasa, hati ya Muungano inayojulikana kama *Articles of the Union*, Rais alipewa mamlaka ya kikatiba ya kuwateua wajumbe wa Tume ya Katiba kwa ajili ya kuandaa mapendekezo ya Katiba ya Kudumu. Majina ya wajumbe hao yalitangazwa kwenye gazeti la Serikali namba 38 la mwaka 1977. Aidha, Rais aliwateua wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria (*Constituency Assembly*) kutoka pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa mabadiliko katika Katiba yetu mwaka 1983 na mwaka 1984, Rais aliunda Tume na kuwateua Wajumbe wa Tume, Tume iliratibu maoni ya wananchi kwa kupokea barua za waliowasilisha maoni kwa njia ya barua kwa kushiriki katika kongamano, midahalo na mikutano ya hadhara ili kupokea maoni ya wananchi. Baada ya hatua hiyo Tume iliyoteuliwa na Rais iliwasilisha mapendekezo kwa Rais na Muswada wa mabadiliko ya Katiba uliandaliwa na kuwasilishwa Bungeni kwa kufuata utaratibu ulioainishwa katika Ibara ya 98 ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na majadiliano katika jamii kuhusu mabadiliko katika Katiba ya nchi, Rais kwa njia ya kiutawala aliunda Tume ya Jaji Nyalali mwaka 1991 na Kamati ya Jaji Kisanga mwaka 1998 ambazo ziliratibu maoni ya wananchi na baadaye kuwasilisha maoni hayo Serikalini. Miswada ya mabadiliko iliandikwa na kuwasilishwa Bungeni na hatimaye sheria ya mabadiliko ya Katiba ilifanywa. Katika hatua zote hizo Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi kilihusishwa kikamilifu. Itakumbukwa kwamba hata waraka wa Serikali (*White paper*) 1998 uliokuwa na maoni ya Serikali ulizinduliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, utaratibu niliuelezea hapa ulifanywa katika mazingira tofauti na haya tuliyonayo sasa ya nia yetu ya kuwashirikisha wananchi na kuhakikisha kwamba wanashiriki kikamilifu, kwa kuwa jambo hili ni la kupanua demokrasia na kuhakikisha tunakuwa na Katiba ya nchi inayoonesha utashi wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano, Serikali inatarajia kuleta katika Bunge hili Muswada wa Sheria ya kuunda Tume katika Bunge lako la Tatu la mwezi April itakayoratibu maoni ya wananchi na kutoa elimu kwa wananchi ili kufanikisha lengo letu la kuwa na Katiba itakayotutoa katika miaka hamsini ya uhuru hadi kufikia umri wa karne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili litapata nafasi ya kutaja majukumu ya Tume katika sheria itakayotegemea kutungwa, utaratibu au namna Tume itakavyofanya kazi, namna ya kuwapata wajumbe wa Tume hiyo, sifa za wajumbe hao na mambo mengine ambayo Bunge hili litaona yanastahili kuwekwa kwenye sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpongeza na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara wa kuunda Tume Maalum ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, pili nakupongeza wewe kwa kunipatia fursa hii ili kuweza kueleza na kutoa ufafanuzi wa utaratibu utakaotumiwa kwenye mchakato wa uandishi wa Katiba.

Tatu, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini unaonipa imani na faraja kwamba watashirikiana na Serikali katika kuwaelimisha wananchi kufahamu shughuli za Tume ili waweze kujitokeza kutoa maoni yao wakati utakapowadia.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu wake, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa uvumilivu wao, kwa kupokea uamuzi wa Rais kwa shauku inayoashiria kama ilivyo kawaida yao kwamba watatoa maoni yao kwa uhuru, uwazi na bila woga kwa kuzingatia umoja wa Kitaifa, amani, mshikamano ambavyo ni tunu zetu za Kitaifa ambazo tunatakiwa kuzilinda na kuzitunza kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ambayo Kauli za Mawaziri zinatakiwa ziwe zimegawiwa kabla hajasoma, nadhani mmezipata lakini *page* namba tatu imerukwa, kwa hiyo watafanya utaratibu wa kuweka hii *page* namba tatu ambayo imerukwa.

## MAAZIMIO

### UFAFANUZI KUHUSU KAMBI RASMI YA UPINZANI

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, waliwasilisha kwako maombi kwa maandishi kuhusiana na kupata nafasi ya kurekebisha fasili ya 11 ya Kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007. Baada ya Spika kupokea maombi hayo ya marekebisho ya Kanuni hiyo ambayo katika maombi hayo walitaka neno 'RASMI' lililopo kwenye Kanuni hiyo ambayo inaiweka nafasi ya Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma kuwa chini ya Chama kimoja cha Upinzani cha CHADEMA, kitu ambacho kwa maoni yao kinavyinayama vyama vingine vya Upinzani vinavyowakilishwa Bungeni fursa ya kuongoza Kamati hizo.

Aidha, Wabunge hao waliomba neno hilo Rasmi lifutwe katika Kanuni hiyo ili kutoa haki na fursa kwa Mbunge yeyote anayetoka katika Chama chochote cha Upinzani kinachowakilishwa Bungeni kugombea na kuchaguliwa kuongoza Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Wabunge hao walihitimisha ombi lao kwa kuomba marekebisho waliyoyapendekeza yafanyike kabla ya kuundwa kwa Kamati za Kudumu za Bunge.

Ombi la Waheshimiwa hao lilikuwa na masuala mawili ndani yake ambayo yalipaswa kushughulikiwa kwa pamoja, masuala hayo ni:-

(a) Kufanya mabadiliko katika Kanuni za Kudumu za Bunge ambalo ni suala la Kikanuni.

(b) Uundwaji wa Kamati za Kudumu za Bunge ambalo nalo ni suala la Kikanuni.

Kwa kuwa suala lenyewe ni la kikanuni na kwa kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 3(3)(a) na (b) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la 2007,

suala lolote la kikanuni linapaswa kushughulikiwa na Kamati ya Kanuni ni dhahiri kwamba suala hili lisingeweza kushughulikiwa iwapo Kamati ya Kanuni za Bunge isingundwa kwanza.

Kwa kuzingatia hali hiyo busara za Mheshimiwa Spika zilitumika katika kulifanyia kazi suala hili kwa kufanya uamuzi ufuatao:-

(a) Kwamba, kwa kuwa suala husika ni la kikanuni na linapaswa kushughulikiwa na Kamati ya Kanuni za Bunge ni lazima Kamati hiyo iundwe kwanza kabla ya Kamati nyingine za Kudumu za Bunge kuundwa ili ilifanyie kazi suala lenyewe;

(b) Kwamba, baada ya kuundwa Kamati ya Kanuni za Bunge kwa mamlaka iliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 3(3)(a) na (b) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, lilifanyie kazi pendekezo hilo na suala la uundaji wa Kamati za Kudumu za Bunge na kutoa mapendekezo yake Bungeni kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 152(1) ya Kanuni za Bunge;

(c) Kwamba, ili kuondoa utata wa tafsiri Kamati ya Kanuni za Bunge ijadili na kupendekeza tafsiri iliyowazi ya maneno “Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.”

(d) Kwamba ili kuwezesha mchakato wa uundwaji wa Kamati za Kudumu za Bunge kukamilika, Kamati ya Kanuni za Bunge ishughulikie pia mapendekezo ya mabadiliko ya majina ya Kamati hizo ili yaendane na muundo wa sasa wa Wizara za Serikali; na

(e) Kwamba, kwa ajili ya uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge, Azimio la Kufanya mabadiliko ya Kanuni husika na pia pendekezo la kutengua Kanuni ya 153(1) yawasilishwe Bungeni na Mheshimiwa Naibu Spika katika Mkutano huu wa Pili wa Bunge ili kuwezesha mchakato wa kuunda Kamati za Kudumu za Bunge kukamilika haraka iwezekanavyo.

Katika kutekeleza uamuzi wa Spika kama ulivyoelezwa kwenye aya niliyokwishaitaja hapo juu, Mheshimiwa Spika aliunda na kuteua Wajumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 113 (4), pamoja na Kifungu cha 3(1) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge ili kulifanyia kazi suala hili. Kamati hiyo iliundwa na jana jioni ilifanya kikao.

Wajumbe wa Kamati hiyo ni pamoja na Mheshimiwa Spika Anne Semamba Makinda, Mwenyekiti; Mheshimiwa Job Ndugai, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa William Lukuvi, Mjumbe; Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mjumbe; Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mjumbe; Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mjumbe; Mheshimiwa Tundu Lissu, Mjumbe; Mheshimiwa Andrew Chenge, Mjumbe; Mheshimiwa Makani Ramo Matala, Mjumbe; Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki, Mjumbe; Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mjumbe; Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, Mjumbe; Mheshimiwa Hamad Rashid

Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa George Simbachawene, Mjumbe; Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mjumbe na Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mjumbe.

Kifungu cha 3(3) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007, pamoja na mambo mengine kinaeleza kwamba, moja ya majukumu ya Kamati za Kanuni za Bunge ni kwamba:-

(a) Kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge; na

(b) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya pendekezo lolote linalohusu Kanuni za Kudumu za Bunge ambalo limepelekwa kwa Kamati hiyo na ama Spika, au Mbunge yeyote.

Kwa Mamlaka iliyopewa Kamati hiyo kwa mujibu wa vifungu hivyo, Kamati ya Kanuni za Bunge ilikutana jana kama nilivyokwishasema tarehe 7 Februari, 2011 mara baada ya kikao cha *briefing*, kujadili mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Katika kushughulikia mapendekezo hayo, Kamati hiyo ilijadili na kupitia kwa makini Kanuni za Bunge zinazohusika ili kubaini kama ni kweli au la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaundwa na Chama chenye haki ya kuchagua kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kama inavyodaiwa na Wabunge waliowasilisha maombi ya marekebisho ya Kanuni.

Katika mjadala huo kuhusiana na tafsiri ya maneno Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Kanuni ya 14 hadi ya 16 zinafafanua kuhusu kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na jinsi anavyochaguliwa, Kanuni ya 14,15 na 16.

Kanuni hizo pia zinafafanua kwamba, Chama chenye haki ya kuchagua kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kile chenye idadi ya Wabunge wengi wasiopungua asilimia 12 na nusu ya Wabunge wote.

Aidha, Kanuni ya 15(2) inafafanua pia kuwa, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atateua Wabunge wa Chama chake au Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambao watakuwa wasemaji wakuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara zilizopo Serikalini.

Kutokana na masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Kanuni za Bunge iliridhika pamoja pasipokuwa na mashaka yoyote kwamba tafsiri sahihi ya maneno Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni Kambi inayoundwa na Vyama vya Upinzani vinavyowakilishwa Bungeni kwa mujibu wa masharti ya fasili ya pili ya Kanuni za kudumu za Bunge. (*Makofi*)

Kwa tafsiri hiyo si kweli kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaundwa na Chama cha Upinzani chenye Wabunge wengi na chenye haki ya kuchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Hitimisho, kwa kuzingatia ukweli huo Kamati ya Kanuni za Bunge yenye wajumbe niliokwishawataja ilipendekeza maneno Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yawekewe tafsiri, kwa maneno mengine hakuna badiliko lolote ambalo litafanyika ndani ya kitabu cha Kanuni mahali popote pale zaidi ya ufafanuzi kwenye eneo la tafsiri, ambao utasomeka kama ifuatavyo:-

“Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni maana yake ni Kambi ya Upinzani inayoundwa na Vyama vya Upinzani vinavyowakilishwa Bungeni kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (2) ya Kanuni ya 14 ya Kanuni hizi.” (*Makofi*)

Kamati hiyo iliyokutana jana ilijiridhisha pia kwamba tafsiri hiyo itaondoa utata uliopo na kulifanya ombi la Wabunge wahusika la kuifanyia marekebisho ya Kanuni ya 113(11) kutokuwa na ulazima wowote.

Kutokana na uamuzi huo Kamati ya Kanuni za Bunge imetoa mapendekezo ili yaridhiwe na Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 152(2). Mapendekezo yenyewe ni:-

- (a) Tafsiri iliyo wazi ya maneno Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni;
- (b) Kufanya marekebisho kwenye nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 ili majina ya Kamati za Kudumu za Bunge yaendane na Muundo wa sasa wa Wizara za Serikali; na
- (c) Kutengua Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 ili kuwezesha mabadiliko hayo kuanza kutumika baada ya kupitishwa na Bunge.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 152(1) mapendekezo ya mabadiliko ya Kanuni yanapaswa kupitishwa na Bunge kwa Azimio la Bunge.

Ili kuliwezesha Bunge kupitisha Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge ya Mabadiliko katika Kanuni zetu, sasa naomba kusoma Azimio husika.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed Mbunge wa CUF na Mheshimiwa David Zacharia Kafulila Mbunge wa Chama cha *NCCR* Mageuzi waliwasilisha kwa Mheshimiwa Spika maombi kwa maandishi ya kurekebisha fasili ya 11 ya Kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007;

Na kwa kuwa, baada ya kupokea Spika kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, aliyapeleka maombi hayo kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge;

Na kwa kuwa, kifungu cha 3(a) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo, kinaelekeza kwamba majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge ni pamoja na kujadili na kutoa mapendekezo kuhusu kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge na kuchunguza na kutoa taarifa kuhusu pendekezo lolote linalohusu Kanuni za Kudumu za Bunge ambalo limepelekwa kwa Kamati hiyo na Spika au Mbunge yeyote;

Na kwa kuwa, Kamati ya Kanuni za Bunge kwa madaraka iliyonayo kwa mujibu wa kifungu hicho cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge imejadili na kutoa taarifa yake kuhusu pendekezo la kufanya mabadiliko katika Kanuni ya 113(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007;

Na kwa kuwa, Kamati ya Kanuni za Bunge imejadili na kupendekeza kwamba tafsiri ya 11 ya Kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 haina ulazima wa kufanyiwa marekebisho kama ilivyoombwa na Wabunge husika niliokwisha wataja;

Na kwa kuwa, kwa ajili ya kuondoa utata wa tafsiri, Kamati ya Kanuni za Bunge imependekeza pia kuwepo kwa tafsiri ifuatayo:-

“Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni maana yake ni Kambi ya Upinzani iliyoundwa na Vyama vya Upinzani vinavyowakilishwa Bungeni kwa Mujibu wa Masharti ya Fasili ya Pili ya Kanuni ya 14 ya Kanuni hizi” ;

Na kwa kuwa, Kamati ya Kanuni za Bunge imejadili na kupendekeza kwamba nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 inahitaji kufanyiwa marekebisho kwa kubadilisha majina ya Kamati za Kudumu za Bunge ili yaendane na muundo wa sasa wa Wizara za Serikali ambayo natumaini Waheshimiwa Wabunge natumaini kila mmoja ana kiambatanisho chenye kuonesha jina la Kamati na Wizara ambazo Kamati hiyo itasimamia;

Na kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 152(1) Bunge lina mamlaka ya kupitisha Azimio la kufanya mabadiliko katika Kanuni yoyote kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge, ili kuwezesha marekebisho yaliyopendekezwa kuanza kutumika mara baada ya kupitishwa na Bunge, Kamati ya Kanuni za Bunge inapendekeza Kanuni ya 153(1) itenguliwe;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 zinafanyiwa mabadiliko kwa kuweka tafsiri ya maneno Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa kupitisha muundo wa Kamati za Kudumu za Bunge, kama ulivyopendekezwa na Kamati ya Kanuni za Bunge kwenye kiambatanisho cha Azimio hili na pia kwa kutengua Kanuni ya 153(1).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Kabla ya kuamua hoja hiyo tunao wageni wetu na kama tulivyokubaliana kwenye mazungumzo yetu kwamba kutokana na wingi wetu Bungeni na muda ambao umebakia ni ule ule, kwa hiyo tutapunguza vitu fulani ambavyo tumezoea kuvifanya vizuri, tutakuwa tunafanya angalau kwa utaratibu kidogo, kimojawapo ni utambulishaji wa wageni. Kwa hiyo, tutatambulisha wageni wa Kimataifa ambao wapo.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni waliopo hapa Bungeni asubuhi hii na wapo sehemu ya Spika, kwanza tunaye Balozi wa Uingereza Mheshimiwa Diane Corner *if you can raise please*, ahsante. Tunaye Mheshimiwa Sir Allan Haselhrst, yeye ni Mwenyekiti wa CPA Bunge la Uingereza, *you are most welcome*, tunaye Mr. Andrew Tuggey, yeye ni Katibu wa CPA Bunge la Uingereza, huyu yupo kama Kasilillah hivi, Tunaye Mr. Stuart Forster, yeye ni Mshauri Masuala ya Utawala katika Shirika la DFID, tunaye pia Mr. Pascal Mayalla, yeye ni Mshauri wa Siasa, Ubalozi wa Uingereza, tunaye pia Mheshimiwa Dkt. Ad Koekkoek, yeye ni Balozi wa Netherlands pia amefuatana na Ms. Agnes Hanti, Afisa Ubalozi wa Netherlands. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wamekuja kututembelea sisi lakini kama hawa wenzetu wa CPA ni mawasiliano ambayo tumekuwa nayo kila wakati, pia walikuwa wamesimamia mambo ya uchaguzi wamekuja kutoa tathmini wanavyoona *European Union* uchaguzi ulifanyika namna gani. Wataonana na Waziri Mkuu, wanapaswa pia kuonana na mimi kama Spika lakini inaonekana kwamba wachangiaji hapa wapo wengi, kwa hiyo, inaweza kuchukua muda, nilikuwa nimemwomba Naibu aende lakini naona pia na yeye hataweza kwa sababu ya muda uliopo hapa.

*We welcome you here because this is our second Parliament but the first when the Members of Parliament are actively involved in their Parliamentary activities. So you will be able to meet Prime Minister and may be my Office at an appropriate time, as you can understand here we have some very serious matters of Standing Order, and I understand you have heard the Prime Minister is trying to put down that the constitution arrangements are going to be accepted as something which the Parliament has passed on, there will be a Bill which will guide on how we can go about trying to get the opinions of the Tanzanians on the new Constitution. So, you are welcome and we shall meet you later, thank you very much. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji, uzuri wa hiki tunachotaka kuchangia kimeletwa kwenye Kamati ya Kanuni ambayo ilipata muda mrefu sana wa kupitia suala hili na wakafika mahali wakakubaliana. Kwa hiyo, pamoja na wingi wetu huu, nitakwenda kwa wachangiaji wawili wawili kila Chama halafu tutapiga kura za ndiyo au hapana. Kwa hiyo, mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Kafulila kwa sababu hawa ndiyo walioleta barua atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.



**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunituua niwe mchangiaji wa kwanza. Kwanza, napenda kuishukuru Kamati ya Kanuni kwa kazi kubwa ambayo wameifanya maana lengo letu sisi tulikuwa tunadhani kwamba tunahitaji mabadiliko ya Kanuni kumbe ni tafsiri tu, kwamba ingetolewa tafsiri peke yake ilikuwa inatosha kabisa kufanya Bunge ambalo lina kambi moja ya Upinzani na kuondoa migogoro ndani ya Kambi ya Upinzani ili kuifanya ifanye kazi pamoja kwa ajili ya kuidhibiti Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru hilo kwa sababu sisi tunafahamu kwamba hapa tulipo kuna Chama kipo madarakani lakini kuna Vyama ambavyo ni Serikali inayosubiri, sisi ambao tupo *opposition* ni Serikali ambayo inasubiri. Kwa hiyo, kimsingi tunapaswa kujipanga kwa namna ambayo tutatoa picha kama watu ambao wanaweza wakawa muafaka kwa Serikali inayosubiri. Dhana ya mgawanyiko ambayo ilikuwa imejitokeza pengine ndani ya Kambi yetu sisi wenyewe, kimsingi ni dhana ya aibu na ni dhana ambayo pengine naishukuru Kamati ya Kanuni kwa namna ilivyofanya kwa sababu itatuepusha na aibu hiyo ya watu ambao tunajenga kambi moja kuhitilafiana katika maeneo ambayo siyo ya msingi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naikumbuka rekodi nzuri ya Spika aliyetangulia wa Bunge la Tisa, Mheshimiwa Samuel Sitta ambaye kwa sasa ni Waziri, chini ya Uongozi wake Kambi yote ya Upinzani ilifanya kazi kwa pamoja na waliwekeana Kanuni, wakafanya kazi pamoja na ilipotokea Mbunge amekwenda kinyume cha makubaliano yao ndani ya Kambi yao walimchukulia hatua ya kikanuni na Spika aliridhia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachokiona hapa ni kwamba Kamati ya Kanuni inatuwezesha sasa kufanya kazi kama Kambi moja kwa kuwa sote tuna malengo yanayofanana. Chama cha NCCR Mageuzi, CHADEMA, TLP, UDP pamoja na CUF sote tunafanana malengo ya namna ambavyo tunataka kuendesha Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, pengine niwaombe wale wachache ambao kwa namna moja ama nyingine wangependa kutokuipitisha Kanuni hii pamoja na uchache wao lakini ni muhimu kuwafafanulia baadhi ya mambo ili kwa pamoja tutoke na msimamo mmoja. Wachache ambao wanapinga Kanuni sioni msingi wao wa kuipinga, zaidi ya ubaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni hatari sana kama leo tunashinda asilimia 20 tunakataa mseto, siku tukipata asilimia 60 sijui itakuwaje. Kama watu wa *Opposition* ambao Serikali inayosubiri lazima tuanze kuonyesha muafaka wa Kitaifa hata kwenye *size* ndogo ya utawala wetu. Ukipewa kidogo uonyeshe kwamba unaweza kuwa ni mtu ambaye una muafaka wa Kitaifa, unaweza ukaongoza watu kwa muafaka wa pamoja. Maana ukipewa kidogo ukashindwa kuonyesha busara ya kawaida ya umuhimu wa kufanya kazi, siku ukipewa kikubwa hauwezi kuaminika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya ya kanuni yatatoa haki kwa Wabunge wote wa Upinzani kuwa na nafasi sawa ndani ya Kambi ya Upinzani. Watu watatoa mfano wa kawaida kwa mfano, NCCR Mageuzi ni Chama Tawala Mkoa wa Kigoma kule hata kama

CCM inaweza isitake tuna Wabunge wanne, CCM ina watatu, CHADEMA ina mmoja ukisema kwamba chama hiki hakina umuhimu wowote kwenye Kambi hiyo, ni jambo la aibu, Chama kinatawala Mkoa useme kwamba hakina nafasi katika Kambi ya Upinzani ni jambo la aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachokisema ambacho kimepelekea niipongeze Kamati ya Kanuni ni kwamba tunakwenda sasa kujenga Kambi imara ya Upinzani, tufanye kazi pamoja, Chama ambacho kimepata Wabunge wengi ambao wanakwenda zaidi ya asilimia 12.5 kitoe kiongozi na sote tumheshimu, tufanye naye kazi pamoja na tofauti zote za vyama ambazo ziko nje ya Bunge zenyewe zinaweza zikaendelea lakini ndani ni lazima tufanye kazi pamoja kwa sababu hata tufanyaje Katiba ya sasa haijaruhusu vyama vyote vya Upinzani kuungana. Kwa hiyo, kwa sababu haijaruhusu labda pengine Katiba Mpya ijayo inaweza ikaruhusu.

Lakini mazingira ya sasa ambapo tunafanya kazi katika mazingira tofauti ya vyama tunapokuwa nje, ni muhimu tunapokuwa ndani tukubaliane kufanya kazi pamoja. Tufanye kazi CHADEMA, tufanye kazi CUF, tufanye kazi TLP, tufanye kazi UDP, tufanye kazi NCCR Mageuzi kwa pamoja na tukubaliane mambo ya msingi. Kama kuna kanuni ambazo zinatuongoza kama Kambi ya Upinzani zituongoze. Akitokea Mbunge wa Upinzani anakwenda kinyume cha Kambi Rasmi ya Upinzani achukuliwe hatua kwa taratibu za kawaida kabisa, kama anawajibishwa, jambo la msingi ni kwamba huwezi ukamhukumu mtu kabla hujamshirikisha. Huwezi ukafanya kazi na Kafulila au na Mkosamali au na Augustino Mrema na wakati hauja-*prove* kama ana kosa gani. Tufanye kazi kwa pamoja, atakayekwenda kinyume cha Kanuni basi achukuliwe hatua kwa mujibu wa Kanuni. Kama kanuni inatosha kumuondoa kabisa basi achukuliwe hatua kwa kadri ambavyo inafaa kuchukuliwa kama Mbunge ambaye anatoka Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo ya kueleza nikiamini kwamba sasa tunaanza mwanzo mzuri na Wabunge wenzangu wa NCCR Mageuzi, naamini tutakuwa watiifu wenye nidhamu kwa Kiongozi Kambi Rasmi Bungeni na tutaacha tofauti zetu za nje tukiamini kwamba Bunge hili ndio alama ya demokrasia katika Taifa. Kwa hiyo, ni lazima tufanye kazi kama watu wazima ambao tunajua ambacho kimetuleta hapa. Nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya pili. Pili nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuwasilisha Azimio hili ambalo naliunga mkono kwa asilimia mia moja.

Pia nikushukuru wewe mwenyewe pamoja na Kamati yako ya Kanuni kwa kuchukua muda mrefu sana jana na bahati nzuri tuna wanasheria wengi. Nimshukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kuja na vitabu vingi sana vya kisheria ili kuisaidia Kamati ipate maamuzi ya busara. Nashukuru sana alitumia uzoefu wake wa Uwakili na taaluma yake ya Kisheria na akafanya kazi yake hiyo nzuri na hatimaye tukafikia makubaliano kama yalivyowasilishwa na Naibu Spika. Namshukuru sana. (*Makofi*)

Lakini namshukuru vile vile Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Upinzani Bungeni namna alivyojenga hoja na kuona kwamba pengine si wakati muafaka kufanya hivyo, lakini hatimaye baada ya uchambuzi, kuelimishana na busara nyingi zilizotumika ndani ya Kamati hiyo, hatimaye naye akaona kwamba kuna umuhimu wa mabadiliko haya. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Naelewa hivyo kwa sababu Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio chombo peke yake katika Tanzania kinachowawakilisha Watanzania wote, hakuna chombo kingine. Kwa hiyo, moja ya wajibu wetu kama Wabunge ni kuelewa kwamba hakuna chombo kingine ambacho kinawakilisha Watanzania zaidi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote tumetoka katika kona yote ya Tanzania. Hivyo, ni muhimu basi Kanuni zetu na taratibu zetu zihakikishe kila Mbunge anapata haki ya Kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pale itakaponekana kwamba Kanuni haitoi haki hiyo, basi hiyo ni haki ya msingi inayopingwa na inahitaji kurekebisha. Kwa hiyo, naipongeza sana Kamati ya Kanuni, nakupongeza sana Naibu Spika na wewe Mheshimiwa Spika, kwa kufanya marekebisho hayo ambayo ni muhimu sana kwa kutoa haki ya msingi ya raia ya kwamba kila mtu ana haki ya kuchaguliwa. Hilo nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kwenye Kamati ndogo aliyounda Mheshimiwa Spika wa Bunge la Tisa katika kuzipitia hizi Kanuni. Tulizipitia Kanuni baadaye tukajifunza kwamba kuna mapungufu hapa na pale. Moja, ni tafsiri kwamba kuna maeneo fulani hatukutoa tafsiri iliyo ya kina na ya kueleweka. Kwa hiyo, hata sisi ambao tuliandika barua mwanzo kutaka vifungu fulani vibadilishwe cha 113 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taaluma ndani ya wenzetu kwamba kumbe tatizo hapa ni tafsiri, naishukuru sana Kamati ya Kanuni kwamba yale maombi tuliyoapeleka sisi wamesema hayana haja ya kubadilisha. Hili ni jambo la msingi sana. Watu wasione kwamba sisi tume-*influence* Kamati kwamba imebadilisha, haikubadilisha kitu Kamati. Kamati ya Kanuni iliyopita ilisahau kutoa tafsiri ya neno Kambi Rasmi. Pamoja na kwamba tafsiri hiyo, inapatikana katika kanuni ya 14(2) na ndio maana Azimio hili linasema kwamba kwa kufuata Kanuni ya 14(2) tuweke tafsiri sahihi ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, iko dhana kwamba labda wengine wanabebwa na Chama cha Mapinduzi, hapana hakuna anayebebwa, ni Watanzania waliomo ndani ya Bunge hili wameona kuna upungufu katika Kanuni na ni utaratibu wa Bunge hili linapooni kuna upungufu wa Kanuni, Kanuni zetu zinaruhusu ama Kamati ya Kanuni au Mbunge kuleta maombi ya mabadiliko ya Kanuni, ni jambo la Kawaida kabisa. Sote hapa tumekula kiapo kwa Katiba hii hapa. Lakini ni sisi tunasema Katiba hii ina kasoro. Si tumekula kiapo na kukabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge asubuhi umewakabidhi Katiba, wameondoka hapa lakini Wabunge hawa hawa tunarudi tunasema hii Katiba ina upungufu. Kwa hiyo, nasema kwanza hakuna aliyebebwa na tafsiri hiyo wenzangu msiitoe kabisa. Kama ni

kubebwa tulikuwa na Bunge la Tisa hapa Chama cha *CUF* ndicho kilichokuwa na Wabunge wengi. Hatukuwa zaidi ya Kiongozi wa Upinzani, Naibu wa Kiongozi wa Upinzani alitoka CHADEMA, Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC* alitoka CHADEMA Dr. Slaa, Mbunge wa *SADC* alitoka CHADEMA, Mwenyekiti wa *POAC* Mheshimiwa Zitto alitoka CHADEMA, Mheshimiwa John Cheyo alitoka *UDP*. *CUF* haikuwa na kitu, hatukulalamika wala hatukusema kwamba CCM wameibeba CHADEMA, leo inakuwa dhambi? Mkuki kwa Nguruwe kwa binadamu mchungu? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba tujenge Tanzania, Watanzania wanataka maendeleo, Watanzania wanataka amani na utulivu. Tukae tushirikiane, tumepata ridhaa ya wananchi. Waheshimiwa Wabunge, sisi tuna Wabunge 24 waliopata kura za wananchi, si Viti Maalum, Majimboni, wenzetu wana Viti 22 vya kura za wananchi. Suala la *population* hilo ndio tatizo la msingi sasa kwamba eti Zanzibar ni ndogo. *Zanzibar was a country* mpaka tumeungana mwaka 1964. Zanzibar ilikuwa Mwanachama wa Umoja wa Mataifa kama nchi *nyingine it has all its rights* na hakuna Tanzania bila Zanzibar *what are you talking about?* (*Makofi*)

Tusizungumze mambo ya kitoto, *let us talk the facts*. Huwezi kuwa na Tanzania bila ya Zanzibar yenye watu milioni moja *can you have it?* Hiyo Zanzibar unayoiona ndogo waulize walioko katika Serikali. (*Makofi*)

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu kanuni ya 64(1)(g) Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine, hayo maneno kwamba hoja ya kitoto ni maneno ya matusi yaondolewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed naomba uyafute maneno uliyosema ya kitoto.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, tuseme maneno ya kiutu uzima, nafuta maneno yangu. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** *Message sent.*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, sisi Zanzibar pamoja na udogo wetu na nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema hapa kutokana na Mapinduzi ya mwaka 1964 ndio yaliyowezesha kupatikana kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na mkataba wa Muungano *Article of Union* ndio imepatikana Tanzania pamoja na uchache, tena walikuwa watu hata 600,000 hawajafika walikuwa laki nne tu, lakini Mwalimu Nyerere na Rais Karume waliona umuhimu wa Watanzania hawa kuungana pamoja, leo tuko hapa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Sasa anayedharau hii akasema Zanzibar ni watu wachache, ni watu wachache maana yake nini? Katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Tanzania inamheshimu hata mtoto mchanga aliyezaliwa leo, wacha watu *population* ya watu milioni moja. Kwa hiyo, wewe kumbe maamuzi yako yote yanaangalia idadi ya watu haiangalii Watanzania kama Watanzania na ujumla wao hiyo ni uvunjaji wa Katiba ya nchi. (*Makofi*)

Chama chochote cha siasa kinatakiwa kihakikishe kwamba kinawajali Watanzania katika aina zao zote kwa rangi zao, kwa dini zao, kwa uwingi wao, kwa udogo wao na kwa silka zao zote, ndio Katiba inavyozungumza. Sasa anapokwambia mtu wewe umechaguliwa na watu 10, 20 Katiba ya Jamhuri inasema.....

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu kifungu cha 64(1)(b) Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala. Suala la Muungano haliko kwenye mjadala, hapa azungumzie Azimio la Bunge. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu hivyo ndivyo alivyojipanga yeye kuzungumza, hajazungumzia Muungano anazungumzia hoja alizonazo yeye mwenyewe, tumsikilize. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hoja tunayozungumzia ni ya Kambi Rasmi Bungeni ambayo inazungumzia Umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba tunayoitumia ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Narudia kusema tunahitaji kujenga jamii ya umoja, yenye amani, utulivu na maendeleo endelevu. Tofauti tunazozijenga sasa siyo wanazozitaka Watanzania. Watanzania hawataki ubaguzi ndio maana tukatumia busara katika Bunge la Tisa baada ya kushauriwa na Spika kwamba ni vizuri tukawa pamoja, tumekuwa pamoja mbona tulifanya kazi nzuri tu hapa ndani ya Bunge. Nawaomba wenzangu kabisa badiliko hili linasaidia kuimarisha Kambi ya Upinzani, Azimio hili linasaidia kuimarisha Bunge na Spika amesema wazi ndani ya Bunge hili anataka *a constructive ideas* katika Bunge ili Wabunge wachangie na yeye yuko tayari kuyasimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakuunga mkono kwa hilo na sisi tunaunga hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Lakini pili, nichukue fursa hii kumkumbusha mchangiaji aliyepita, baba yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Bunge la Tisa alipopata ridhaa ya kuwa Kiongozi wa Upinzani aliunda Kambi yake. Kanuni za Bunge zilivyobadilishwa, zikatengeneza asilimia ambayo ilifanya yeye ashindwe kutengeneza Kambi yake ndipo alipotuita. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, zilibadilishwa hizo asilimia?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwaka 2007.

**SPIKA:** Hapana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Katika mabadiliko tuliyoyafanya Bunge lililopita.

**SPIKA:** Hapana mimi ni msimamizi wa Kanuni.... Naomba ukae.

Mimi ni msimamizi wa Kanuni hizi na bahati nzuri nina historia ya kuwa humu ndani. Mwaka 1995 ndio kwanza Bunge hili lilikuwa la Vyama Vingi. *Benchmark* tuliyoiweka katika kanuni za mwaka 1995 ili iwe Kambi Rasmi ya Upinzani, Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani ilikuwa lazima wa-meet asilimia 30. Mwaka 1995 wali-meet hiyo walikuwa zaidi ya 46, kwa hiyo, waka-form kambi yao ya Upinzani hakukuwa na tatizo.

Mwaka 2000 Wapinzani ndani ya Bunge walikuwa 26 tu, kwa hiyo, ilikuwa isiwepo Bunge ya Upinzani, wapo Wapinzani lakini hakuna Kambi ya Upinzani. Maana asilimia 26 ilikuwa hai-meet. Kwa hiyo, kwa uongozi wa Mheshimiwa Spika Msekwa tulifanya busara kwamba haiwezekani tumekuwa na Vyama Vingi halafu hawa wawe humu ndani Wapinzani lakini siyo Rasmi. Ndio tukafanya bidii, tukashusha ile *benchmark* kutoka 30%, tukafika 12.5 hiyo ikaweza kuwa-accommodate wale 26 kuwa Kambi Rasmi Bungeni, walikuwa vyama vyote. (*Makofi*)

Ilipofika mwaka 2005, *CUF* wakawa wengi na wenyewe wakafanya mchezo mdogo kama wanavyofanya hawa wakajitengenezea Kambi yao ambayo haikuungwa na mtu yeyote, ilikuwa haina maana yoyote. Bahati mbaya ndiyo hii tafsiri haikuwepo tunayoingiza leo. Wenyewe walikaa kipindi kifupi tu ndio ikabidi sasa wahusishe na wenzao ndio haya aliyoeleza huyu. Sasa imefika mwaka huu 2011 CHADEMA kama wao peke yao ni asilimia 12.5, *CUF* kama wao peke yao wanafika kwenye asilimia kumi na kitu. Sasa Kanuni tunayozungumza hapa ambayo tunaomba ifanuliwe ni Kanuni ya 14(2) yenyewe inasema Wabunge wote wa Vyama vya Upinzani kama hawatapungua chini ya asilimia 12.5 wata-form Kambi ya Upinzani wasipopungua asilimia hiyo.

Kwa hiyo, inarudi kama ilivyokuwa mwaka 2000 ambapo walikuwa wamepungua hata asilimia 30, ndio tukalazimisha iwe 12.5. Kwa hiyo, si kweli kwamba hii ilifanyika mwaka 2007, ilifanyika mwaka 2000. Hiyo ndio inaendelea kutumika sasa. Kinachosema hapa Kambi ya Upinzani yenye Wabunge wengi ndio watatoa Uongozi kitu ambacho CHADEMA wamefanya. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Halima uendelee. Hayo ni masahihisho.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naona tunazungumza lugha moja. Unachokizungumza wewe ndicho nilichokuwa nikisema. Kwa hiyo, umenipotieza muda mwingi tu bila sababu. Waliunda mazingira ya kuwaruhusu ndio wakatukaribisha, wasilete unafiki.

**SPIKA:** Ondoa maneno ya unafiki tafadhali, jadili tu lakini hilo neno ondoa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Unafiki ni tafsiri ya kawaida.

**SPIKA:** Hapana wewe jadili hoja yako maneno ya unafiki naomba uondoe. Kama tulivyomwambia yule aondoe maneno ya kitoto na wewe ondoa maneno ya unafiki.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima yako, nalitoa tu lakini ujumbe umefika.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashangaa kwa mara ya kwanza katika Bunge naona eti Wabunge wa Upinzani wanapigiwa makofi sana na CCM, hiyo inatupa picha gani?

**MBUNGE FULANI:** CCM, CCM.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hiyo inatupa picha gani.

**MBUNGE FULANI:** Umoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, inaonyesha kwamba watu ambao wanajivika vilemba vya kutaka kuwa wawakilishi wa Watanzania ambao waliwaaminisha wao kama Wapinzani wamegeuka CCM (B) leo. (*Makofi*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Naomba nitumie kanuni ya 64(g) Mbunge yeyote anapoonzea hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. Mimi naona hapa kwanza tunataka kutumia lugha ya kuudhi na kudhalilisha na kusema kuna wenzetu wa Upinzani ambao ni wana CCM. Wana CCM ni wana CCM na Wapinzani ni Wapinzani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Halima Mdee endelea, nadhani umesikia, labda kama na wewe unaweza kuwa CCM siku nyingine.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwenye mijadala tunatakiwa kuwa na ngozi ngumu tunapokuwa wanasiasa.

Mheshimiwa Spika, ninachokiona hapa ni lile suala zima la muafaka ambao wenzetu walifikia Zanzibar na kuunda Serikali yao moja na kujadili sera zao kwa pamoja linataka liletwe kwa njia ya kinyume nyume Bungeni. Kwa *atmosphere* ninayoiona Bungeni hapa kunyamazisha nguvu ya CHADEMA ambayo wakati tukiziongoza zile Kamati tuliweza kuwafanya Watanzania wajue ufisadi unavyoendeshwa nchi hii. (*Makofi*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kwa kanuni ya 64(b) hatutazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala, hatuzungumzii mambo ya Muungano.

**SPIKA:** Pale nilisema mtu anaweza kujadili hoja yake na muache ajadili hoja yake, wanaojibu watajibu humu ndani. Halima Mdee endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hawajazoea bado, wapya watazoea tu.

**MBUNGE FULANI:** Hata Tundu Lissu ni mpya.

**SPIKA:** Maneno hayo unatoa wapi wewe? Maneno mengine mnayatafuta tu hawa Wabunge wameletwa na watu wao upya na kutokuwa mpya yanatoka wapi! Hebu endelea na hoja yako. Naomba msikilize anayo hoja yake.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Azimio la leo linazungumzia kutoa tafsiri ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Ukiangalia kipengele cha 14 na 15 cha Kanuni za Bunge ambazo tunazo, kwa makusudi kanuni inatuambia kwamba kuna uwezekano wa aina mbili, uwezekano wa kwanza ndio kama ule ulioueleza kwamba kukawa kuna vyama mbalimbali ambavyo vimekaa kwa pamoja na kukubaliana kushirikiana masuala kadhaa ili waweze kutimiza ile idadi inayotakiwa kikanuni na kuunda Kambi yao ya Upinzani. Hiyo ni 14(2). Lakini kanuni hizi hizi kwa kutambua kwamba ni haki ya Chama cha Siasa ambao huu ndio utaratibu wa Jumuiya ya Madola ukiangalia hata tafsiri ya Upinzani na tafsiri ya *Official Opposition* ama Kambi Rasmi ya Upinzani ni tafsiri mbili tofauti.

Upinzani ni mchanganyiko wa Vyama mbalimbali vya Upinzani ndani ya Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani ni Kambi yenye viti vingi, ukijumuisha vyama vyote ambavyo viko kwenye Upinzani. Yaani tuko kama vyama saba tukagombea, CHADEMA ikapata viti vingi vya Ubunge, kwa tafsiri ya neno Kambi Rasmi kwa tafsiri za kawaida za *dictionary* za kisheria, za Kiswahili, za *practice* ya Mabunge mbalimbali ni kile Chama chenye Wabunge wengi Bungeni. Sasa nashangaa leo kuna wenzetu hapa sijui kwa vile hata Kiswahili hawajui tunapitishapitisha mambo yanakiuka masuala ya *customs* ambazo zinatungoza kuwa sisi member wa zile Jumuiya, wao wako hapa wanashangaashangaa kwa kuwa hawajui.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kusema tafsiri ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni Umoja wa Vyama vyote vilivyopo Bungeni. Huwezi kumlazimisha kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani awaongoze watu ambao hawakubaliana nao kimsingi wala kimsimamo. Tutatengenezaje nidhamu kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani kama hakuna misingi mliyokaa nayo? Ndio maana Hamad Rashid Mohamed kipindi alituita tukakaa baada ya kanuni kubadiliishwa tukakubaliana tunakwenda pamoja kwa misingi ipi. Kwa hiyo, nadhani kubadilisha neno Kambi Rasmi ama kuingiza tafsiri ya Kambi Rasmi inavuruga kanuni kwa mapana yake. Tunaweza tukaamua kwa kuwa mko wengi mkapitisha, lakini ukweli utabaki pale pale. (*Makofi*)



## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kanuni ya 68, kwa ufupi maneno aliyoongea Mheshimiwa Mbunge anayechangia hoja sasa hivi ya kusema kwamba wapo watu pale juu wameshangaashangaa hawajui wanalolifanya, wakati Kiswahili ni lugha ya Taifa huwezi kujua mgeni huyo anaijua kwa kiasi gani, ni kudhalilisha wageni wetu, tunaomba aafute usemi huo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu, hicho kifungu cha kanuni...

**SPIKA:** Utaratibu wa kwanza unatakiwa ufanyiwe maamuzi, mwacheni Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu mimi nilikuwa sijasimama. Lakini kwa sababu sasa nimeshasimama inabidi akae. Wakati anasema nilikuwa sijasimama. Tunachokisema Waheshimiwa Wabunge msijiletee matatizo bila sababu, maana yake vitu vingine mnaviingiza, kama hamna hoja muwe mnaacha tu, tusiingize vitu visivyokuwa na maana. Nilikuwa nashangaa qnasema nani wanaoshangaqshangaq, nikashangaa ni qking nani wasiojua Kiswahili, basi kumbe ilikuwa ni wageni wetu. Tunaendelea!

Mheshimiwa Tundu Lissu ilikuwa hiyo?

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo hiyo.

**SPIKA:** Haya tunaendelea, alikuwa anaongea nani?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Halima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima hotuba yako imeingiliwaingiliwa kwa nini mnakuwa hamna msimamo? Haya tuendeleo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tunafanya funika kombe mwanaharamu apite, lakini ukweli utabaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, tunajua kwamba watapatikana Wenyeviti wa Kamati, sisi hatuna shida ya Uenyeviti wa Kamati, Wenyeviti wa Kamati ni watu ambao wanasaidia kupata ajenda za Bunge ambazo zinaweza zikawa ama zina maslahi ya Umma, ama hazina maslahi ya Umma. Kwa upepo huu ninaouona wa ushirikiano wa hawa watu wanaojiita Wapinzani *vis-a-vis* CCM, kuna hatari kubwa tukakuta ajenda zinazoletwa ni zile ambazo mtawala anazitaka. Nasema nimalizie kama watu wanafikiria muziki wetu utapungua kwa kutunyima nguvu hizi za kimaandishi, muziki wa CHADEMA utakuwa mzito wa 2015. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** We Halima unataka kumtisha nani? Mtakwenda kama Bungeni? (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Hana wa kumtisha.

**SPIKA:** Kama ni hapa Bungeni mtatumia kitabu hiki ambacho mmekitunga wenyewe, huko kwingine mimi hakunihusu.

**MBUNGE FULANI:** Ni bora waanzishe bendi ya muziki.

**SPIKA:** Sasa tunaendelea nilisema Mheshimiwa Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuzungumza juu ya Azimio ambalo lipo mbele yetu. Nataka kujikita kwa mambo mawili, matatu tu. Kwamba nchi yetu, kama kuna kitu inahitaji sasa hivi ni kwamba itawalike kwa amani na mshikamano. Hili ni jambo ambalo ni muhimu sana, zaidi katika wimbi ambalo linaonekana sasa hivi kwenye runinga. Nchi itawalike vizuri pia Bunge liweze kufanya kazi yake kama vile wananchi wanavyotegemea lifanye, pia kwa amani. Kitu chochote ambacho kitahakikisha kwamba Watanzania tunakaa na amani na Watanzania tunafanya mambo yetu Kitanzania na kiundugu wa Kitanzania, kwa maoni yangu inafaa kiungwe mkono. Kitu chochote kile ambacho kinashabikiwa ili nchi isitawalike kwa njia yoyote ile, kwa migomo, kwa maandamano na mambo kama hayo na mauaji, mambo haya lazima tuyakemee wote na tuyakatae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania kwa uchaguzi ambao tumemaliza walichotupa na mimi nawashukuru sana Watanzania, nikizungumza kwa upande wa Kambi ya Upinzani, wametuongezea Wabunge wa Kambi ya Upinzani, hili ni jambo zuri la kuwashukuru Watanzania na wametuongezea Wabunge wa Kambi ya Upinzani ili kujaribu kutafuta njia ya kuimarisha upande mwingine wa shilingi. Nina hakika ndiyo nia hiyo na sisi wote tuliokuwa kwenye majukwaa, tulikuwa tunasema tunataka mfumo wa vyama vingi na tupate mfumo wa uchaguzi ambao utaturahisishia kuwa na Wabunge wengi wa aina mbalimbali katika Bunge la Tanzania ili kila Mtanzania kwa njia tofauti apate njia ya kushinikiza maamuzi katika Taifa lake.

Mheshimiwa Spika, najua, mfumo wa uchaguzi tulionao haujawa mzuri. Najua wengi wetu hatupendi kabisa *First-Past-the-Post* na leo nimejibiwa swali hapa na hilo swali halikuzungumzia mchango mkubwa unaotuharibia uchaguzi, mchango wa pesa, nasema mara nyingine nilikosea kuwaambia Watanzania mapesa kibao labda tungefanya jambo lingine. Pesa ndiyo inaharibu uchaguzi wa nchi hii na ndiyo maana wengi wetu nafikiri tungepata uchaguzi *through propotional representation* yaani uchaguzi wa uwiano, labda hiyo ingeondoa hii silaha kubwa ya kuwazuia watu waingie katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na mapungufu yote yanayotokea, ukishindwa, umeshindwa. Unaweza ukapiga, ukasema sababu za kila aina na sababu zenyewe zinaweza zikawa nzuri lakini umeshindwa. Wale walio Wabunge ukishindwa kama una

sababu nzuri unapeleka kortini ndiyo mahali pa kupeleka mambo haya. Kwa bahati mbaya Katiba yetu ilivyokuwa Urais kama mimi nilivyoshindwa Urais, unakaa nyumbani unalia tu, lakini umeshindwa na hakuna mahali pengine, hii ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kuwaambia ndugu zangu wote ambao wanaisikiliza, Watanzania wana shauku ya Kambi ya Upinzani iliyo na nguvu na kama kanuni zetu zina vipengele ambavyo vinaweza kutumika vibaya kuidhoofisha Kambi ya Upinzani, yale ni matumizi mabaya ya Kanuni, kama hili limedhihirika na linaonekana.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri basi na nawashukuru wale waliokaa jana na nashukuru pia kwamba kulikuwa na watu mbalimbali pamoja na Vyama vya Upinzani vilikuwepo katika hicho kikao, wakakaa wakaona kwamba tafsiri kumbe ndiyo inayotupa nafasi ya kudhoofisha Kambi ya Upinzani, kwa kuwa wameona hilo na mimi baada ya kuitafakari, hilo lipo na ndugu zangu, watu wa CHADEMA natumia nafasi hii kulisema hilo kwamba jamani punguzeni hasira, punguzeni jazba, tutengeneze Bunge linalotegemewa na wananchi huko nje.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wazuri sana katika CHADEMA na sitaki kuwataja, wengi wanajijua na Watanzania wanawategemea na kama kunafanywa *campaign* kuna baadhi ndani ya CHADEMA, mmoja ananiangalia hapa, nitafanya *campaign* mimi mwenyewe apate nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa mojawapo ya Kamati, watu wazuri na sisi wote ni Watanzania wazuri. Hakuna Mtanzania ambaye ni mbaya kwa sababu ya chama chake na uadui huo tusiundeleeze ukiwa CCM mbaya wapi, ukiwa CHADEMA ndiyo umekuwa mzuri nani kakwambia, ukiwa UDP wewe sijui nini, hapana tusiweke *judgment* kwa watu kwamba wewe CCM una mambo yako ya ki-CCM mimi siko CCM na nilishasema tangu miaka mingi lakini usinichukie mimi kwa sababu siko CCM. (Makofi)

Mimi siko CHADEMA, usinichukue kwa sababu siko CHADEMA, na mimi sitakuchukua wewe kwa sababu haupo UDP. Nina hakika nia ya mabadiliko haya ni kuwarudishia Watanzania matumaini ya kujenga Kambi ya Upinzani yenye nguvu, naomba ndugu zangu wote tuache mambo ya majukwaa kule, turudi hapa tujenge Bunge litakaloleta matumaini kwa Watanzania na Bunge lile ni lile ambalo lina Chama Tawala na lina Vyama Vingi ambavyo vinakiangalia hicho Chama Tawala. Kwa ninyi watu wa Chama Tawala nawaomba kitu kimoja, mambo ya kura sasa yamekwisha mtawale, *govern the country*. (Makofi)

Ukiona watu wanafanya hovyoyovyoyo *stop it*, ndiyo kazi yenu na sisi tutawaambia hivyo na naomba hata Mheshimiwa *President* tumsaidie atawale nchi hii, baada ya miaka mitano awakabidhi watu wengine labda sio Mrema au mimi lakini Mtanzania mwingine apigiwe kura na yeye tutamuunga mkono atawale nchi hii baada ya uchaguzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kabisa badiliko hili au Azimio hili kwa sababu moja tu kubwa, litatutengenezea Kambi ya Upinzani iliyo na nguvu na ndiyo lile ambalo Watanzania wanategemea katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. (Makofi)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na kwa hakika Mungu anapaswa kupewa sifa maana hata kusimama hapa leo hii ni kwa sababu ya uweza wake. Lakini na ndiyo maana Mchungaji Rwakatare leo amekaa karibu na mimi hapa najua upako umenikaribia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nianze kum-*quote* Mheshimiwa Cheyo, sisi kama Chama kinachounda Serikali uchaguzi umekwisha sasa tutawale, Bunge ni Chombo kitakatifu sana na Watanzania wanatuomba ili tuweze kufanya kazi yao vizuri. Matarajio yao ni kwamba tutajadili mambo yanayogusa shida zao lakini tusigeuza hiki kama kijiwe cha kuleta fujo za kwenye Kampeni na kutuhumiana ovyo na wakati mwingine kuvunja Kanuni na kudai ujumbe umefika kwa makusudi. Kuna haja ya kuangalia Kanuni zetu pia. (Makofi)

Maana mtu ananyanyuka tu anasema jambo analolijua ni kinyume na Kanuni halafu anaambiwa, afute kauli yake tu halafu imekwisha, halafu anasema tena kuna haja ya kuangalia je, akirudia hivyo afanywe nini? (Makofi)

Matarajio ya Watanzania ni kuona tunawapa kile wanachokitajaraja, wana shida za maji, za afya na shida mbalimbali, ndiyo mambo ya ku-*address* hapa. Masuala ya kampeni, masuala ya vurugu za kwenye majukwaa yamekwisha na Cheyo kasema vizuri, CCM sasa tutawale na tumsaidie Rais wetu kutawala. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mgogoro uliokuja hapa na uliosababisha Kamati ya Kanuni na nikushukuru kwa kunitua na mimi, umeletwa na watu wanaotoka kwenye upande mmoja katika Bunge, Wapinzani, Mheshimiwa Kafulila na Mheshimiwa Hamad Rashid wanalalamika na kunung'unika, kusema wanatengwa na waliopata Wabunge wengi kwa maana ya Chama fulani kilichopo katika kambi yao, CHADEMA. Sie kama CCM tumehusika tu katika kusaidia kutoa mawazo kikanuni na hapa tunaendelea kutoa mawazo hayo, walioanza kusema ni wao. Sasa tuhuma kwamba wale CCM, wale waumini wa CCM, inatoka wapi? Huko ni kudhalilishana na pengine ni kuwa na ufahamu ambao hautoshi katika kujua umuhimu wa Kambi ya Upinzani Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu unatokana na kutokuwepo kwa tafsiri ya Kambi Rasmi ya Upinzani, katika Kanuni yetu, haikuwepo hiyo tafsiri, tafsiri iliyo katika Kanuni fungu la 3 inatafsiri tu kiongozi wa Kambi ya Upinzani lakini haitafsiri Kambi Rasmi ya Upinzani ni kitu gani. Niseme hata katika Azimio hili lililoletwa, kusema ni mabadiliko ya Kanuni, sio mabadiliko ya Kanuni, hii ni nyongeza ya tafsiri, kwa hiyo, hatubadilishi hapa Kanuni. Hapa ni kwamba waliokuwa wanatafsiri kila mmoja livutie upande wake na mgogoro ulikuja kutokea kwenye kifungu cha 14 na 15.

Nyongeza hii inayoleta tafsiri ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapaswa kwa namna yoyote ile iwepo ili kuondoa kutokueleweka vizuri kwa

vifungu vilivyokuwepo na ambavyo kwa tafsiri za kisheria, mimi kama wanasheria, ninaiona kabisa ilikuwa wazi na wala mabadiliko haya yalikuwa hayana hata ulazima wa kuletwa labda kwa maana ya kutafsiri tu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 14(2) kinazungumzia Wabunge wote wa Upinzani wanaweza kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani iwapo idadi yao itakuwa si chini ya asilimia 12.5. Wabunge wote wanaweza kama hakuna chama kinachofikisha asilimia 12.5, basi watajumlishana wote na wataweza kuunda ile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda Kanuni ya 15(2), Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atateuwa Wabunge wa Chama chake au Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani, maana yake basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni ile inayojumlisha Wapinzani wa Vyama vyote. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Sio kweli.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, kusema kwa sababu Chama cha CHADEMA wana Wabunge wengi na wanapata idadi hiyo ya wingi inawapa haki tu ya wao kumchagua tu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani maana hata wakikaa wenyewe Wapinzani wote kwa namna yoyote wataamchagua wa CHADEMA. Kwa hiyo, ndiyo maana wanapata haki hiyo ya kwamba wataamchagua Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Lakini wataunda Serikali kivuli, Mheshimiwa Mbowe ndiyo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, yeye ataunda Mawaziri Vivuli, kwa hiyo, watapata hiyo haki. Hata Mnadhimu wa Upinzani atatokana na wao wenyewe, watapata hiyo haki, lakini kusema Wabunge wengine wa Vyama vingine vya Upinzani hawapati haki hata ya kugombea nafasi ya Uenyekiti wa Kamati, huku ni kuwaonea na kuwanyima haki yao ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 ya Katiba yetu inatoa haki ya mtu kuchagua na kuchaguliwa. Unaposema kwa kuwa wewe huna nafasi kubwa katika Upinzani wetu basi usigombee hata Uenyekiti ni sisi wenyewe CHADEMA ndiyo tugombee peke yetu, naona *it is a bad interpretation* na ni kinyume cha Katiba na kwa maana hiyo kinachotaka kuoneshwa hapa na wenzetu wa CHADEMA ni kwamba wameonewa katika hili jambo. Kwa tafsiri iliyopo katika Kanuni hizi, ujumbe huu usiende kwa wananchi walio nje, wanaotusikiliza, kwa tafsiri wanayoitaka wao, lakini tafsiri nzuri ni ile ambayo inawaweka wao kuwa wamoja, maana mantiki na msingi mzima hapa ni kuwafanya Kambi yao iwe na nguvu. Huwezi kuwa Kiongozi halafu hupendi kuungana na wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, inaonyesha kasoro na upungufu mkubwa kama utakuwa unapunguza wigo wa mamlaka uliyonayo, unaunda tayari matabaka, unaweka ubaguzi katika kitu kidogo tu ulichokipata kama alivyosema ndugu yangu Kafulila, je tukikupa kikubwa itakuwaje? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimeanza kupata hofu ya namna tutakavyoishi katika Bunge hili, lakini kwa mila na desturi ya sisi Watanzania, tuwe na staha. Watanzania watatuona vizuri zaidi na kwamba tunafanya kazi yao, endapo tutaendelea kuheshimiana kwa mila na desturi za Kitanzania na tusiige Mabunge mengine ambako watu wanafanya vurugu, watu wanazomeana, nadhani Watanzania hawakitegemei kitu hiki.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono Azimio hili.

**SPIKA:** Ahsante. nimwite Mheshimiwa Kairuki, atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. ANGELLAH J.M. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Aidha, napenda pia kuipongeza Kamati ya Kanuni za Bunge kwa busara kubwa iliyotumia wakati ikijadili hoja hii iliyoko mbele yetu. Wajumbe walichangia kwa umakini mkubwa uliojaa busara na hekima za hali ya juu. Kwa kweli hoja hii ilikuwa na ubishi mkubwa, lakini watu walitumia busara zao na elimu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, hapa hoja ambayo ina mgogoro ni tafsiri ya “Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni”. Kwa kweli Kanuni ziko wazi kabisa tena bayana, ukiangalia Kanuni ile ya 14(2) ya Kanuni zetu za Bunge, Toleo la 2007 zinaeleza kabisa kwamba Kambi hii inaundwa na Wabunge wote na inatoa msisitizo, neno “wote” ambao wapo kwenye Upinzani kutokana na Wabunge wote wa Vyama vya Upinzani Bungeni hapa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Kanuni ya 14,15 na 16 za Kanuni za Kudumu za Bunge zinaelezea mchakato mzima wa hatua ambazo zinapaswa kufuatwa katika kumchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya ya Upinzani na baada ya hapo, idadi ya Wabunge ambao wanapaswa kuwa katika Kambi hiyo.

**SPIKA:** Sio kengele yako mama.

**MHE. ANGELLA J. M. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunilinda. Haina ubishi kwamba Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni anatoka CHADEMA na kwamba wamekidhi asilimia 12.5 inayotakiwa. Pia haina ubishi, ukisoma iko wazi kabisa. Nadhani CHADEMA ni kwa makusudi wanaamua kutotaka kuliona hili, inaeleza kabisa kwamba ni Wabunge wote na Wabunge wote wanajulikana kwamba ni Wabunge wote wa vyama vya *NCCR, CUF, TLP, UDP* na CHADEMA.

Mheshimiwa Spika, ni vema tusichanganye dhana hizi mbili. Dhana hizi zina mahusiano lakini ni dhana tofauti, kwa sababu “Kiongozi” ni Kiongozi na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inajulikana. Katika Mabunge yote ambayo na sisi tunafuata utaratibu huo, kuna Kambi mbili tu Bungeni. Kambi inayotokana na Chama Tawala ambayo ndiyo inaongoza Serikali pamoja na Kambi ya Upinzani. Hebu tujiulize, hivi Kambi hii Rasmi ya Upinzani ingekuwa haijafikisha asilimia ya idadi ya Wabunge

wanaohitajika, kweli hapa tungekuwa tunajadili suala hili na wangetambulika? Au sio tu kwamba, tungefahamu kwamba kuna Kambi ya Upinzani, lakini sio Kambi Rasmi inayotambulika?

Mheshimiwa Spika, ningependa kuunga mkono Azimio lililowasilishwa ili marekebisho yafanyike yatakayoweza kuingiza tafsiri ya neno “Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni” kama ambavyo imewasilishwa na Mheshimiwa Naibu Spika ili kuweza kutatua mgogoro huu ambao kwa kweli hauhitajiki na kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Tundu Lissu, atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge hili Tukufu na jana wakati Kamati imekaa nilipinga Azimio hili na naomba niweke rekodi kwenye Bunge lako Tukufu kwamba msimamo wangu kuhusiana na Azimio hili haujabadilika. Barua ambayo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa David Zakaria Kafulila walikuandikia ilikuwa ya kuomba mabadiliko ya Kanuni ya 113(11) inayosema kwamba Wenyeviti wa Kamati za Usimamizi wa Fedha za Umma watatokana na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Walioandika barua, walisema wazi kwamba lengo la kuomba mabadiliko ni ili wao waruhusiwe na Kanuni kushika hizo nafasi za Uenyekiti wa Kamati.

**SPIKA:** Tafadhali, Mheshimiwa Mbunge sio kushika, kugombea.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Waruhusiwe kugombea Uenyekiti wa hizo Kamati ambapo kwa sababu vyama vyao havikufikisha asilimia 12.5 inayotakiwa na Kanuni ya kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani wasingeweza kugombea. Kwa hiyo, lengo la mabadiliko ya Kanuni kama walivyoomba wenyewe ni waruhusiwe kugombea wao nafasi washikilie Kamati za Usimamizi wa Fedha za Umma. Hakuna lengo lingine, ni ili wapate madaraka ambayo wapiga kura wa Tanzania hawakuvipa vyama vyao, hawakupata kura za kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa Bunge letu Tukufu pamoja na mambo mengine, linaongozwa na mila na desturi za Mabunge mengine yanayofuata utaratibu kama wetu. Mila na desturi za Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Kanuni ya 2(2), utamaduni, mila na desturi za Mabunge ya Jumuiya ya Madola kila mahali, ni kwamba Chama kikubwa Bungeni huwa kinaunda Serikali, kinakuwa *A Government Party*, chama kinachofuatia kwa ukubwa kwa mila na desturi hizo huwa kinaunda *The Official Opposition*. Waingereza wanaita *Her Majesty's Loyal Opposition*. Kwa hiyo, *the prerogative* ya kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani huwa ni *prerogative* ya wale waliopewa kura na wananchi kuwazidi wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo moja. La pili, kwa utamaduni huohuo ambao tumekuwa tunaufuata, wale wanaokuwa wa pili kwa wingi wa viti Bungeni, *The Official Opposition* ndiyo wanaoshikilia Uenyeviti wa Kamati zinazosimamia fedha za Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni *tradition* ya muda mrefu sana, *it goes back centuries*. Sasa pendekezo la Azimio hili ni la kuachana na mila na desturi hizo, pendekezo lililoko Mezani ni la kuruhusu chama chenye Mbunge mmoja Bungeni kuwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Fedha za Serikali; kwa mfano, chama chenye Wabunge wanne kiweze kushikilia nafasi ya Uenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Fedha za Mashirika ya Umma. Chama chenye Wabunge ishirini na nne ambao 22 kati yao ukijumlisha kura zao hazifikii kura za Jimbo moja la Mheshimiwa John Mnyika, waweze kushikilia Uenyekiti wa Kamati ya Fedha za Halmashauri za Mitaa. *We are breaking with tradition*, tunaondokana na utamaduni wa Mabunge ya *Commonwealth* ambayo chama kilichopewa kura nyingi kuliko Vyama vingine vya Upinzani kinashikilia *oversight committees* hii ndio moyo wa hili Azimio. Hii ndiyo *heart* ya hili Azimio. Sasa siyo hayo tu, lengo *whether intended or unintended* ya mapendekezo hayo itakuwa ni kuuha Upinzani Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini, kama Azimio hili likipitishwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha za Serikali atakayetokana na chama chenye Mbunge mmoja...

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ENG. STELLA A.M. MANYANYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 64 tunafahamishwa kwamba, Mbunge yeyote anapoonea, hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Mimi kwa mtazamo wangu, tunapomchagua Mwenyekiti wa Kamati, hatumchagui kwa kuangalia anaongoza Jimbo lenye watu kiasi gani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naona suala hili linapotosha uelewa wetu na wa wananchi. Naomba mwongozo Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kamati za Bunge zinaundwa na vyama vyote halafu mtachagua Wenyeviti wa Kamati. *Watchdog Committees* toka zamani tulikubali zitaongozwa na Upinzani. Sasa Upinzani Rasmi kwa tafsiri ya Kanuni ya 14(2) ni Wabunge wote wa Upinzani, ndiyo tafsiri iliyopo pale. Haikuwekwa *express* ndiyo maana leo tumesema tuingize tafsiri hiyo ili iwe *express* na ijulikane hivyo. Kwa hiyo, watakapokwenda kwenye Kamati, watachagua Mwenyekiti si kutoka Chama Tawala, watachagua Mwenyekiti kutoka Chama cha Upinzani. Endelea Mheshimiwa Tundu Lissu. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, tunawafahamu kwa sababu wameomba kwa barua, kwa maandishi kwamba wanataka wagombe nafasi za Uenyekiti wa Kamati za Usimamizi wa Fedha.

### **TAARIFA**

**SPIKA:** Simwoni hata anayesema taarifa ni nani, yuko wapi? *Okay* sawa.



**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), napenda nimtaarifu Mheshimiwa Lissu kwamba hizo mila na desturi anazozungumzia za Mabunge ya *Commonwealth* kuhusiana na nafasi hizi za vyombo vya fedha, muda mfupi pia tumeambiwa kwamba mila na desturi ya Bunge letu la Tisa, Waheshimiwa Wabunge wa Vyama vya Upinzani ambavyo vilikuwa na viti vichache kwa mfano Chama cha Mheshimiwa Cheyo, Mheshimiwa Kabwe, waliweza kuwa Wenyeviti wa vyombo vikubwa. Sasa ni vipi mila na desturi ya Bunge letu sisi wenyewe tuone si nzuri mpaka ahangaike kuogelea mila na desturi ya Mabunge mengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Haya taarifa unaweza kukubali au usikubali. Ukweli ni kwamba hizi mnazoita mila na desturi kwanza tunaanza na za kwetu, kama hazipo za kwetu ndipo tunaenda huko kwingine, za kwetu ziko *very clear* toka mwaka 1995 huu utamaduni tunaufuata. Endelea Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kama zingekuwa *clear* tusingekuwa hapa tunajadili Azimio hili, kuna tatizo, ndio maana tunajadili Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba niendeleo, nimesema kwamba lengo la Azimio hili *whether intended or otherwise*, ni kuua upinzani na naomba niseme kwa nini nasema hivyo. Chama cha Wanchi *CUF*, kina Makamu wa Rais, kimeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Kwa maneno yao wenyewe, wamesema Upinzani umekufa Zanzibar, hakuna Kambi ya Upinzani. Sasa...

**SPIKA:** Zanzibar?

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Ndiyo Mheshimiwa. Namna pekee ya *CUF* au *NCCR* kuchaguliwa kwenye *Oversight Committee* za Fedha za Umma, ni kwa kupigiwa kura na chama chenye Wabunge wengi Bungeni, Chama cha Mapinduzi, ndiyo maana wanapiga makofi namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itakayojengwa kwa kura za CCM, hatuwezi, haiwezekani wale ambao tunataka kuwaondoa madarakani wakatujengea Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hayo tu, tukiruhusu Chama chenye Mbunge mmoja kama cha Mheshimiwa Cheyo au chenye Wabunge wawili au wane, kushikilia Uenyekiti wa *Oversight Committee* kwa kuungwa mkono na Chama Tawala, maana yake ni kwamba ulinzi wa fedha za umma utapotea.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kazi hiyo imefanywa vizuri sana, *shut your mouth*.

**MBUNGE FULANI:** Acha ubinafsi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hebu acheni maneno ya chini chini, nimempa nafasi aendelee.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Kwa utaratibu huu, kama Azimio hili litapitishwa kwa utaratibu huu, Watanzania wasahau kusikia ufasadi kama wa *EPA*, wa Richmond...

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, hapa mzungumzaji ametumia lugha nyingi sana ambayo inaudhi na anakiuka Kanuni ya 64(g). Kwa hiyo, naomba aifute hiyo *statement* yake pamoja na ile ya kuwaondolea haki Wabunge wengine kwa sababu Wabunge wote wana haki sawa katika Majimbo yote kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 66 ambayo inasema Wabunge wote wako sawa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya tuendelee Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kama hoja hiyo ya Wabunge wote wako sawa ni hoja yenye mashiko, wangepombea hapa wa upande wa pili lakini Uenyekiti wa *Oversight Committee's* kila mahali unashikiliwa na Chama cha Upinzani Rasmi Bungeni, Chama chenye Wabunge wengi kwenye Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Nimesema, matokeo ya ku-*adopt* Azimio hili ni pamoja na ku-*weaken Parliamentary Oversight ya Public Finances*, hatutasikia tena *EPA* au *Dowans* au *Richmond* humu Bungeni kama hao wataruhusiwa.

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kusimamia muda mrefu lakini niliona si busara lakini kwa kauli hii ya mwisho ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu anaendelea kuizungumzia maana yake anataka kuwaambia Watanzania kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hawana uchungu na pesa za nchi hii, jambo ambalo si la kweli. (*Makofi*)

Anataka kuwaambia Watanzania kwamba Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi ni wezi jambo ambalo si la kweli. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba hata suala la *Richmond* ambalo lilikuja humu ndani ya Bunge lilitokana na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sio kweli

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kumbukumbu ziwewe sawa kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kama walivyo Wabunge wa Vyama vingine, wote wana uchungu na pesa za nchi hii, wana uchungu na

mambo ambayo yanaendelea ya kuvunja maadili kwa upande wa viongozi. Ahsante Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kamati zinaundwa na Vyama vyote ila *Watchdog Committees* ndio zinaongozwa na Upinzani na hawaongozi peke yao na Wabunge wengine wanakuwemo sio kwamba yule akiwa Mwenyekiti, basi yeye anaendesha Kamati peke yake. Zile Kamati zinaundwa na Vyama vyote tena tunajitahidi Vyama vyote vinakuwepo kwenye Kamati hizi ila atachaguliwa Mwenyekiti wa Kamati hizi kutoka Kambi ya Upinzani, hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa, endelea Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Ahsante Mheshimiwa Spika.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Kanuni ya 64(a) inasema Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Kwa kuwa mfululizo wa mazungumzo ya Mheshimiwa Tundu Lissu yanaonekana ni ya kupotosha, je, hakuna utaratibu wa kumwelekeza apumzike ili asiendelee kupotosha umma? Hamna namna ya kuziba hilo tundu? (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Tundu Lissu endelea kusema, atajibiwa.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Acheni utoto.

**SPIKA:** Sasa mkitoa miongozo juu ya miongozo hatutakwenda. Haya Mheshimiwa Tundu Lissu endelea.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, hoja hii haiendi kwenye uchaguzi wa Wenyeviti wa *Oversight Committee's* peke, tukiruhusu haya mambo, basi tufahamu kwamba Wabunge kwa zile nafasi ambazo Sheria zimesema Wabunge watawakilishwa, hizo nafasi vilevile zitaamuliwa kwa niaba yetu na kile Chama chenye Wabunge wengi Bungeni. Vyombo kama *SADC Parliamentary Forum* ambayo tayari tunafahamu kilichotokea, vyombo kama *PanAfrican Parliament*, vyombo kama *East African Legislative Assembly* na vyombo mbalimbali ambavyo Sheria inasema ziwakilishwe na Wabunge, Wabunge hawa watatokana siyo na Chama ambacho Watanzania wamekipa ridhaa ya kuwa Chama Kikuu cha Upinzani bali watatokana na Vyama ambavyo...

### **TAARIFA**

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Taarifa Mheshimiwa Spika

**SPIKA:** Taarifa, hata anayesema simwoni, haya endelea.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimtaarifu Mheshimiwa aliyekuwa anaongea kwa kutumia Kanuni ya 68(7) kwamba Wabunge ambao wanakwenda kwenye Bunge la *East African Community* si Wabunge wa Bunge hili kama anavyosema, ni wananchi wa kawaida kwa kupitia Vyama vyao ambapo Bunge hili ni wapigakura. Napenda kumsahihisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa tunataka tumalizie kwanza hata muda umekwisha, malizia Mheshimiwa Tundu Lissu, ulibakiwa na dakika zako tatu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, hili Azimio ambalo linapendekeza tafsiri ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa ni Kambi ya Vyama vyote vya Upinzani vyenye uwakilishi Bungeni, vilevile ni *impractical*. Kwa sababu gani? Kuna Vyama zaidi ya vinne humu ndani ambavyo viko kwenye Upinzani, vina Katiba tofauti, vina *Parliament Caucus* tofauti, vina Kanuni tofauti, huyo Kiongozi wa Upinzani au Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani, ata-*reinforce* vipi *discipline* ya Kambi ambayo si ya Chama chake, Kambi ambayo Chama kingine kinashirikiana na Chama Tawala, wako Serikalini, itakuwa *impractical*.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile, hii si ndoa ya mapenzi, ni ndoa ya kulazimishwa. Hatuko tayari na hatutakuwa tayari kuwa kwenye ndoa na Chama ambacho kina ndoa nyingine ukivuka Bahari ya Hindi kwenda Unguja. Sheria za nchi yetu zinaruhusu *polygamy* haziruhusu *bigamy*, zinaruhusu ndoa ya wake wengi, haziruhusu ndoa za waume wengi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwisho...

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kidogo, anaposema ndoa, anamaanisha nani na nani walioana?

**SPIKA:** Naomba amalize kwanza. Hebu endelea Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Naomba nimalizie kwa kusema kwamba sisi kama Chama Kikuu cha Upinzani Tanzania chenye Wabunge 48, chenye asilimia 13.7 ya Wabunge wote...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Hakitakuwa tayari kwa mazungumzo ya namna hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa, msemaji wa mwisho.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ni nani anayeomba utaratibu? Nimemwita Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sidhani kama nitauvunja utaratibu. Kwanza, nianze kwa kusema naunga mkono Azimio hili. Nitabanaisha tu kuwa hizi Kanuni ni mali ya Bunge hili, zimekuwa zikibadilishwa kwa faida za Wabunge wa Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni shaidi. Tumeanza Bunge la Vyama Vingi hapa pamoja na utamaduni huo wa Jumuiya ya Madola lakini Bunge la 1995/2000 Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali alikuwa Mheshimiwa Pius Mbawala kutoka Chama cha Mapinduzi wala hakuwa Mpinzani, wala hapakuwa na mgogoro. Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma ambayo miye nilishakuwa Mjumbe wake, zote mbili alikuwa Mheshimiwa William Shellukindo, wala hapakuwa na mgogoro. Mimi sikuelewa kuwa kumbe zogo lote hili watu wanataka nafasi ya Uenyekiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilidhani tunarekebisha Kanuni kwa faida ya Watanzania, kwa faida ya kuliboresha Bunge, kumbe ni kwa sababu ya Uenyekiti. Hebu tukumbuke tunaposema kuwa watu wanaokuwa na Wabunge wachache hawawezi kufanya kazi vizuri, Bunge lililopita sisi tulikuwa na Wabunge wengi zaidi kuliko Chama kingine chochote cha Upinzani lakini Kamishna wa Bunge kutoka Upinzani alitoka CHADEMA, hatukuwa na mgogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa *PAC* alitoka *UDP*, hatukuwa na mgogoro. Mwenyekiti wa *LAAC* alitoka CHADEMA, hatukuwa na mgogoro. Mwenyekiti wa *POC* alitoka CHADEMA, hatukuwa na mgogoro, kwa sababu tulikuwa Kambi moja. Unapokuwa na wenzako ni lazima ukubali mara nyingine unapoteza, mara nyingine unapata, kwa nini hatuna ukomavu katika mambo madogo kama haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri lazima tuelewe, wanaochagua Wenyeviti wa Kamati, ni Wajumbe wa Kamati kwa ujumla wao. Mimi katika Bunge lililopita nilishagombea nafasi ya Ubunge wa Afrika lakini kwa sababu Wabunge hawakunipa kura za kutosha sikununa alipopata Mheshimiwa Cheyo, si ndiyo utamaduni ulivyo na walionipiga kura walikuwa Wapinzani na wa CCM lakini sikushinda. Sasa huko tunakokwenda, watu watagombea, watakaoshinda wataongoza Kamati, nongwa ya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu nimeanza kushtuka, sasa inaonekana pana lugha za ajabu ajabu za kama kudharau hivi Wabunge wa Zanzibar, *this is serious*. Jambo hili naomba ulikemee sana. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Napenda watu waelewe katika mgawano wa *share*, kuna kitu kinaitwa *golden share*, Bunge la Zanzibar

pamoja na udogo wake lakini katika suala zima la Muungano wa Tanzania, ina *golden share* katika Muungano huu. Kwa hiyo, wale watu 6,000 waliomchagua Mbunge wasilinganishwe kabisa na watu milioni moja waliomchagua Mbunge mwingine kwa sababu mwisho wa siku wote ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia si kweli kuwa Wabunge wa Zanzibar hawaongozi Kamati, Mheshimiwa Abdulsalaam Issa Khatib, Mbunge wa Makunduchi, wapiga kura wake ni 10,000 tu katika Bunge lililopita alikuwa Mwenyekiti wa Viwanda na Biashara. Ni vizuri kama mambo hatuyajui tukauliza kuliko kukurupuka kusema na inaonekana kuna woga kuwa watu hawatakuwa Wenyeviti wa Kamati, wa nini woga huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Shakespeare* anasema “Waoga hufa kabla ya wakati wao lakini hawayaonji mauti isipokuwa mara moja tu”. Sasa tuna wasiwasi wa nini? Turekebishe Kanuni zetu, watakaopata Uwaziri Kivuli watapata, watakaopata uongozi wa Kamati watapata, mwisho wa siku hakuna ripoti inayokuja ndani ya Bunge hili kama haikuridhiwa na Kamati hata kama Mwenyekiti atakuwa anatoka Upinzani, hivi anaweza akaleta ripoti yake hapa inayokuja si ripoti ya Kamati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Richmond* walikuwemo Wapinzani walikuwemo CCM lakini aliyeleta hapa hoja alikuwa Mheshimiwa William Shellukindo, aliyekuwa Mbunge wa Bumbuli. Kwa nini tuna-*trivialize issues* kwa sababu ya ubinafsi? Tukubali ukweli ulivyo. Utamaduni tunaotaka kuujenga ni wa umoja. Bunge hili ni shahidi, Rais ana Wabunge 200 na Mawaziri 26 lakini amejitahidi kuteua Mawaziri hao katika kila kona ya nchi yetu ili kuonyesha *integrity*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kiongozi wa nchi anathubutu kuchukua hatua hiyo ya umoja, kuna nongwa gani sisi watu tusiofika mia mbili kuwa wamoja katika Kambi na tumekuwa wamoja hapa, tumekuwa wamoja mwaka 1995, 2000 na 2005, kumbe nongwa ni Uenyeviti wa Kamati, mimi sikuelewa, yanakuja maneno ya ajabu ajabu, Kanuni nyingi zinaletwa, mwisho wa siku ...

## TAARIFA

**SPIKA:** Eeeh! Nani anasema juu ya Taarifa?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68.

**SPIKA:** Sijakuona muda mrefu Mnyika, ulikuwa wapi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Niko hapa Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Haya, ahsante, endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda tu kumtaarifu mzungumzaji kwamba mifano anayoitumia haiendani na suala tunalozungumzia hapa. Mfano wa Rais kuunda Baraza la Mawaziri na kuchukua watu kutoka katika maeneo

mbalimbali, aliwachukua kutoka ndani ya Chama chake. Hivyohivyo basi, kwa kuwa Kanuni sasa hivi zinasema bayana, Wenyeviti hao watatoka Kambi Rasmi ya Upinzani maana yake ni kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani ndiyo inaamua sasa watoke maeneo gani, kwa maana lazima watokane na Kambi Rasmi ya Upinzani.

**SPIKA:** Jamani nyie mnabishana tu, Kanuni ya 15(2) inasema, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani atateua Mawaziri Kivuli kutoka ama kwenye Chama chake akitaka ama atachagua kwa wenzake wale kwenye Kambi ya Upinzani. Hiyo ndiyo *relevant*, hii habari ya Kamati sijui mnaiingizaje hapa, tunaendelea. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa Bunge letu, unapopewa taarifa, unahiari ya kukubali na kuikata, hiyo taarifa yake mimi siitaki. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo tunaelimishana hivi, si suala la kuwa ukisimama taarifa ni taarifa tu, unayempa taarifa ana haki ya kuikubali au kuikataa, ndiyo tunajifunza hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaendelea, napenda sasa nigusie kidogo katika suala hili analosema kuwa Rais anachukua Mawaziri wa Chama chake na sisi hatumkatazi atakayekuwa Mwenyekiti wa Upinzani kuunda hiyo Serikali atakayo, hatumkatazi hata kidogo lakini tunachokisema, tunataka Umoja wa Vyama vya Upinzani ndani ya Bunge kama Watanzania waliotuleta hapa na moto tuliokuwa nao tokea nyuma. Sasa hii hofu ya kuwa sijui *CUF* wako pamoja na CCM Zanzibar, ni kweli lakini hapa ni Chama cha Upinzani. Ni Serikali mbili tofauti au leo Serikali ya Zanzibar iko hapa?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, yuko pale *by virtual* ya Ubunge wake kwa kuwa yeye ni Mbunge wa Jimbo la Kitope si kwa sababu ya nafasi yake. Lazima tujue tunachokisema, yupo pale kwa sababu yule ni Mbunge wa kuchaguliwa wa Jimbo la Kitope, hayuko pale *by virtual* ya kuwa ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ndio maana siku ile alipokuja hapa yeye hakuombewa nafasi ya kuingia humu ndani kwa sababu haki hiyo alikuwa nayo kwamba yeye ni Mbunge wa Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba watu waangalie Kanuni ya 115(2), mambo haya hatuyasomi. Tusomeni vizuri wazee kuliko kuja hapa, tukapiga makelele mengi hayasaidii kitu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba Bunge hili bila ya kujali kelele za mtu yeyote, tubadilishe Kanuni hii kwa faida ya Wabunge na kwa faida ya Watanzania, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa kuwa muda uliobakia hautoshi kumpa nafasi mtu mwingine, hata hivyo, nikirudi hapa, nitampa mtu mmoja tu, Mheshimiwa Anna Abdallah baada ya hapo nitampa nafasi mtoa hoja, tutakuwa tunafunga hoja hii. Nimefanya hivi kwa sababu

tunarudia, tunaenda nje ya utaratibu, wala hatujadili hoja, nina sababu zote za kufunga mjadala huu.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, nasitisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tulipositisha shughuli za Bunge mchana, nilisema nitampa nafasi mchangiaji mmoja, Mheshimiwa Anna Abdallah, mtoa hoja atakuja kuhitimisha halafu tutafanya maamuzi. Mheshimiwa Anna Abdallah.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niungane na wenzangu kukubali kabisa Azimio lililopo mbele yetu, la kufanya mabadiliko katika majina ya Kamati ni sawa kabisa na pia nakubaliana na kutengua Kanuni ya 153(1) na vilevile nakubaliana kuweka ufafanuzi wa maneno Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Kanuni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja nyingi ambazo zimesemwa katika Bunge hili kuhusu jambo hili tulilolifanya, mimi nimekaa katika Bunge, hiki ni kipindi changu cha nane na katika vipindi vyote nilivyokaa hapa Bungeni, tumekuwa tukifanya mabadiliko ya Kanuni, wakati mwingine makubwa sana kama yale ya mwaka 2007 na wakati mwingine madogomadogo ili kukidhi haja ya wakati, hili ni jambo la kawaida kabisa. Wala hakuna sababu ya mtu ama kikundi cha watu kufikiria kwamba mabadiliko haya yanafanywa kwa sababu ya kukidhi mahitaji ya kikundi fulani, si kweli, tumekuwa tukifanya hivi kutokana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, katika Kanuni yetu, Kanuni ya 15(2) inasema:-

*“Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atateua Wabunge wa Chama chake au Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambao watakuwa wasemaji wakuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara zilizopo za Serikali.”*

Mheshimiwa Spika, ndio kusema Kanuni inatambua kwamba upande wa Upinzani kuna sehemu mbili, sehemu ya kwanza ni Chama anachotoka Kiongozi wa Upinzani lakini Kanuni hii inasema au Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.



Mheshimiwa Spika, sikusikia hata mtu mmoja akipinga Kanuni hii kwa kuwa imo. Sasa kinachopendekezwa mbele yetu ni tufafanue ni nini maana ya Kambi Rasmi Bungeni. Katika mazungumzo yote tangu asubuhi, sikusikia hata mtu mmoja au Mheshimiwa Mbunge mmoja aliyeleta mapendekezo ya tafsiri iweje, wote tunazungumzia tafsiri iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kama Kanuni hii ya 15(2) inatambua kwamba kuna Kiongozi Rasmi wa Kambi ya Upinzani, ambaye atateua Wabunge wa Chama chake au wa Kambi Rasmi, sasa kinachofanyika leo ni kufafanua maana ya Kambi Rasmi. Mimi nashangaa kweli kwa maneno mengi yaliyosemwa leo; tena ni ufundi kabisa wa kupangilia maneno, mbichi, mbivu, ili mradi tunapendezesha tu. Nasema hii ni hatari sana kwa Bunge letu, jambo zuri tunalifanya linaonekana halifai. Nasema hapa sio mkutano wa hadhara wa Chama cha Siasa, hapa ni Bunge la Jamhuri ya Muungano na lugha zetu pia ni lazima ziwe za Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hizi Kanuni ni lazima tuziboreshe sana, mtu hawezi kusema anafuta usemi wake halafu anasema *message sent*, hiyo ni lugha ya mtaani tu, haitujengei heshima. Nikisema kule kwangu kijijini ni sawa au nikiwa kwenye mkutano wa hadhara ni sawa, lakini sio ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesikia maneno ya ajabu sana humu ndani, Mjumbe wa Kamati yako anasema tulipokuwa kwenye Kamati ya Kanuni, alipinga Kanuni. Sasa kwa kuwa wengi hawakuwepo na mimi niseme ni kweli alipinga lakini ni tofauti na hapa Bungeni ambapo ukipata nafasi moja ni basi imetosha, pale ndani ya Kamati ukisema jambo mwenzako pia anapata nafasi ya kuelezea, inakuwa kama ni maswali na majibu, watu wanaelezana. Inavyoelekea kulikuwa na hoja ya nguvu na nguvu ya hoja, nguvu ya hoja ikashinda. Demokrasia inataka wakati nguvu ya hoja inashinda kama hata wewe huitaki ndio basi. Mke wa baba yako hata kama ni mama wa kambo ndio mama yako, kwa hiyo, nguvu ya hoja ilishinda. Kwa kuwa ndani ya Kamati nguvu ya hoja ilishinda na wale waliokuwa wanapinga wakanyamaza, leo wanakuja ndani ya Bunge kusema, basi nataka niseme, kama mnataka kuwa-*adress* watu waliowachagua, wamesikia lakini na wenyewe waelewe kwamba yale mliyoahidiwa kule, sivyo, hapa tunazungumzia nguvu ya hoja sio hoja ya nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la kwamba eti *CUF* ni Chama Tawala! Kwa Zanzibar, sawa. Katiba yetu inatambua kuwepo kwa Zanzibar na Katiba yake. Maridhiano yaliyofikiwa na ni kati ya Vyama viwili Zanzibar. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sio Baraza la Wawakilishi, maridhiano yapo Zanzibar na tuwaachie wao maridhiano yao waendele nayo na ni mazuri kwa afya ya demokrasia ya Zanzibar. Lakini ukisema huku Bara *CUF* ni Chama Tawala, si kweli na mimi nataka niwaambie *CUF* msije mkabweteka, ninyi sio Chama Tawala, ninyi ni Wapinzani tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku moja nilimsikiliza Makamu wa Kwanza wa Rais, aliwaambia watu wa *CUF* kule Zanzibar, “msibweteke kwa kuwa tuko ndani ya

Serikali.” Kazi yao moja ni kuipindua CCM na kushika madaraka ya Serikali, hakusema hivyo?

**MBUNGE FULANI:** Alisema!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Sasa haya ya kusema eti *CUF* ni Chama Tawala, kwa hiyo, msishirikiane nacho; ni hoja dhaifu ndani ya Bunge, haistahili. Kwa hiyo, nasema hili halipo wala halina mantiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kanuni vilevile inatambua kwamba katika Kambi ya Upinzani kuna sehemu mbili, moja ni ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ambaye anaweza kuteua Viongozi wa Chama chake au Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, tafsiri sahihi ya Kambi ya Upinzani, ni Wabunge wote ambao sio wa CCM walio upande ule, ndio tafsiri sahihi na ndio tunayokwenda nayo na wala isitupotezee muda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema malumbano ya kisiasa yalikuwisha, walioshinda wameshinda, waliokosa wamekosa. Nakubaliana na Mheshimiwa Cheyo, aliyesema hebu sasa Serikali itawale maana ndio mtawala, tuache mambo haya ya kupendezesha. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, hiyo ni kengele yangu?

**SPIKA:** Ni ya kwanza, endelea.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme hivi, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, ni cheo kikubwa sana, ni Wadhifa mkubwa sana. Akitoka hapa, hata akienda huko tunakosema *Westminster*, hatasema mimi ni Kiongozi wa Chama fulani, yeye ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Wakati mwingine wanapokwenda huko, wanakwenda Kambi zote, yeye na wa Vyama vingine, hatakwenda na wa Chama chake pekee, kule huwezi ukasema, mimi hawa sio wa kwangu. Kwa hiyo, hadhi ya Bunge inajengwa hapo na tuanze kupatana sisi humu ndani, tuanze kujenga humu ndani, kama humu ndani hatuelewani kwa maneno yaliyotokea humu leo asubuhi, sijui huko nje tutakaaje, kunywa chai pamoja, Itawezekana kweli? Haiwezekani! Tunajenga nyumba moja tusigombanie fito vinginevyo fito au matofali yataunjika, wote tukakosa nyumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa rai kwamba hakuna tatizo la utata wa tafsiri, wala tusiwaingize Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Kafulila katika hili. Wameandikwa katika Azimio kwa sababu wao walileta jambo ambalo Kamati ya Kanuni ililikataa ikasema kinachotakiwa ni kutafsiri tu ni nini maana ya Kambi Rasmi na ndicho kilichofanyika, kwa nini hatukubaliani na hilo? Tuache haya mambo mengine yote

ambayo hayatujengei heshima ndani ya Bunge letu na yanatuletea matatizo yasiyokuwa na sababu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba niseme hivi, nafikiri na Kanuni hizi zinahitaji kuangaliwa upya ili ziwe na meno zaidi ili tuondoe kabisa maneno ya kejeli na kashfa hizi. Hivi CCM kumpigia makofi Mpinzani imekuwa nongwa? Imekuwa dhambi? Kama umesema jambo zuri, ni lazima upigiwe makofi. Humu ndani hata wewe ukisema jambo mimi nikiliona zuri, nitakupigia makofi na usinihakumu, wala sitaki wana CCM wanihakumu kwa sababu nimempigia Mpinzani makofi, kwa sababu nimependezewa na alichokisema, hiyo ndio demokrasia. Nimeshangaa sana leo hapa, tunaambiwa eti mbona hawa wamepigwa makofi na CCM? Hiyo sio siasa ndugu zangu, inavyoelekea wengine tumeingia humu ndani kujifunzia siasa, hapa sio mahali ambapo kuna *cross examination*, hapa hakuna, hapa tunazungumzia mambo ya nchi bila kupotosha jambo lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

### **TAARIFA YA SPIKA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, natoa taarifa hii ili kuondoa upotoshwaji wa tafsiri ya Kanuni, ambao mzungumzaji aliyepita ametaka kuubainisha.

**SPIKA:** Kanuni gani?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, mzungumzaji aliyepita amezungumzia tafsiri ya Kanuni 15(2) ili kuhalalisha dhana ya kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa kusema kwamba Kiongozi wa Kambi ya Upinzani atateua Wabunge wa Chama chake ama Wabunge wa Kambi ya Upinzani. Kwanza, sheria haisomwi kipande kipande, sheria inasomwa kwa ujumla wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, unanza kujadili sheria sasa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, natoa taarifa.

**SPIKA:** Taarifa gani?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ni lazima nijenge hoja ili taarifa yangu ipokelewe na Bunge lako.

**SPIKA:** Ngoja kwanza

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, siitaki kabisa.

**SPIKA:** Kanuni inamruhusu kukataa taarifa yako, ameikataa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mnataka kuficha ukweli? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ukweli gani? Amekataa taarifa yako, ndivyo Kanuni zinavyosema.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hajaisikia taarifa yangu!

**SPIKA:** Anasema, haitaki taarifa yako, naomba ukae chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, *this is nonsense!*

**SPIKA:** Nimekwambia kwa utaratibu wetu, kama jambo fulani hujaridhika nalo, kuna utaratibu mwingine wa kufuata. Huyu unayempa Taarifa akisema haihitaji Taarifa yako ndio hivyo, haitaki sasa, ndio hivi inavyokuwa. Kanuni hiyo ya 15 kinachosemwa, ni kumpa madaraka zaidi Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema atachangia huyu baadaye nitamwita Mtoa hoja. Nilichojifunza ni kwamba...

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Unaniongoza mimi tena? Mimi natoa maelezo, hutakiwi ku-*interfere* napozungumza.

Nachokisema ni kwamba tuna orodha kubwa sana ya wazungumzaji, lakini ukiangalia toka asubuhi ni maneno ya kuzunguka tu hakuna hoja mpya kabisa. Kwa hiyo, ninazo sababu zote za kumwita Mtoa Hoja ili aweze ku-*summarize* halafu tunachukua hatua nyingine. (*Makofi*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kifungu gani? Nani tena?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika, rejea Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, Bunge letu linaongozwa kwa Kanuni, Mila na Desturi na kwa Mila na Desturi hizo, mijadala kama hii inapoendelea, kwa kawaida kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, haswa hoja inapotolewa na upande mwingine, huwa anapata fursa ya kuzungumza, nina taarifa kuwa, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliomba kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine la ziada tu ni kwamba mtiririko wa majadiliano kuanzia asubuhi yalikuwa na sura ya pande mbili; upande mmoja ambao wamezungumza watu saba ukiwa unaelekea upande wa kukataa na upande mwingine ambapo ndio upande ambao maslahi yao yanaguswa kwa maana ya upande wa pili wa Kambi Rasmi ya Upinzani, wamezungumza watu wawili, naomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo basi, pamoja na kuomba Muongozo wako, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni 69(1) kwamba mjadala huu uahirishwe mpaka pale ambapo Kiongozi wa Upinzani atakapopewa fursa ya kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Kicheko*)

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Kwani kuna tatizo gani kwamba azungumze? Azungumze tu na watapiga kura baadaye.

Unajua tatizo lililotokea, hawa wanaandika halafu wanakwambia mimi nataka kuzungumza mwishoni au mwanzoni na mimi siwezi kuongozwa na watu kutoka kwenye *floor*, naongozwa na Kanuni. Zaidi ya hapo, heshima niliyotoa ni kwamba nisingependa kabisa wale Wajumbe wa Kamati ya Kanuni wasipate nafasi ya kuzungumza kwa sababu hili ni Azimio lao, limewasilishwa na Naibu Spika tu kwa sababu wao walipata muda mrefu zaidi wa kulishughulikia. Kwa hiyo, hakuna tatizo kumwambia Kiongozi wa Upinzani azungumze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbowe, nakupa nafasi, zungumza. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru sana kwa kukubali hoja ya kuniruhusu na mimi nichangie nikiwa ni mdau muhimu sana katika mjadala huu unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika mambo machache ya msingi sana kuhusu hoja inayoendelea hapa Bungeni. Nawaheshimu sana Waheshimiwa Wabunge na michango yao yote. Ninaheshimu uzoefu wa baadhi ya Wabunge, lakini vilevile si haki na nitakataa kupuuzwa kwa Wabunge wengine, labda kwa sababu ya uwepo wao Bungeni kuwa ni wa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, ushirika ni jambo la msingi katika maisha ya binadamu, hakuna anayekataa hilo lakini pale Bunge linapopuuza umuhimu wa maridhiano katika ushirika wowote, tunaondoa misingi ya msingi wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi ikiwepo mifano ya msingi kabisa kwamba Bunge la Tisa Vyama vilishirikiana, ni kweli lakini ambacho hakizungumzwi ni kwamba tulikuwa na mazingira gani ya kisiasa wakati wa Bunge la Tisa na leo tuna mazingira gani ya kiasiasa katika Bunge hili la Kumi. Kweli tulikuwa na ushirika pamoja na Vyama vingine katika Bunge la Tisa lakini katika Bunge la Kumi, tumekuwa na tofauti za kimsingi. Kwa tofauti hizi za kimsingi, naomba Bunge lako lielewe, kila Chama kina haki zake na haki yetu ya Chama ama haki ya wenzetu ya Vyama, haiwezi ikaondolewa kwa dhana ya juu juu kwamba tunataka ushirika, Kambi ya Upinzani iwe imara, kuchagua mshirika ni uamuzi wetu, sio uamuzi wa Chama kingine chochote. Vilevile hii ni haki ya Kikatiba, Sehemu ya Tatu ya Katiba yetu, Ibara ya 18 na 20 inazungumzia suala hili, uhuru wa mahusiano kwamba hatuwezi kuingizwa kwenye ndoa ambayo hatujaridhia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ya kisiasa yanatatuliwa kwa muda. Tumetoka kwenye uchaguzi, Vyama vina makovu tofauti, wagombea wana makovu tofauti, kama wagombea ama kama Wabunge ama Viongozi wa Vyama, watafika mahali wakaridhiana washirikiane, ni utashi wao, wapewe muda. Sasa leo mnaniambia mimi ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, sikuja kuomba Uongozi wa Upinzani Bungeni kwa sababu ya maslahi, kwa maana hiyo, naposimama kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kitu cha kwanza ninachoki-*expect* kwa watu naowaongoza ni *trust* na *loyalty*; *trust* ipo wapi katika vijembe nilivyoviona mahali hapa leo? Cha ku-*ensure* ni kwamba eti tunaingia kwenye ushirika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Vyama mbalimbali, kama kweli tunazungumzia maslahi ya Taifa, hatuwezi kuyapata kwa stahili hii. Kupata maridhiano sio kwa wiki moja au mbili. Leo mpo wengi, mnatumia wingi wenu, mtafanya maamuzi, maamuzi ambayo yanabomoa badala ya kujenga. Ni kweli Bunge sio majukwaa ya kisiasa, lakini ninyi mnajivuaje wajibu wa kisiasa Waheshimiwa Wabunge? Wabunge wazoefu wanapojaribu kujenga hoja kwamba Bunge hili sio jukwaa la siasa, ni jukwaa la nini hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la Kanuni zetu Waheshimiwa Wabunge, sio tafsiri kama mlivyosema. Tatizo letu hapa leo halijawa tafsiri kama ambavyo juhudi zinafanywa kuaminisha Dunia kwamba tuna tatizo la tafsiri, hatuna tatizo la tafsiri, tuna tatizo la dhana; dhana ya ushirika tunaoutaka hapa, kuwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, unakuwa unapata *privileges* fulanifulani, pengine wengine mnaweza kufikiri kuwa *privileges* hizo ndio zinatuleta Bungeni, sio! Kuna mambo ya msingi tunayoyaamini, tunayoyapigania na tutaendelea kuyapigania ndani ya Bunge na nje ya Bunge, lakini hatuwezi kulazimishwa na wenzetu wa Chama kingine tuingie kwenye ushirika ambao hatujauridhia; mtakuwa mnatulazimisha kuingia kwenye jambo ambalo hatuliamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi ni wawakilishi wa wananchi zaidi ya milioni 40. Watu wamepiga kura, ile ndio *deciding factor*, ile ndio *factor* iliyo-*determine* ni nani aongoze Serikali na ndio sababu mpo upande wa pili, mna Waziri Mkuu, mna Mawaziri na mnaye

Rais na ni wananchi hao hao walioamua kwamba Chama cha pili cha kukipa ridhaa ndani ya Bunge ni CHADEMA na ni wananchi hao hao mnaosema kwamba wanataka ushirika, waliamua kwamba Vyama vingine vipate mmoja vingine wawili na vingine vikakosa, ndio demokrasia. Sasa mnapuuza kauli ya wananchi, mnapuuza utashi wa wananchi kwa kutumia namba ya Wabunge 360 au 350 ambayo tunayo ndani ya Bunge... (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema nia njema ambayo mnaidai hapa, mwenye akili Duniani ataona kama ni nia njema, ambaye atatuona labda pengine tumekosea vilevile watasema lakini *logic ya forced marriage* ipo wapi? Ninyi wote hapa mna ndoa au labda wengine hamna ndoa au mna mahusiano; hebu jaribu kujiweka katika mazingira ya kulazimishwa kwenye uhusiano! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuna ugomvi na muafaka wa Zanzibar, hatuna ugomvi wa kimsingi na wenzetu wa Chama cha Wananchi – *CUF* lakini tuna tofauti ya kimtazamo na tofauti ya kimsimamo kutokana na mambo tunayoyaamini na kuyapigania. *Approach* tunayoitumia sisi katika mambo yetu pengine ni tofauti na wenzetu; hizi tofauti naweza nikasema zinazungumzika lakini sio kwa utamaduni mliouonesha hapa leo. Utamaduni wa kutumia wingi vibaya, tukafikiri tunatumia wingi kwa busara, kumbe tunatumia wingi kupotosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nikushukuru sana lakini niweke msimamo mmoja na kwa sababu naamini pengine naweza nikajikuta nina fursa ya kuwa mchangiaji wa mwisho, ni vema Waheshimiwa Wabunge, wakaelewa sio vizuri kutishana na Kanuni. Tuheshimu Kanuni, lakini Kanuni zinapokuwa zinauwa msingi wa msingi wa haki, hiyo Kanuni ni batili. Kama Sheria, Kanuni, zinauwa msingi wa asili ambao ni haki, sisi hatuwezi ku-*support* kwenye hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikisema kwamba mimi nitaiongoza Kambi kwa ulazimisho mliotufanyia, nitawadanganya, sitakubali hilo na huo ndio msimamo wa Chama changu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo na kwa sababu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, ya kwanza au ya pili?

**SPIKA:** Ya kwanza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, huo ndio msimamo unaowakilisha dhamira ya Chama chetu na tunaamini hatujatendewa haki kwenye hili, tutakuwa wanafiki sana kama tutashiriki kwenda kwenye hatua ya mwisho ya kubariki utaratibu huu wa kutunyima haki na zaidi wa kuwanyima haki Watanzania zaidi ya milioni 2.8 waliotupigia kura kwamba pengine walikuwa ni wapuuzi hawakujua wanachagua nini. Tunawakilisha maslahi yao, kwa hiyo, maadam Bunge lako limeona ni

busara, busara sana kwa mtazamo wenu wa kuileta hoja hii ikiambatana na kauli kalikali, vijembe vingi tu... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko sana mimi na Wabunge wangu, hatutashiriki hatua ya kumalizia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, naomba kutoa hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hapa Wabunge wa Chama cha CHADEMA walitoka nje ya Ukumbi wa Bunge huko Waheshimiwa Wabunge waliobaki wakizomea)*

**MBUNGE FULANI:** Tumeshawazoea!

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 66(a) kinachosema kwamba Mbunge aliyeko Bungeni wakati wa majadala atatakiwa kuingia au kutoka kwenye ukumbi wa Bunge kwa staha na atainamisha kichwa kuelekea kwa Spika au kufanya mkunjo wa magoti kwa heshima kila mara Mbunge huyo atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake.

Mheshimiwa Spika, naona hii tabia ya kudharau Kiti inazoeleka hasa kwa wenzetu wa upande wa CHADEMA, wamenyanyuka, wameondoka, sijaona kati yao Mbunge yeyote aliyeinamisha kichwa au kupiga magoti akionyesha kwamba anatoka nje ya ukumbi, naomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Aliyekuwa Kiongozi wao, sasa sijui nimwite Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, yeye aliinama, kwa hiyo, aliinama kwa niaba ya wote.

Sasa nimwite mtoa hoja.

### **TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Taarifa kuhusu nini?

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Kuhusu msemaji aliyezungumza kabla ya Mheshimiwa Manyanya.

**SPIKA:** Yeye hayupo, sasa utampa nani taarifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwahakikishia Watanzania kwamba kilichoko mbele ya Bunge hili ni jambo jema, lenye nia ya kujenga



na wala Mbingu haitadondoka kwa ajili ya hilo, wawe na matumaini na imani na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi niliwasilisha Azimio la kuliomba Bunge lako kufanya mabadiliko katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 chini ya Kanuni ya 152(1)(3), nilifanya hivyo kwa niaba ya Kamati ya Kanuni za Bunge. Hoja niliyoitoa na ikaungwa mkono na Wabunge wengi, ilikuwa na dhumuni moja tu la kuondoa utata wa tafsiri ya neno Kambi Rasmi ya Upinzani kama inavyotajwa ndani ya Kanuni hizi, kama inavyotumika kila mahali utakapokuta Kambi ya Rasmi ya Upinzani kumaanisha kwamba kila utakapoliona neno hilo Kambi Rasmi ya Upinzani humu ndani ya Kanuni basi tafsiri yake ni kuwa Kambi iliyoundwa na Vyama vya Upinzani vinavyowakilishwa Bungeni kwa mujibu wa fasili ya 2 ya Kanuni ya 14 ya Kanuni hizi. Fasili ya 2 ya Kanuni ya 14 ya Kanuni hii inasomeka ifuatavyo:-

*“Wabunge wote wa Upinzani wanaweza kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani iwapo idadi yao itakuwa si chini ya asilimia kumi na mbili na nusu ya Wabunge wote”.*

Mheshimiwa Spika, Kanuni hii ipo na ilikuwepo, haitengenezwi leo, nairudia tena, Wabunge wote wa Upinzani wanaweza kuunda Kambi Rasmi ambayo inatambuliwa na Bunge kama Taasisi iwapo idadi yao itakuwa si chini ya asilimia 12 na nusu ya Wabunge wote. Kwa hiyo, wanaweza wakaamua wasiunde maana ukiambiwa unaweza, unaweza usiunde, kwa kutoka na kugoma, mnaweza na mambo yakaendelea maana Kanuni imetoa *option*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba wamejitokeza wachangiaji kumi, katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Khalifa Khalifa, Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Pindi Chana ambaye amechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Na Mheshimiwa Mbowe je?

**NAIBU SPIKA:** Na Mheshimiwa Mbowe wa kumi na moja.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema, hoja yangu haikusudii kufuta au kubadili kifungu chochote cha Kanuni za Bunge bali kuweka tafsiri ya maneno Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge ni kitu gani. Nashangaa baadhi ya wachangiaji na wenzetu waliofanya kitendo kingine cha ajabu tena hapa ndani, wanasema kitu hiki lengo lake ni kuua Upinzani Bungeni, jambo hili si kweli hata kidogo. Eti sababu wanayotoa ni kwamba badiliko hili litasababisha Chama chenye Wabunge wachache kuwa na nafasi ya kuongoza Kamati ya kusimamia Matumizi ya Fedha, yaani ile Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Mashirika ya Umma na Kamati ya Mahesabu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mfano umetolewa hapa, wakati wa Bunge lililopita, Bunge la Tisa, aliyekuwa Spika wetu hapa, Mheshimiwa Sitta, aliteua Kamati ndogo ya Wabunge saba kupitia na kufunua Kanuni zilizokuwepo mwaka 2006 kurudi nyuma na mimi nikapewa kazi ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo ndogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Kamati hiyo, baadhi ya Wajumbe ambao bado wamo humu ndani, ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, lakini nakumbuka wakati huo tulikuwa na kina Mheshimiwa Dr. Slaa na wengine, ndio tuliokuja na huu utaratibu wa kupatia fursa Upinzani kuweza kusimamia Kamati za Fedha za Bunge, kabla ya hapo ilikuwa ni Chama Tawala ndiyo wanasimamia. Tukapendekeza utaratibu huu kwamba Kambi ya Upinzani ndiyo isimamie kwa maneno mengine viongozi wake wa Kamati hizi wasitoke miongoni mwa Wabunge wa Chama kinachounda Serikali na Kanuni za wenzetu wengi wanatamka hivyo kwamba viongozi wa Kamati hii watatokana na Wabunge wa Chama kisichounda Serikali, ukishasema hivyo, unaondoa hili neno Kambi ya Upinzani. Wale viongozi wa Kambi hiyo wa Bunge la Tisa ambalo liliongozwa na Mheshimiwa Hamad Rashid, kwenye Kambi hiyo hapakuwa na choyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, japo Chama cha *CUF* ndicho kilichokuwa na Wabunge wengi kuliko Wabunge wa vyama vingine vyote kwenye Bunge lililopita, bado kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu, Mwenyekiti wa *PAC* alichaguliwa kuwa Mheshimiwa John Momose Cheyo, *CUF* hawakusema kwamba wale ni wachache, kwa hiyo, haiwezekani. (*Makofi*)

Kamati ya Serikali za Mitaa, alichaguliwa Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kuwa Mwenyekiti, japo Chama chao cha CHADEMA wakati huo hakikuwa na nusu ya Wabunge wa *CUF*, Mheshimiwa Kabwe Zitto vilevile akawa Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma na kazi ilifanyika na Wabunge mtakubaliana na nami kwamba katika Kamati hatubaguani hata siku moja. (*Makofi*)

Bunge hili katika Kamati limefanya kazi yake kwa ushirikiano mkubwa sana. Zile Kamati ambazo zimeongozwa na Wabunge wa CCM, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, wale wote mliokuwa wajumbe wangu mkitoka kwenye Kambi ya Upinzani mlibaguliwa lini? Mlibaguliwa kwa jambo gani? Tulifanya kazi wote kwa pamoja. Kutoka CHADEMA, alikuwepo Mzee Ndesamburo, Mjumbe wa Kamati yangu, kutoka *CUF* alikuwepo Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Riziki tulikuwa wote, wengi tu na kazi ilifanyika vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge walipochangia walisema kwamba asubuhi tulikuwa na wageni Wabunge kutoka Uingereza, wakasema kwamba hawa wageni wanatushangaa sana kwa kuwa tu hawajui Kiswahili. Wageni wetu kutoka Bunge la Uingereza walinalika *Dodoma Hotel* kwenye chakula cha mchana na mmoja wa Wabunge wale ambaye bahati nzuri anatoka kwenye Chama ambacho kina ushirikiano mzuri na CHADEMA, alionyeshwa na kushangazwa na kukerwa kweli na kilichoendelea. (*Makofi*)

Akaniuliza swali na ni *quote* alivyoniambia, *is it normal that the opposition in Tanzania commits political suicide in public like that?* Mnaweza mkaelewa jinsi nilivyokuwa mahali pagumu kulijibu swali hilo na alisema kwamba hata kule Uingereza *Minority Parties* wana namna ya kuwa pamoja katika Bunge ili kusukuma *agenda* yao dhidi ya Serikali.

**WABUNGE FULANI:** Tafisiri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, chombo hiki cha Bunge ndicho chombo cha uwakilishi.

**SPIKA:** Wanasema utafsiri hayo maneno.

**NAIBU SPIKA:** Tafisiri yake kwa Kiswahili, swali alilioniuliza ni kwamba, hivi ni kawaida kwa Kambi ya Upinzani Tanzania, alisema *for the opposition generally*, je, ni kawaida hapa katika nchi yenu kwa Upinzani kujimaliza wenyewe kwa kujitoa mhanga hadharani namna hiyo? Yeye alitafsiri kama ni kujitoa mhanga tu hakuona msingi wa hoja iliyokuwepo.

**WABUNGE FULANI:** Kujinyonga.

**NAIBU SPIKA:** Kujinyonga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ndiyo chombo kikuu cha uwakilishi cha Watanzania na kwa hiyo ni jukumu la Kanuni zetu kutoa fursa hiyo ya msingi sana kwa uhai wa demokrasia ya nchi yetu. Tafisiri niliyoipendekeza, kama nilivyosema haibadili chochote ila imetoa tafisiri sahihi ya neno Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, pendekezo hili la tafisiri linaimarisha Bunge. Mzee Cheyo alipochangia alisema kwamba CHADEMA punguzeni jazba na mimi kama mtoa hoja nirudie, ndugu zangu, najua mnaniangalia kwenye luninga, punguzeni jazba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kikao chetu cha kwanza cha Bunge hili kilichofanyika kwa mujibu wa Katiba yetu, kiliitishwa na Mheshimiwa Rais, ndivyo Katiba inavyosema, hivi vinavyofuata Mheshimiwa Spika katuita hapa, ila kile cha kwanza Mheshimiwa Rais. Wabunge tukaja pamoja na wenzetu wa CHADEMA, Mheshimiwa Rais mwenyewe anafika wanatoka nje, sasa kama kweli humtambui aliyekuita kwenye kikao ulikuja kufanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata chaguzi zilizofuata, wakati ule Mheshimiwa Waziri Mkuu tumthibitishie nongwa, hata Naibu Spika naye nongwa, mimi nasema maneno ya Mzee ya Cheyo tu kasema jamani punguzeni jazba hata yeye Mzee Cheyo aligombea Urais, kasema hapa, alikosa na ameendelea kuvaa tai yake vizuri tu, mambo haya yana kupata na kukosa. Kutuhumiana na kusingiziana kama ilivyofanyika hapa si jambo la kweli. Nawaomba Watanzania wasipokee hata kidogo tuhuma hizi ambazo hazina msingi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati za Bunge zinafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na katika Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola Duniani, Spika hukaa katikati kama Spika wetu alivyokaa, kulia kwa Spika wanakaa Wabunge wa Chama kilichounda Serikali, kwa Bunge letu sisi wanakaa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, wakiongozwa na Kiongozi wao ambaye ni Waziri Mkuu na anakuwa na kiti chake mbele pale kama Kiongozi wa Kambi ya Chama Tawala kilichounda Serikali. Mabunge yote kushoto kwa Spika wanakaa Wabunge wa Kambi ya Upinzani, Kambi yote ya Upinzani wanakaa kushoto kwa Spika na wanaongozwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, yule kiongozi wa ile Kambi ya pili maana kambi ni mbili ya Chama Tawala na ya Upinzani na Kambi zote mbili zina viongozi wake na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu akisema lazima Mheshimiwa Spika atamwona na kumpa nafasi kutegemeana na hali ilivyo. Ndiyo maana Kiongozi wa Upinzani Bungeni akisimama, kwa kadri iwezekanavyo Mheshimiwa Spika atampa nafasi ya kuzungumza kwa sababu yule anawakilisha mawazo ya Kambi nzima, anapata heshima hiyo. Sasa wenzetu wengine sio viongozi wa Kambi kumbe ni viongozi wa Chama fulani tu peke yake tufahamu leo na kwa mujibu wa Kanuni hizi watajifuta wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, navyosema haya sibahatishi kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa Umoja wa Mabunge ya Jumuiya za Madola Duniani, *CPA International*, mimi ni Mjumbe *Executive Committee*, hiyo ndiyo *practice* kwamba Kiongozi wa Upinzani ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni kama alivyo Kiongozi wa Serikali Bungeni Mheshimiwa Waziri Mkuu pakiwa na Wabunge ndani ya Kambi ya Chama Tawala ambao hawamheshimu, hiyo sio sababu ya yeye kulalamika Bungeni, hilo ni la kwake yeye na Kambi yake. Pakiwa na Wabunge katika Kambi ya Upinzani ambao wanasumbua kidogo, hilo ni jukumu la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Wabunge wake kujua namna ya kuweka mambo yao sawasawa. Kanuni ya 16(4) inasema hivi:-

*“Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni vinaweza kutunga Kanuni za vyama kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Vyama hivyo Bungeni”.*

Mheshimiwa Spika, Kambi hiyo inaweza kutunga Kanuni zao za namna bora ya uendeshaji wa mambo yao ili kuweka nidhamu humu ndani. Katika Bunge la Tisa palitokea sintofahamu, likaletwa lalamiko, Spika, Mheshimiwa Sitta akakubaliana na malalamiko yale, Mheshimiwa Cheyo akawa *disciplined* kwa maamuzi yaliyofanywa na Kambi ya Upinzani, japo yeye alikuwa anatoka Chama ambacho ni kimojawapo katika ile *coalition*.

Mheshimiwa Spika, tena katika Mabunge mengi ya *Commonwealth* yanawapa Upinzani Kamati moja tu ya *PAC* na sababu yake ni kwamba ndiyo inayosimamia matumizi ya Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali. Lakini Bunge letu limeenda mbali badala ya Kamati moja limetoa tatu, zote ziendee Upinzani, kwa hiyo, mtu akilalamika na kusema CCM, wanakandamiza wakati mwingine mambo hayo sio kweli sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sina haja ya kusema mengi, niseme tu kwamba hoja iliyo mbele yetu ni kuondoa utata wa tafsiri tu, hoja hii haibadili chochote kwa kufuta au kuondoa bali ni kutoa ufafanuzi wa tafsiri ya neno hilo kadri lilivyotumika ndani ya

Kanuni kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni maana yake ni Kambi ya Upinzani iliyoundwa na Vyama vya Upinzani vinavyowakilishwa Bungeni kwa mujibu wa masharti ya fasili ya 2 ya Kanuni ya 14 ya Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Naona hoja imeungwa mkono na kwa sababu hili ni Azimio, hutuendi kwenye Kamati ya Matumizi, tutawahoji tu wanaokubaliana na Azimio lilioletwa kwamba sasa tutafsiri maana ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Naibu Spika, jamani tunafanya siasa, *tradition* ya humu ndani toka tunaanza mfumo wa Vyama Vingi Wabunge wa Kambi Rasmi walikuwepo, hiyo ndiyo ilikuwa *practice*. Nimesema mwaka 1995, ndipo tulipoingia kwa mara ya kwanza kuwa na Bunge la Vyama Vingi. Mwaka ule Wapinzani katika Bunge letu walikuwa zaidi ya 46 na Kanuni zetu ambazo zilitungwa hata kabla hatujaingia kwenye mfumo huu, zilikuwa zinasema *threshold* ya Upinzani ndani ya Bunge ikifika asilimia 30 ndiyo inaweza kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwa hiyo, mwaka 1995 *threshold* ya asilimia 30 ya Wapinzani waliokuwepo kwa Vyama vyote walitimiza asilimia hiyo wakaunda Upinzani wao, walikuwa CHADEMA, NCCR MAGEUZI, walikuwa pamoja sio kwamba kilikuwa Chama kimoja. Ilipofika mwaka 2000, nadhani *performance* ya Vyama vya Upinzani ilikuwa sio nzuri wananchi wakawaacha wakawa 26 tu na hao 26 hawakuwa Chama kimoja walikuwa vyama vyote, sasa ikawa tatizo kwa Mheshimiwa Spika anafanyaje, maana wale 26 sio asilimia 30 tuliyosema mwanzo.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 14(2) ilipaswa wakati ule kama Spika angekuwa hakutumia busara yake kungekuwa na Wapinzani lakini hakuna Kambi, ndiyo neno Kambi Rasmi lilipoanzia pale kwamba una Wapinzani wamefikia *threshold* si chini ya asilimia 12.5 wanaweza ku-*form* Kambi Rasmi na hii basi ni kwa busara ya Spika huyu aliyekuwepo. Aliona haiwezekani kwamba tumeanza tu zoezi la kuwa na Upinzani katika siasa zetu, halafu nawaambia kipindi kinachofuata kwamba wako Wapinzani lakini hakuna Kambi Rasmi, maana wangukuwa *treated* kama mtu mwingine yeyote, hakuna ku-*recognize* sijui nani aseme kabla, hakuna kwa sababu hakuna Kambi. Kwa hiyo, busara ya *threshold* kutoka 30 kwenda 12.5 ilitumika ili wale 26 waweze ku-*form* Kambi Rasmi ya Upinzani na ilikuwa ni Vyama vyote hao 26.

Kwa hiyo, tunachokifanya sasa sio tofauti, sasa hivi tuna Wabunge wa Upinzani 90, wako zaidi ya asilimia 12.5, kwa hiyo wote wana haki ya ku-*form* Kambi ya Upinzani. Kanuni inakwenda zaidi inasema baada ya hii Kambi ya Upinzani kutambuliwa kwa sababu wako zaidi asilimia 12.5, sasa hawa watu wote hawa tisini wanapataje uongozi, ndiyo Kanuni ya 14(4) inasema Chama chenye Wabunge zaidi ya asilimia 12 kitachagua ama kuteua Kiongozi wa Kambi hiyo kubwa ya Upinzani yote maana ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani sio CHADEMA, ni wote. Zaidi ya hapo Kanuni ya 15 inasema huyu kiongozi atakayekuwa amechaguliwa kwenye Chama chenye

Wabunge wengi kuliko wenzake atateua Baraza lake la Mawaziri Vivuli na anaweza akateua kwenye Vyama vingine ama akawateua kwenye Chama chake tu. Sasa kwa sababu atakuwa na Vyama vingi humu ndani na wengine kama hivyo wanavyowataja, wengine hatuwezi kwenda. Kanuni tena ya 16(4) inasema hizo Kambi zitatengeneza Kanuni za kuendesha shughuli zao. Sasa jamani *principal* ya kuwemo na Vyama Vingi Bungeni, hawa wenyewe Chama Tawala wanataka kubakia madarakani, hawa wanaopinga wanataka kuondoa hawa walioko madarakani waingie wenyewe, sasa ni lazima muonyeshe kwa wananchi kwamba mnaweza kustahili kuwa Serikali mbadala baadaye. (*Makofi*)

Lakini kwa tabia hii, kwa mfano ile siku walipoondoka wakati Mheshimiwa Rais anakuja kutoa hotuba yake hapa, kwa Kanuni zetu jamani tunaondoka hasa wakati wa bajeti kwamba hamkubaliani na bajeti hiyo na ni njia ya maana ila bajeti ikipita Chama Tawala kinatekeleza Ilani yake. Kwa hiyo, mnapinga kama isingepita kusudi washindwe kutekeleza Ilani yao sababu zinakuwepo, lakini hii kwa kweli, hata mimi nimekuwa na hao wageni anaosema Mheshimiwa Naibu Spika wamesema Mheshimiwa si unajua hata sisi Chama Tawala kimeungana na Vyama vingine, wameniambia sasa hivi. Sasa kwa maana hii ile siku Mheshimiwa Rais ametoa hotuba yake kama Vyama hivi vingekuwa makini, vingeisikiliza ile hotuba, tunapoanza sasa hivi kuijadili wangeichambua ile hotuba kwamba sisi tungekaa, tungefanya hivi na hivi na sio aliyosema huyu mtawala. Kwa hiyo, wangukuwa wamepata hoja ya kuweza kuiponda ile hotuba ya yule mwenye Chama Tawala. Sasa una *walkout*, uki-*walkout* umesikia hicho alichokuwa akikisema, sasa utakuwa unazungumzia nini? Hilo ndilo lilikuwa kosa lingine la kwanza, ile ilikuwa kabisa sio tabia ya Kibunge hasa ya Chama kinachotaka kuchukua madaraka. (*Makofi*)

Maana uwezo wa Chama kinachotaka kuchukua madaraka ni kuonyesha kile kilichoko madarakani hakina maana wala si lolote, wao wana hoja nyingine, lakini ukitoka utasema nini sasa? Utabaki tu kuzomea, kuhusu utaratibu, kuhusu *information*, hiyo haikuweki madarakani bali ni hoja zenye uzito. (*Makofi*)

Leo hii, kama kila tutakaposhindana kwenye kupitisha Miswada tutakuwa tuna *walkout* basi litakuwa Bunge la ajabu sana, maana hapa hapa tutakuwa tunapiga kura ya ndiyo au hapana, sasa wewe ukiona kura yako ya ndiyo ndio u-*walkout*, jamani mtakuwa mnawaeleza nini Watanzania? Siasa yote ni kuvumiliana halafu kuwa wa kweli kwenye hoja, katika hoja hii hakuna ukweli wowote wenzetu wa CHADEMA wanasimulia, hakuna ukweli, *practice* ya kuungana ipo kwenye Kanuni. Mheshimiwa Spika aliyetangulia mwaka jana alitumia tu busara ya kuwaambia jamani mkae pamoja, haipendezi lakini ukweli ni kwamba Kanuni ya 14(2) ndicho kilitakiwa kitumike.

Sasa kuondoa utata wa tafsiri kwamba ni sisi tuliokuwa wachache ndiyo tunakuwa Chama Pinzani Rasmi, ndiyo tumesema sisi tuongeze tafsiri ya Chama Pinzani Rasmi, tofauti yake ni kwamba wakizidisha *threshold* ile ya 12.5 wanaweza ku-*form* Kambi Rasmi. Lakini wangukuwa chini ya hiyo asilimia, wangukuwepo Wapinzani humu lakini hawana Kambi Rasmi ndiyo tofauti yake. Kwa hiyo, sasa Kiongozi anatoka kwenye Chama katika hao Rasmi mwenye Wabunge wengi zaidi, ndiyo CHADEMA imetoa Mbunge Kiongozi na huyu kiongozi ana mamlaka ya kuunda Baraza lake Kivuli kwa

Chama chake tu, ingawa busara za kidemokrasia hazipendezi lakini Kanuni zetu zinamruhusu na hata kama alivyosema Naibu hapa akienda nje anatambulika kwamba ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Tanzania sio kiongozi wa Kambi ya CHADEMA. *(Makofi)*

Kwa hiyo ndugu zangu, hapa tunabishana na watu wengine wana ufundi wa kuwaeleza wananchi mambo ambayo si ya kweli yakaaminika kama ni ya kweli. Mimi nataka niwaambie Watanzania, hapa wenzetu wamepitiwa namna ya kuiona Kanuni hii na sio siri tabu waliyonayo ni Kamati tatu, wao walishatafsiri kwamba wangeweza kushika Kamati ya PAC, ya Hesabu za Serikali, wangeshika Kamati ya Mashirika ya Umma, wangeshika na Kamati ya Serikali za Mitaa, ndiyo ugomvi uliopo hapa. Sasa zile Kamati zinaundwa kwa nafasi ya Spika halafu Wajumbe wa Kamati ndiyo watakaochagua Wenyeviti wao. *(Makofi)*

Sasa nyie mnasema Kambi ya Upinzani nayo iweke na Mwenyekiti wa Kamati, atakuwa anawaongoza akina nani, maana Kamati ile inatakiwa ichague Mwenyekiti wao wanayekubaliana naye lakini sisi tukasema hapana kwenye Kamati hizi tatu mtaweka Upinzani hata kama nyie wa Chama Tawala mko wengi lakini kiongozi atakuwa wa Chama cha Upinzani, hilo ndilo tunalobishania hapa.

Waheshimiwa Wabunge na ndugu wananchi, tunataka kusema kwamba kitendo kilichotokea cha wenzetu kutoka nje, wanahiari kutoka lakini tunauliza kila tutakaposhindana hapa watakuwa wanatoka nje? Ndiyo kazi tuliyotumwa na wananchi kufanya? Sasa hapo ndiyo itakuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Baada ya kufafanua zaidi yale aliyosema Mheshimiwa Naibu Spika ambapo amewasilisha vizuri, Mheshimiwa Naibu Spika yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya CPA International anayewakilisha Kanda ya Afrika Mashariki, ni Kamati tendaji, sio Mjumbe tu hivi, kwa hiyo, haya mambo yote anayajua. Hii *practice* wanayosema ya *Commonwealth*, kwanza kabisa, tunaanza na *practice* yetu sisi. Toka tumeanza mwaka 1995, Kambi Rasmi ya Upinzani ni Wabunge wote ila kiongozi anatokana na ile Kambi ambayo ina Wabunge wengi zaidi na hivyo ndivyo ilivyofanyika.

Kwa hiyo, ndugu zangu baada ya kusema hayo napenda tuelewane kwamba kilichotokea hakuna mabadiliko ya Kanuni, tulifanya kutafsiri utata ambao ulikuwa unaendelea na ukatufanya sisi tusieleweke tunazungumza kitu gani. Kwa hiyo, naomba niwahoji kwa hili. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge Toleo la 2007 liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kuanzia sasa Kambi Rasmi ya Upinzani inaelezeka kama Kanuni inavyostahili. Kabla hatujaingia kwenye ajenda inayofuata ambayo ni ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kulikuwa na mapendekezo mnakumbuka pale tulikuwa tumesema iwapo tutaendelea na mtindo wetu wa dakika 15 kujadili hoja hizi na leo ndiyo tumechukua muda mwingi zaidi basi watajadili wachache tu. Kwa hiyo, tulikuwa tunapendekeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, sera Uratibu na Bunge atengue Kanuni ya 61 ili tuweze kujadili hotuba ile ya Mheshimiwa Rais kwa dakika 10 badala ya dakika 15.

## **HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa maelezo ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 23(1)(i) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 Bunge lina wajibu wa kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais, na kwa kuwa kutokana na ratiba iliyopangwa na kwa kuzingatia idadi ya Wabunge tulionao na muda wa kuchangia kwa kila Mbunge, Wabunge wengi hawatapata nafasi ya kuchangia hotuba hiyo. Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 62(1)(a) inayomtaka kila Mbunge anayejadili hoja kusema kwa muda usiozidi dakika 15 itenguliwe ili kila anayepata nafasi atumie dakika 10 badala ya dakika 15 kwa lengo la kupata idadi kubwa ya Wabunge watakoachangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Bunge liliafiki Kutengua Kanuni iliyotajwa*)

**SPIKA:** Kwa hiyo, kwa maana tu ya Hotuba ya Rais tutakuwa tunatumia dakika 10, lakini baadaye tutaendelea na utaratibu wetu ule ule.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa nafasi uliyonipa napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na kuiwasilisha kwa muhtasari tena Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati akifungua rasmi Bunge jipya



la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama Kanuni niliyoisoma inavyosema sisi Waheshimiwa Wabunge tunayo fursa ya kuijadili hotuba hii kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ilitolewa tarehe 18 Novemba, 2010 hapa Bungeni. Katika hotuba hii Mheshimiwa Rais alitumia nafasi yake kuwashukuru wananchi kwa kumchagua yeye kuwa Rais, lakini pia kwa kuchagua chama chake kuongoza kwa kupindi cha pili. Alitushukuru sana sisi Wabunge kwa kumthibitisha na kukubali uteuzi wa Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda, kuwa Waziri Mkuu. Alipata nafasi pia katika hotuba yake kuelezea majukumu ya msingi na vipaumbele kumi na tatu (13) kama ambavyo vinasomeka katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele ambavyo alisisitiza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ni kudumisha umoja wa nchi yetu. Jambo hili alilizungumza kwa nguvu sana na Wabunge wengi najua katika eneo hili watachangia kwa nguvu zao zote.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili alizungumzia suala la Muungano na kuudumisha Muungano, alizungumzia umoja wa watu wetu wa Tanzania, usalama wa raia na suala zima la kukuza uchumi. Pia alizungumzia jukumu kubwa la kuendeleza sekta ya uzalishaji mali, kilimo na mifugo, uvuvi, kuleta mapinduzi ya viwanda, madini, utalii, shughuli na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Rais pia alizungumzia masuala ya kukuza ajira na nia yake ya kuifanya Tanzania kuwa lango kuu la biashara, akazungumzia masuala ya bandari na reli ambayo Waheshimiwa Wabunge watapata nafasi ya kuchangia. Alizungumzia masuala ya miundombinu hasa barabara na uboreshaji wa huduma za kijamii na kiuchumi hususan elimu, afya na pia alijikita katika maji na mazingira.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo, alizungumzia matatizo makubwa tuliyonayo ya upungufu wa nishati lakini pia na mikakati ya Serikali ya kukabiliana na tatizo hilo. Vilevile alizungumzia masuala mazima ya kuimarisha demokrasia katika nchi na utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa, utawala wa sheria haya ni mambo muhimu ambayo amezungumza katika hotuba yake.

Katika hotuba hii Mheshimiwa Rais hakuacha nyuma masuala ya wanawake katika nafasi ya maamuzi na mpango wake wa kufikisha uwiano wa kijinsia wa 50% - 50%. Alizungumzia Tume ya Mipango, Michezo na Utamaduni na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na pia Ushirikiano wa Kanda.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa Mheshimiwa Rais alitoa kwa muhutsari mambo ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kwa kipindi cha miaka mitano ambayo ndiyo yalifanya wananchi waipere ridhaa ya kutawala katika miaka mitano hii inayoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini Waheshimiwa Wabunge wote wanazo hizi hotuba na bila shaka kwa sababu umetenga siku tano kwa wale ambao watakuwa wamesahau labda

mahali pengine, wanaweza kupata kwenye *Hansard* zetu maana ilikuwa imenukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa muhutsari huu nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa. Asante sana, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. DKT. BINLITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais ya kufungua Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwanza, kumpongeza sana Rais kwa kutoa hotuba iliyotukuka na iliyoelezea tulikotoka, tulipo na tunakokwenda, pia iliyoonesha mikakati ya mambo ambayo tunatakiwa kuyatekeleza ndani ya miaka mitano ijayo (2010-2015). Kwa maana hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo inaweka misingi ya mjadala huu wa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kimsingi ninachotaka kufanya mengi ameyaongea yanaeleweka ni suala la kujaribu kufafanua baadhi ya mambo na kuongezea tu baadhi ya mifano kulingana na hali halisi ya maeneo tunayotoka.

Mheshimiwa Spika, jambo langu la kwanza ambalo naomba kuchangia ni vile vipaumbele 13 alivyovionesha na kuvieleza.

Naenda kwenye kipaumbele cha nne ambacho Mheshimiwa Rais amesisitiza umuhimu wa kuimarisha na kushirikisha sekta binafsi katika kukuza uchumi wetu, lakini vilevile nataka niainishe kipaumbele namba tisa ambacho Mheshimiwa Rais amesisitiza kuendelea kuboresha huduma za maji, elimu, afya, umeme, barabara, bandari na vitu vingine. Nataka kuunganisha vipaumbele hivi viwili ili kujenga hoja na kuona umuhimu wa kutatua matatizo tuliyonayo kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta ya maji, sekta ya elimu, sekta ya afya kwa kutumia sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, yapo mafanikio makubwa sana ambayo sekta hii imefanya, kwa hiyo, nilikuwa nataka kujenga hoja kwamba kwa kutumia mifano ile Serikali ione umuhimu sasa wa kutumia sekta binafsi katika kutatua tatizo la umeme lililopo hapa nchini sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunavyo vitu viwili pale; tunao watu binafsi, sekta binafsi lakini vilevile Sheria ya Nishati ya Mwaka 2007 inaruhusu uwekezaji kwenye mambo ya nishati na madini. Nilikuwa naomba na napendekeza kwamba nchi hii imejaliwa kuwa na mito mingi mikubwa na midogo na wenzetu wa China wametumia sana hii mito midogo kujenga vituo vya kufua umeme ambao unaweza usizidi *Kw 100* kwa ajili ya

kusambaza vijijini. Kwa hali tuliyonayo sasa hivi ya matatizo ya umeme tuliyonayo haitakuwa rahisi kutekeleza *vision* ya 2025 ya kusambaza umeme vijijini, kwani umeme wa gridi bado hautoshi, lakini kwa kutumia mito midogo tuliyonayo kwenye mikoa mingi ambayo ina maji mengi tungeweza kutengeneza vinu vya kufua umeme huu ambao baadae utasambazwa kwenye vijiji na umeme ambao unabaki unaingizwa kwenye gridi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali peke yake haitaweza vyote hivi, namna pekee ya kufanya ni kushirikisha sekta binafsi waweze kufanya vile na tumeona mifano mingi kwa wenzetu wa *mission* wamekuwa wakijenga vinu kama hivi kwa ajili ya kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, lingine katika sehemu hii kwa kutumia umeme wa maji ambao utafuliwa kwenye mito yetu midogo itasaidia wananchi ambao wanaishi vijijini zaidi ya 80% wanatumia kuni kwa ajili ya nishati ya kupikia. Hii itasaidia sana kuzuia tatizo la uharibifu wa mazingira kwa sababu tutawaelimisha wananchi sasa jinsi ya kutumia zaidi umeme badala ya kwenda kuokota kuni na kupikia, kitu ambacho kinaharibu mazingira zaidi.

Mheshimiwa Spika, sehemu yangu ya pili ya mchango inakwenda kwenye sehemu ambayo Mheshimiwa Rais amesisitiza Mapinduzi ya Viwanda. Nilikuwa napendekeza kwamba moja ya kitu ambacho tumekifanya vizuri katika awamu ya nne kwa miaka mitano iliyopita (2005 - 2010) ni mkakati wa kujenga vyuo vya ufundi (*VETA*) katika kila Wilaya, lakini hawa vijana wakimaliza kule lazima wawe na sehemu ama za kujijaji kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali ama kwenda viwandani na hii si kitu kingine bali kuwa na viwanda vidogo vidogo yaani vya *SIDO*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amesisitiza umuhimu wa kuendelea kuboresha viwanda hivi vidogo vidogo vifike mpaka huko kwenye wilaya na viweze ku-*create* ajira kwa vijana wetu. Lakini alichosisitiza ni kuona kwamba Sheria ya viwanda vidogo vidogo inarudishwa hapa na inafanyiwa marekebisho.

Naomba Sheria hii iletwe haraka na irekebishwe ili kuharakisha viwanda vidogo vidogo kufika katika Wilaya na hivyo kuwawezesha vijana wengi kujijaji baada ya kupata mafunzo ya *VETA*.

Mheshimiwa Spika, sehemu yangu ya tatu ya mchango inahusu suala zima la elimu. Mheshimiwa Rais amesisitiza kuboresha elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vikuu na vyuo vingine. Hapa ninachooomba kama kweli tunaamini kwamba nchi zote ambazo zimeendelea zimewekeza katika sayansi na teknolojia basi ni vizuri tukamuunga mkono sana Mheshimiwa Rais katika kile kipengele ambacho ameahidi na amesema kwamba katika miaka hii tutahakikisha kwamba vyuo vya ufundi vinajengwa Wilaya zote, lakini vilevile tutahakikisha kwamba Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya katika ule mchakato wa kwenda kuwa Chuo Kikuu unafanywa haraka na kile chuo kinaanza kuwa *University of Science and Technology (MUST)*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa muda wa miaka mitano iliyopita Taasisi imeweza kuwa na uongozi mpya, imeweza kuanza kutoa Digrii za

Uhandisi na sasa tunachokiomba ni kwamba wale wenzetu wa *Tanzania Commission of Universities (TCU)* watumie mkakati walioufanya kwa Chuo Kikuu cha Dodoma kuanzishwa watembelee kile chuo ili kuharakisha mchakato kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia na ni ukweli usiofichika kwamba hawa ni watu ambao wakimaliza wanaweza kujijaji na wanaweza kusaidia nchi yetu kusonga mbele zaidi na tatizo kubwa katika vyuo hivi ni maabara au vifaa vya ufundi ambavyo tayari vimeishapitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, ukienda Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam maabara ni za zamani sana, ukienda *MIST* maabara ni za zamani sana kwa hiyo, tunaomba Serikali iwekeze kwenye Sayansi na Teknolojia badala ya kuongea tu bila kuweka kwenye vitendo.

Mheshimiwa Spika, la pili katika sehemu hii ni suala zima la ufundi katika nchi. Tulikuwa na vyuo vitatu vya ufundi (*Technical Colleges*) vya Arusha, Mbeya na Dar es Salaam. Leo hii Dar es Salaam inatoa digrii na *MIST* tunataka kiwe Chuo Kikuu kwa hiyo, tunabaki na *Technical College* moja tu. Nilikuwa nadhani ni vizuri Serikali ikauweka ule mkakati uliokuwepo miaka ya nyuma kwamba kuwe na chuo cha ufundi karibu kila Kanda kwa sababu vyuo hivi ndio vinatoa watu ambao wanaweza kujijaji wenyewe na wanaweza wakashiriki sekta zote za kimaendeleo. Hata hii Sekta ya Kilimo Kwanza wanaoweza kusaidia sana ni vijana wa hizi fani za ufundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba hii nzuri. Sisi tuko tayari na kwa niaba ya wananchi wangu wa Makete tutashirikiana nae kuona kwamba yale yote ambayo ameyasema yanatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Asanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi nilishangazwa sana kwa sababu katika Hotuba ya Rais sikuona eneo ambalo amezungumzia suala la Taifa kuwa na falsafa kwa sababu nchi yetu imekuwa inaenda au inaongozwa bila kuwa falsafa inayoeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Katiba ukisoma Ibara ya 9 tuko kwenye falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea na ninapozungumza falsafa sizungumzii maana ya Ujamaa na Kujitegemea, ila nazungumzia misingi ya nchi ikiwezekana zaidi hata ya miaka mia mbili au mia tatu mbele, ndiyo maana ya falsafa. Katika nchi yoyote ili iweze kuendelea huwa tunaanza na falsafa, baada ya falsafa tunakuja kwenye sera, baada ya sera ndiyo tunatunga sheria.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Rais tumeona kwamba hakuna falsafa, lakini ameeleza kwamba atakuza elimu katika nyanja mbalimbali. Nampongeza katika hilo na amesema kwamba atakuza elimu hasa katika ubora wake (*quality education*), lakini hatuwezi tukakuza elimu katika Taifa hili endapo yanatokea matukio na Rais huyu huyu aliyetoa hotuba hii amekaa kimya. Kwa mfano, kumekuwa na migomo inayoendelea katika Vyuo Vikuu, kumekuwa hakuna utaratibu mzuri wa kuziwezesha shule kupata walimu.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, kwa takwimu za elimu mkoa wa Kigoma ni kwamba kila shule ina walimu watatu yaani ukichukua idadi ya shule ukagawanya na walimu waliopo ni kwamba kila shule ina walimu watatu na sababu kubwa ni kwamba walimu wakipangiwa maeneo ya vijijini hawaendi kule. Sasa tunasema kwamba hii hotuba ili iweze kwenda kwenye vitendo ni lazima kuwe na mkakati maalum (sera) wa kuwafanya wale walimu waweze kuendana na mazingira yale. Leo Mwalimu aliyeko kijijini analipwa malipo sawa na mwalimu aliyeko Kawe, Dar es Salaam. Ni lini huyu mwanafunzi anayemaliza Chuo Kikuu atakubali kwenda akufundishe kule Kigoma Vijijini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia elimu kama elimu tumeona nchi yetu imekuwa na mambo mengi ya ubadhirifu. Tuwe na masomo ambayo yawe ni ya lazima katika Vyuo Vikuu, masomo haya ya falsafa tumeona viongozi wengi wa Bara la Afrika ambao walikuwa ni wazalendo, wamesoma masomo ya maadili (*ethics*). Kina Mwalimu Nyerere wamesoma masomo ya falsafa ndiyo maana hata akawa anatumikia Taifa hili bila kuiba raslimali za nchi. Kwa hiyo, uboreshaji wa elimu bila kuingiza masomo ya falsafa, masomo ya maadili itakuwa tu ni hotuba ambazo utekelezaji wake ni mgumu na elimu itaendelea tu kuwa katika dhana ya wingi lakini si elimu ya kiukombozi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala zima la barabara na umeme, nishati na madini. Hizi Wizara za Miundombinu na Nishati na Madini zimekuwa zinasema kwamba zinatenga Bajeti kwa kutoa vipaumbele. Hata Mheshimiwa Rais mwaka 2005 alihutubia na akasema kwamba atahakikisha Mkoa wa Kigoma tunapata Gridi ya Taifa, lakini mpaka sasa hivi mambo haya hayapo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ndani ya miaka hii mitano tujiulize hivyo vipaumbele vinavyokuwa vinapelekwa baadhi ya mikoa toka mwaka 1960 ni vipaumbele vya namna gani? Kuna mikoa ambayo imesahaulika kwenye kila kitu, imesahaulika kwenye umeme, barabara, maji, mitandao ya simu, leo watu walikuwa wanauliza asubuhi. Hii hotuba iangalie huko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la ajira kwa vijana. Kumekuwa na wanafunzi wengi wa Vyuo Vikuu ambao wanamaliza *Diploma* mbalimbali, lakini Serikali haiwatambui kwamba ni wangapi ambao wanakazi na wapo wapi, wamefika wapi na wanapaswa kwenda wapi. Tunaomba katika hotuba hii suala la ajira liwe katika *frame work* ambayo inaeleweka kwamba mtu ametoka hapa anakwenda wapi. Leo mtu anaajirwa kesho anakwenda kusoma, tunalalamika kwamba hatuna walimu. Kwa hiyo, mfumo mzima wa ajira kwa hii miaka mitano tunaomba uwe wenye kueleweka kwa

Watanzania, uwe ni mfumo ambao unatambua, kwa mfano sasa hivi ukiangalia kuanzia mwaka huu watu 3,000 watakuwa wanamaliza Shahada ya Sheria, lakini kuna chuo kimoja tu cha Sheria (*School of Law*) ambacho kiko sehemu moja sasa hawa watu wengine watakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais tumeisikia, tumeiona lakini kama hakutakuwa na utaratibu wa kuweka *frame work* nzuri kujua kwamba vijana wamemaliza Vyuo Vikuu wanakwenda huku tutakuwa tunatengeneza siasa ambayo haitekelezeki. (*Makofi*)

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba nikupongeze sana kwa kutupa upendeleo mkoa wa Kigoma, Mkoa uliosahaulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ametangulia Mbunge mwenzangu tunayetoka mkoa mmoja, sitazungumza mengi. Katika Hotuba ya Rais nisimame tu na kuonesha masikitiko kwamba nimeipitia lakini imekuwa ni taratibu ya kusoma maandishi mazuri, maelezo mazuri lakini utekelezaji hakuna. Naiomba Serikali ikumbuke kufuata taarifa na ahadi mbalimbali ili kuweza kujenga heshima ya viongozi wetu wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunapata ahadi nyingi ambazo hazitekelezeki, lakini nina imani kwa uongozi wako unavyoonesha kuwa mahiri, kipindi hiki cha miaka mitano naona dalili ni nzuri, mikoa iliyosahaulika tunaweza tukapata mabadiliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nilikuwa naomba nichangie kwenye kuinua uchumi nchini hususani kwa wazalishaji wadogo wadogo hasa kama akina mama tunaotegemea vikundi vya *SACCOS* na *VICOBA*. Hivi vikundi sasa hivi naiomba Serikali ipitie utaratibu upya kwa sababu asilimia kubwa ya wanaonufaika na *SACCOS* ni wale wenye mitaji, ambaye atapata mtaji wa kwenda kuwekeza ndiye atakayeweza kukopa lakini yule Mtanzania maskini wa hali ya chini kijijini ambaye hana mtaji hanufaiki na *SACCOS*. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali iangalie ni namna gani tutaweza kuwasaidia hawa Watanzania maskini waweze nao kunufaika na *SACCOS* na *VICOBA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kunipa uhai mpaka siku hii ya leo na nikasimama kwenye Bunge lako Tukufu nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Pili napenda kuwashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya ya Ilemela kunitewa tena na Chama Taifa kikaniona na kikanirejesha tena Bungeni kwa mara nyingine. Nawashukuru wajumbe hao na ninawaambia asante sana kwa uteuzi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipenda kujielekeza moja kwa moja katika hotuba ya Rais upande wa uvuvi, suala la uvuvi tumeliongelea muda mrefu. Mheshimiwa Rais ameliongelea suala la uvuvi na kuhusiana na mikopo ya wavuvi lakini mikopo hii inakuwa migumu sana kuwafikia wavuvi, imekaliwa zaidi na watu ambao si wavuvi na haiwafikii wavuvi moja kwa moja, kwa sababu mikopo hii mvuvi anapoweza kuuliza kwamba mkopo anaupata wapi maelekezo ya watendaji yanakuwa ni magumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wavuvi wengi wanahitaji kupata mikopo hii ili waweze kujiendeleza katika uvuvi na hasa pale tunaposema wasitumie nyavu haramu waweze kutumia nyavu zinazokubalika lakini ugumu wa pesa unakuwa ni mkubwa na wavuvi wengi wanakuwa hawana uwezo kwa sababu nyavu zao wanaponyang'anywa zinachomwa pasipokuwaelekeza ni nyavu zipi watumie. Kwa mfano, unaweza ukamchomea mtu nyavu hata kama ni kumi lakini mpe moja ya mfano ili aweze kwenda kuvua na kuweza kujiendeleza katika maisha yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeiomba Serikali kipindi cha pili cha awamu ya nne kiwaangalie wavuvi kwa jicho la huruma sana hasa wavuvi wa Ziwa Victoria. Wavuvi hawa wana matatizo makubwa pamoja na nyavu tulipiga kelele ambao ndio uliomuondoa Mbondo lakini wanakuja wakaguzi wa kila aina kuja kusema mitumbwi haifai ikiwa imekwishaingia majini. Tungeomba Serikali ijipange na kama mtu anahitaji kuingiza mtumbwi majini ukaguliwe uwe unafaa ndipo uweze kuingizwa ndani ya maji ili mvuvi huyu aweze kutumia rasilimali yake vizuri bila kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kidogo katika suala la elimu. Suala la elimu baadhi yetu tunalalamika na tunasema kwamba elimu imeshuka, lakini tukijiuliza sababu ya elimu kushuka kila mmoja anakuwa hana jibu la uhakika la kuweza kutoa. Wengine wanasema elimu imepanda, lakini kiukweli ni kwamba shule zimekuwa nyingi na walimu wamekuwa wachache kwa vyovyote vile ni lazima elimu yetu itabaki ikiyumba. Unakuta shule ina mwalimu mmoja hapa tumesema tumeboresha. Shule ina mwalimu mmoja wanafunzi 300. Ukimwuliza yule mwalimu, Mwalimu Mkuu ni nani, anakwambia ni mimi. Mwalimu wa Taaluma ni nani, ni mimi. Sasa unabaki unajiuliza wewe huna mwalimu mwingine wa kukusaidia inakuwaje mahali pengine kuna walimu wengi wanapangiwa kwenda katika shule zetu hizi kufundisha, lakini kwa kuwa maslahi ya walimu ni madogo ambapo anaona ni bora asiende kufundisha hata kama amesomea ualimu lakini abaki mjini aweze kupitia njia zingine zozote ambazo anaweza zikampatia kipato ili aweze kuendesha maisha yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuishii hapo, mwalimu anaweza akafanya mgomo baridi kulingana na mshahara anaupata. Badala ya kuingia darasani akafundisha, anaingia darasani kazi hii mtaifanya, zoezi ni hili, mwalimu anatoka akienda zake hana mfano alioutoa.

Hii yote ni umuhimu kwamba tumejenga shule nyingi wanafunzi wasome wengi na baada ya hapo maslahi ya walimu Serikali iwajali walimu kuangalia maslahi yao. Tuliwaahidi nyumba walimu, nyumba hazipo, tunawaambia wananchi mfanye mpango muwajengee walimu nyumba, mwananchi huyu anayemwambia achange mchango wa

kuweza kumjengea mwalimu nyumba ni jana umemkamatia nyavu zake ukazichoma moto hata ukifanya vipi mwalimu huyu hawezi kupata pa kukaa, elimu yetu itaendelea kudorora kama tunavyoiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi kuna shule za kulipia za watu binafsi na shule za Serikali. Tunasahau wazi kwamba shule za Serikali zina walimu pungufu, hazina vifaa, wala maabara, shule za watu binafsi zina maabara, maktaba na walimu wa kutosha. Lakini mtihani unapokuja wa kumaliza Kidato cha Nne au cha Sita mtihani unaoletwa ni mmoja. Ndipo pale tunaposema shule zetu za Kata zinafanya vibaya na shule za watu binafsi zinafanywa vizuri. Ni kwamba mtihani unaotungwa ni mmoja, wenzao masomo yote wameyapitia kwa wakati, lakini wao hawa wanaotoka kwenye shule zetu za Serikali wanakuwa wamefanya mtihani ni kama wamefanya kiini macho.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali tuweke kipaumbele kama tulivyosema ni elimu kweli kiwe kipaumbele, ni elimu na ningefurahi zaidi kama sisi sote Watanzania tugesema kwa pamoja elimu yetu itakuwa hivi kwa sababu kesho anaweza akaja Rais mwingine naye akaibadilisha tena elimu, kwa hiyo wanafunzi wanabaki kuyumba bila ya kujua kwamba washikilie wapi.

Katika hali hii Watanzania tujipange na tuseme elimu ndio kipaumbele na elimu yetu itakuwa hivi. Nafikiri itakuwa ni bora na ni muhimu zaidi tunaweza tukaiondoa nchi ilipo na kuipeleka mahali ambapo panastahiki kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa muda huu. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki kwa kuniadini tena kwa mara ya pili, naomba niwahakikishie kwamba nitakuwa mtumishi wao muadilifu ili waniadini kipindi cha tatu na cha nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hotuba yake aliyoitoa alipotuita Mkutano wa Kwanza, ilikuwa ni hotuba nzuri ambayo imekidhi haja. *(Makofi)*

Mimi ningejikita kwenye kipaumbele cha kwanza ambacho kinasema kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa yenye umoja, amani na usalama na Muungano wetu unaendelea kudumu na kuimarika. Kama kuna jambo muhimu katika nchi yoyote duniani ni amani. Tumetoka kwenye kipindi cha Uchaguzi Mkuu, kipindi ambacho kilikuwa ni cha mapambano, kila chama kilikuwa kinatafuta kukamata dola, aliyeshinda ameshinda na sasa uchaguzi umekwisha. Watanzania wanachotegemea kukiona sasa hivi ni maendeleo endelevu na amani ya kudumu. *(Makofi)*



Mheshimiwa Rais alipoweka kipaumbele hiki kwamba kiwe kipaumbele cha kwanza alikuwa anajua mambo mengine yote yatawezekana kama nchi yetu itaendelea kuwa na amani, amani ya nchi ndiyo inayozaa maendeleo endelevu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ukweli, wote tuliopo hapa ndani ni Wabunge ambao tumechaguliwa na wananchi, tumetumwa kazi na wananchi. Sisi ndio wenye uwezo wa kuchochea maendeleo, sisi ndio wenye uwezo wa kumaliza nchi kimaendeleo, lakini vilevile sisi Wabunge hapa ndani kwa kutumia madaraka yetu tuna uwezo mkubwa wa kutetea amani ya nchi yetu. Lakini tusipokuwa makini tuna uwezo wa kupoteza amani ya Tanzania mara moja. Nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge wote bila ya kujali itikadi yetu, nawasihi Watanzania tena nawasihi kwa unyenyekevu kulinda amani ya nchi yetu. Sisi Wabunge ni waniasia, tutumie Ubunge wetu vizuri, tuangalie tunayoyafanya ndiyo wananchi wanayoyatamani. Watanzania wanatamani nini kutoka kwetu, wanatamani amani ya kudumu na maendeleo endelevu basi. Tuchochee hayo mawili na tunahakikisha tunachochea maendeleo. Tuhakikishe tunalinda thamani ya nchi yetu na Watanzania wataridhika.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliyopo madarakani pamoja na sisi kama sehemu ya Serikali, ni lazima tuhakikishe tunawaletea wananchi maendeleo. Wakiona tunawaletea maendeleo nchi itakuwa na amani, lakini pale pale sisi tuliopo madarakani mmoja mmoja kama Mbunge. Sisi Wabunge tuna uwezo wa kuchochea uvunjaji wa amani sana na hili nasema ukweli limeanza kuonekana. Hata mbuyu sote tunaujua mbuyu ulianza kama mchicha, ukaendelea ukaja ukawa mbuyu, sasa kuna kamchicha kanakoanza tuache kujenga mibuyu kwenye nchi hii. Tanzania ni nchi nzuri, naomba tujikumbushe wimbo mmoja wa *Atomic Jazz Band* uliimbwa na Stephen Hiza. Wimbo huo sitauimba kwa sababu sauti yangu sio nzuri kwa kuimba. Nitasema maneno yake kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika; “Tanzania yetu ndio nchi ya furaha, kote ulimwenguni watu wote watambua, Tanzania yetu ndio nchi ya amani.”

Mheshimiwa Spika, nawasihi Wabunge wote kwa umoja wetu, mshikamano mkubwa tusimame imara kulinda amani ya nchi hii. Usalama wa Watanzania upo mikononi mwetu humu, tukianza kuchocheachochea vitu vidogo tunamaliza Taifa letu.

Nawasihi Waheshimiwa Wabunge wote kila mmoja akashike jimbo lake, uchaguzi umekwisha tusimame kwenye usalama wa wananchi, maendeleo ya wananchi, amani ya wananchi, nchi yetu iwe na rutuba ya thamani tupu. (*Makofi*)

Naomba nirudi kwenye Muungano wa nchi yetu. Muungano wa nchi yetu sasa hivi ndio unazidi kuwa shwari. Hakuna mahali pazuri kama Zanzibar sasa hivi, hayo ndiyo maendeleo tunayoyataka. Yote yanawezekana kwa sababu ya mazungumzo, watu wamezungumza, wameelewana sasa hivi Zanzibar amani tupu. Hata huku yanawezekana, hakuna haja ya uchochezi, vurugu tuzungumze tu. Narudi pale pale kwamba sisi Wabunge ndio wenye uwezo wa kuchochea maendeleo, kuchochea amani lakini ndio wenye uwezo wa kuanza vurugu, naomba wote tuwe kitu kimoja, Bunge moja, baba yetu mmoja, mama yetu mmoja, tunajenga nyumba moja tusigombanie fito. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri. *(Makofi)*

Napenda niwapongeze Wizara ya Maliasili na Utalii kwa hatua nzuri ambazo wameanza kuchukua za kuondoa wavamizi wanaovamia misitu yetu. Misitu ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi za Halmashauri za Wilaya imevamiwa sana. Imevamiwa na wapasua mbao, wachoma mikaa, lakini pia imevamiwa na wafugaji wanaopeleka mifugo katika hizi hifadhi. Naomba nishauri Wizara iweze kuongeza *forest rangers* au niseme maafisa misitu katika misitu hii ili tuweze kuilinda. Lakini katika Halmashauri za Wilaya kuna fedha zinaitwa *Participatory Forest Management* ambazo fedha hizi zinaweza kuelekezwa kwa vijiji husika vile vijiji ambavyo viko kwenye maeneo ya misitu ili wahamasishwe wanavijiji waone kwamba ile misitu iliyoko karibu nao ni ya kwao, kwa namna hii inawezekana tukaokoa misitu yetu ambayo inamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linaweza likasaidia pia hii misitu ni katika sera yetu ya kuleta mapinduzi ya mfugaji kwa kuhamilisha mifugo. Mifugo ni mali na wafugaji watakubaliana na mimi. Lakini wengi katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora na pengine Mwanza (sio sana wale wakubwa) ndio wanafanya biashara ya mifugo, lakini wale wengine wanapenda waone kundi la ng'ombe kama 1,000 liko mbele yake anawachunga. Naomba elimu itolewe kwa wafugaji hawa kwa ajili ya kufanya biashara na mifugo hii na ihamilishwe kwa sababu kule Arusha kuna kituo cha kuhamilisha na kwenye Halmashauri za Wilaya kila Halmashauri imeanza huo mkakati wa kuhamilisha ili waweze kupata mifugo michache iliyo bora. Kwa hiyo, naomba sana elimu iweze kutolewa na Idara za Kilimo kwenye maeneo husika au kwenye Halmashauri za Wilaya ili mifugo iweze kuhamilishwa na kupata mifugo bora na baadae tutapata mifugo michache ambayo itatosheleza maeneo ilipo na hivyo hifadhi zetu hazitavamiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. AINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Rais. Vile vile nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo kuwepo katika Bunge lako hili nikiwa na afya. Vile vile nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Mkutano Mkuu Wilaya ya Tanga kwa kuweza kunichagua na Baraza Kuu la Uongozi Taifa kuweza kuniona kuwa nafaa kuwepo katika Bunge lako hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaelekea katika eneo la elimu ambalo Mheshimiwa Rais alilipa kipaumbele cha nane. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maelezo yake mazuri aliyoyatoa katika eneo hili. Mheshimiwa Rais ameongelea kuendeleza juhudi za kupanua fursa za elimu kwa vijana wetu tangu elimu ya awali, msingi, sekondari, ufundi na elimu ya juu. Kama kweli hili litatekelezeka, kwa kweli Rais atastahili pongezi za dhati kwani elimu ni tatizo kubwa, tena ni kubwa sana. Sote tunalijua hilo kwa sababu ya matokeo ya hivi karibuni ya Kidato cha Nne. Kwa kweli

yametishia amani ya nchi yetu, kwani elimu ndiyo viungo muhimu sana katika maendeleo ya nchi yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hilo Rais alisema kutoa msukumo wa kipaumbele maalum kwa masomo ya sayansi katika ngazi zote. Hili nina mashaka nalo kidogo labda endapo litafanyiwa msukumo wa hali ya juu, kwani kwa hali halisi tuliyonayo sasa hivi.

Mimi katika eneo langu ninalotoka la Tanga shule za sekondari ni 26 tulizonazo. Katika shule hizo ambazo zina maabara ni shule tano tu na hizo tumezirithi kutoka kwa wakoloni. Shule zote zilizobakia ambazo zimejengwa na kata hakuna maabara. Wanafunzi safari hii wamefanya *alternative practical*, kwa kweli hatuwezi kusema tunatoa msukumo katika sayansi kama hali hiyo iliyopo ni hiyo. Haiwezekani labda Serikali iweke kipaumbele tena kwa hali ya juu ili kuweza kuhakikisha shule zote zinazojengwa za kata zinakuwa na maabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shule hazina walimu kabisa, kama walivyochangia wachangiaji waliopita hali za shule zinakatisha tamaa kabisa. Ni Watanzania wengi sana wanapeleka watoto wao katika shule hizo kwani hawana uwezo wowote wa kupeleka katika shule za binafsi au za taasisi ambazo ada yake ni kubwa sana, jambo hili liangaliwe mara mbili au tatu.

Watoto tunawapeleka madarasa ambayo wanapita bila mafundisho yoyote kwa hali hii hatuwezi kutegemea matokeo mazuri ya Kidato cha Nne hata siku moja. Vilevile kama kweli tunataka watoto wetu wapate elimu basi tuwaangalie walimu. Hali ya walimu imekuwa mbaya sana na ni kweli kabisa sehemu wanazopangiwa kwenda kufundisha mazingira yake yanatisha, mazingira yake hayako rafiki, wanashindwa kabisa kuishi katika hayo mazingira na ndiyo maana wanaamua kufanya shughuli nyingine kuachana na ualimu.

Mheshimiwa Spika, naomba na hilo lizingatiwe sana ili tuweze kupata watoto ambao wameelimika na kuweza kupunguza hii aibu ya watoto ambao wamefeli kwa asilimia kubwa sana. Ni kweli elimu yetu imeshuka mno na mimi katika eneo langu Wilaya niliyotoka ya Tanga Mjini kuna shule mbili ambazo zimo katika kundi la shule kumi za mwisho. Hii inasikitisha sana. Katika shule hizo hakuna *division one, two* wala *three* ni *division four* tena mmoja au wawili na wote waliobakia ni zero. Hii inakatisha tamaa na naongelea hilo katika Wilaya hiyo iangaliwe kwa macho mawili au matatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado Tanzania ina safari ndefu kufikia utoaji wa elimu bora. Kiwango cha elimu cha sasa hakilingani kabisa na kile cha mwaka 1980. Kila kukicha elimu inashuka, tatizo la ubora la elimu ni suala la mfumo ambao haujatengemaa kwani mfumo huo tulionao ndio unaoruhusu matumizi ya lugha mbili za kufundishia katika daraja la elimu. Katika shule za Serikali tunawafundisha watoto darasa la kwanza mpaka la saba Kiswahili. Katika shule za binafsi na za Taasisi wanafundishwa watoto kwa lugha ya Kiingereza.

Kwa hiyo, mazingira hayo yanawapelekea watoto wale wanaposoma kwa Kiswahili wanapofika sekondari wanafelishwa na inabidi wajilazimishe kuweza kuelewa lugha ambayo hawakutumia miaka saba iliyopita. Hilo linachangia sana katika kufeli kwao, kwani baada ya ku-*concentrate* katika masomo hawaelewi kinachoongelewa, inabidi kwanza wachukue hatua za kuweza kujifundisha lugha. Wakati wakiwa tayari wanaielewa lugha hiyo wenzao wameshafika mbali hali hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili.

**MHE. AINA M. MWIDAU:** Asante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Amechangia vizuri tu.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipatia nafasi hii, kwanza kabisa kwa namna ya pekee napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama tena ndani ya Bunge hili Tukufu kwa kipindi cha pili. *(Makofi)*

Pia napenda niwapongeze wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba wakiwemo wapiga kura wangu wanawake kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao katika kipindi hiki cha pili, naahidi sitowaangusha. Nawashukuru sana kwa uchaguzi wao huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake aliyoitoa katika Bunge hili Tukufu akifungua Bunge Novemba, 2010. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake hiyo. Mheshimiwa Rais alielezea vipaumbele 13 katika hotuba yake, lakini ni mwendelezo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo ilikuwa inatekelezwa siku hadi siku kuanzia mwaka 2005, 2010 hadi 2015. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba katika utekelezaji wa Ilani uliokuwa unatendeka siku hadi siku au unatekelezwa na Serikali iliyoko madarakani na kila baada ya kipindi cha Bajeti Serikali ilikuwa inatenga fedha nyingi kupitia sekta mbalimbali kwa madhumuni ya kuleta maendeleo kwa Watanzania. Niliipongeza Serikali katika kipindi kilichopita ambapo ilitekeleza kwa kiwango kikubwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika maeneo mbalimbali, sekta mbalimbali kama ilivyokusudiwa, lakini narudia maneno ya Mheshimiwa Rais, katika kipengele cha 13 alichosema, naomba nimnukuu; “Kulinda mafanikio tuliyoyapata katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tangu Uhuru mpaka sasa. Aidha, tukamilishe yale tuliyohidi mwaka 2005 ambayo hatukuweza kuyakamilisha.”

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ambayo kila Wizara au kila sekta ilitekelezwa hatua kwa hatua lakini ziko changamoto ambayo zilijitokeza na zinaendelea kujitokeza na ndiyo maana wengi wao wakawa wanachangia hayo ni mapungufu ambayo yamejitokeza. Lakini jamani Serikali iliyopita imetekeleza kwa kiwango kikubwa sana. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wote na Serikali iliyopita kwa utekelezaji huo. Yapo mapungufu ambayo yalikuwepo na changamoto mbalimbali kwa mfano katika sekta ya elimu. Ucheleweshwaji wa mishahara ya walimu, kutokuwepo kwa maabara, kuhusu masuala ya Mfuko wa Bodi ya Elimu zipo kasoro mbalimbali au changamoto mbalimbali na haya ni kutokana na utendaji au watendaji kutokufanya kazi zao vizuri ili kuweza kuwafikia vizuri wanafunzi. Fedha zinatengwa kwa ajili ya mishahara ya walimu lakini kutokuwafikia walimu mishahara yao kwa wakati.

Kwa hiyo, hii ni changamoto kwetu, changamoto kwa Serikali au kwa Waziri aliopo madarakani sasa hivi pamoja na watendaji wa Wizara waliopo katika sekta hii kuweza kuhakikisha walimu wamepata mishahara kwa wakati, maabara ambayo imekusudiwa kujengwa katika kipindi hiki zimejengwa, shule ambazo zitaendelezwa na zimeendelezwa na Bodi ya Mikopo tuweze kuweka juhudi sisi Wabunge kuweza kuongeza fedha siku hadi siku ili wanafunzi wetu walio wengi waweze kufaidika na mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mheshimiwa Rais ameunda Tume Maalum kwa ajili ya kushughulikia masuala ya mikopo ya wanafunzi. Jamani tumpongeze Mheshimiwa Rais amejitahidi sana na anaendelea kujitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naeleza kuhusu changamoto ambazo zilikuwa zimejitokeza katika kila Wizara. Hiyo ni sekta ya elimu yapo mambo mengi lakini muda hautoshi. Lakini kuhusu kilimo, katika kipindi kilichopita Serikali iliweka msisitizo wa kusema au wa kuweka mkakati wa Kilimo Kwanza. Katika kipindi kilichopita suala la Kilimo Kwanza ni pamoja na pembejeo kuanzishwa kwa Benki ya Wakulima, kwa hiyo tuangalie katika kipindi hiki Serikali haijaanzisha Benki ya Wakulima. Kwa hiyo, ni mkakati gani ambao utawekwa sasa hivi katika harakati za kuanzisha Benki ya Wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na lingine ni kuhusu suala la kuwezesha hawa ambao watakopesha. Wanawake wapewe kipaumbele cha aina yake ili tuweze kuondokana na suala la njaa ambalo lipo. Kuboresha mazingira ya umwagiliaji katika sehemu ambazo hatuzalishi kwa wingi au zile ambazo zinazalisha chakula kwa wingi kwa hiyo, tuboresha mazingira ya umwagiliaji kuweka miundombinu ili chakula kiweze kupatikana kwa wingi. Kipindi kilichopita tumezalisha katika maeneo mbalimbali mpaka chakula kilikuwepo cha kutosha. Lakini kutokana na jua lilikuwepo sasa hivi mazao yamekauka ndiyo yametokea hayo. Kwa hiyo, tuipongezeni sana Serikali kutokana na juhudi zake. Kwa hiyo, sasa hivi ni kuangalia changamoto gani ambayo inataka kushughulikiwa tuweze kuitatua hatua kwa hatua ili tuweze kufikia maendeleo ambayo Mheshimiwa Rais amekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uwekezaji. Kuna changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza, mara nyingi tulikuwa tunalalamika hapa wanaofaidika sana katika suala la uwekezaji ni wageni. Tutilie maanani au tuweke mkakati ili wazalendo wafaidike na suala la uwekezaji na wale wawekezaji ambao wanakwepa kodi wadhibitiwe kwa sababu ikifika mwaka mmoja miaka mitano wanabadilisha jina wanaweka jina lingine.

Kwa hiyo, tuangalie kwa undani kabisa mwekezaji huyu anakwepa kodi kwa namna gani ili tuweze kumdhibiti aweze kulipa kodi inavyotakiwa. Kwa hiyo, lazima tusifie mafanikio yaliyopatikana na jinsi Mheshimiwa Rais alivyojitahidi hadi kufikia hapa tulipo sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, hoja.

**SPIKA:** Sikusikia, endelea.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja chini ya Kanuni ya 55(3)(e) na (f). Hizo Kanuni ndogo ya (3) inasema, hoja zifuatazo inasema zinaweza kutolewa bila taarifa (e), hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura na (f) hoja kuhusu jambo lolote linalohusiana na Haki za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba...

**SPIKA:** Sasa lipi, dharura au Haki za Bunge?

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ni dharura na ni Haki za Bunge.

**SPIKA:** Hapana, tuna moja ndiyo maana yapo tofauti. Sasa kama ni dharura tusomee kifunga cha dharura na masharti ya dharura.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, hoja...

**SPIKA:** Naomba usome masharti ya dharura.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba unipe muda kidogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema endelea.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, basi naomba nisome cha Haki za Bunge.

**SPIKA:** Nimekupa muda usome, Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema anaendelea kujadili.

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Vunjo, waliziba masikio, hawakudanganyika, nilichangiwa kama mpira wa kona lakini kwa upendo na ukarimu wao wakasema iwe isiwe Mrema ni Mbunge wetu katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru sana waendeleo na upendo huo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya yeye na Serikali yake kule Vunjo. Mradi mzuri unaosimamiwa na Serikali ya awamu ya nne ni utengenezaji wa barabara za lami. Barabara ya lami kutoka Mwika Madukani kwenda Kilacha, barabara ya lami kutoka Mwika kwenda Marangu Mtoni hazikuishia hapo, barabara ya lami kutoka Marangu Mtoni kwenda Kilema Kaskazini, Kirua Vunjo Magharibi mpaka Kawawa, namshukuru sana. Hizo ni barabara za lami zilizo katika Jimbo langu maana kuna watu walikuwa wanaambiwa kwenye Wapinzani hakuna maendeleo, kwa Mrema kuna maendeleo tena ya lami. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pili barabara za udongo. Kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya barabara za Kilema Tofo kwenda Kilema Hospitalini pale. Naishukuru sana Serikali naomba isimamie barabara ile kwa sababu pale kuna Chuo cha Elimu ya Taifa Mandaka na Seminari ya *St. James*. Kuna barabara ya Uchira kwenda kwa Raliadi Kirua Vunjo Mashariki. Naomba sana na naambiwa TAMISEMI ilikuwa imetenga shilingi milioni 172 kwa ajili ya kutengeneza barabara ile. Naomba niwakumbushe wenzetu wa TAMISEMI wahakikishe fedha zile zinapatikana ili barabara zile za Uchira kwenda Kisomachi ikamilike.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niishukuru Serikali inajenga Hospitali kubwa ya Wilaya pale Himo na karibu inakamilika, imebaki ujenzi wa nyumba za kulala wagonjwa badala ya kwenda Mawenzi na *KCMC* watu wa Vunjo tunaweza tukaishia pale Himo, hongera sana.

Kuna suala la kujenga soko la kisasa pale Njiapanda. Soko hili litakuwa na maana kwa sababu wenzetu wa Kenya wanajenga Kituo kikubwa cha kurusha ndege, badala ya ndege kwenda Nairobi zitakuwa zinakuja pale mpakani pamoja na ghala kubwa sana. Sasa sisi tunaweza tukatumia nafasi ile kwa kuendeleza lile soko la kisasa tayari Serikali imekwishatenga shilingi milioni 93 kujenga uzio.

Kwa hiyo, nasisitiza na naiomba Serikali iendeleo na ikamilishe huo uzio na hilo soko likamilike ambalo naambiwa soko litakuwa kubwa na zuri kuliko hata Kariakoo. Kwa hiyo, watu kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi wanaweza wakaja pale kununua mazao yetu ambayo tunayo kama ndizi, maharage na mazao mengine yanayofanana kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana Serikali kwa kusambaza maji safi katika Jimbo la Vunjo. Leo asubuhi limejibiwa swali lakini nataka niendeleze kuonesha kazi nzuri sana inayofanywa. Wajerumani wameleta mradi pale wenye thamani ya shilingi bilioni 15.3 kwa hiyo vijiji vya Kirua Vunjo Magharibi, Kirua Vunjo Mashariki,

Kirua Vunjo Kusini, Kahe Mashariki, Kahe Magharibi, Kilema Kusini na sasa hivi kuna suala la kusambaza maji Mji wa Himo ambao tayari Rais wetu alitoa ahadi ya kuchangia shilingi milioni 150 na leo Waziri amehakikisha kwamba fedha zile zitapatikana ili mradi ule ukamilike. Karibu wiki tatu niliongea na Rais na akaniambia mradi ule ukikamilika atakuja kuufungua mwenyewe. Namshukuru sana. (*Makofi*)

Mhesimiwa Spika, katika hotuba yake amezungumza suala la Kilimo Kwanza. Sasa naomba bei ya kahawa imepanda kidogo ni dola 3.20 kwa kilo lakini kwa bahati mbaya kahawa kwetu Vunjo imeshatelekezwa wakati bei ilikuwa ndogo. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba naomba Serikali ione namna gani inaweza ikatufanya tukafufua lile zao kwa kuotesha miche mipya ambayo ukiiotesha miaka miwili na nusu unavuna kahawa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba msaada wa Wizara ya Kilimo na Serikali kuwa watu wangu wako tayari kubadilika, ile miche ya zamani ina miaka 70 karibu 100 haizai tena vizuri. Kwa hiyo, tupate miche mizuri ya kahawa ambayo miaka miwili na nusu mpaka mitatu tunaweza tukavuna. Mtakuwa mmetusaidia sana na kwa kuwa kule eneo ni dogo, naomba ng'ombe wa kisasa. Serikali inatoa ruzuku kwa mbolea na pembejeo sijui na vitu gani, sisi ng'ombe wa kisasa kwa sasa ni shilingi laki kwa ng'ombe mmoja watu hawana uwezo. Kama mbolea tunapeana kwa ruzuku kwa nini tusipate ruzuku ya ng'ombe akauzwa laki mbili hizo nyingine Serikali itafidia na ndama akizaliwa tunaweza tukatoa kwa mtu mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho na hali ya usalama. Sisi tumejitahidi sana kule, ujambazi umezungumzwa kwenye Hotuba ya Rais. Ninachotaka kusema kwamba sisi Vunjo tumeshaorodhesha majambazi yote wapo 378, tangu miaka miwili iliyopita. Tumeorodhesha na wanywa gongo pamoja na wanaovuta bangi. Tatizo Serikali hamjawakamata wala hamjawahoji. Kwa hiyo, nimeleta orodha ya yale majina ambayo wananchi walipiga kura ili Waziri wa Mambo ya Ndani na Serikali yote, tuna *RPC* mzuri, *OC-CID* tunashirikiana vizuri.

Kwa hiyo, wanahitaji mafuta kwenye magari yao, ndiyo tatizo ambalo nimeliona pale. Naomba muwasaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nashukuru hoja mliyopitisha kuhusu kuimarisha Kambi ya Upinzani. Kuna watu wanaamini kabisa lengo la Muswada ule ni kudhoofisha Upinzani. Nadhani imepanua wigo kwa sababu ingawa Mrema yuko hapa mwenyewe na ukiangalia *CV* ya Mrema na shida ya wengi waliopo hapa mimi nilitegemea wapinzani wenzetu wangenitumia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo mnaweza mkamtenga mtu ambaye alikuwa Naibu Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, mtu amegombea Urais mara tatu, mtu ambaye nimekuwa Mbunge kwa vyama vitatu katika majimbo matatu na hata hili suala la ufisadi. Mwaka 1992 nilikamata ndege yenye dhahabu, kwa hiyo ufisadi haujaanza juzi. Nyie CHADEMA mjifunze kutoka kwenye uzoefu nilio nao. Kesi ya Chavda mpaka nikajitoa mhanga nikafukuzwa, nyie



mmefukuzwa kwenye jambo gani ambalo mmefanya? Hata nilivyokuwa *NCCR*, kesi ya shilingi milioni 900 niliteseka. Sasa nakuja hapa na kama ingekuwa ni kwamba Kiongozi wa Upinzani iangaliwe *CV*, mimi ndiye ningekuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nimeanza Ubunge kule Vunjo nimepambana na mmesikia *RPC* kule Kilimanjaro ananisifu. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumaliizka muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Asante sana, kengele imegongwa. Sasa nitamwita Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA:** Nadhani *message sent*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, kuhusu nini?

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba idhini ya Spika ya kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma chini ya Kanuni ya 47(3) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 55(3)(e) na (f). Naomba idhini Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ungeeleza kidogo maana idhini ni mimi ninayeitoa na kwa muda huu dharura. Ngoja nisome mimi kwanza, lakini mimi nikisimama nyie muwe mnakaa.

Kuhusu suala la dharura. Kifungu cha 47 Kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura kifungu cha 47(1) “Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi na la dharura na muhimu kwa umma.” Sasa nataka kujua hilo jambo dharura na muhimu kwa umma sasa hivi ni nini na tena wala si kipindi cha maswali.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako Tukufu linaendelea na kikao chake sasa hivi nimeletewa *summons* ya Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma humu ndani ikiniagiza niende kwa Jaji Mwangesi siku ya Alhamisi tarehe 10 Februari, 2011 yaani kesho kutwa.

**SPIKA:** Kufanya nini huko? Sisi hatuhusiki na hilo.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuna *summons* hapa imeletwa sasa hivi.

**SPIKA:** Kwa kosa gani?

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba nisikilizwe tafadhali. Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Kinga na Mamlaka na Haki za Bunge kinasema kwamba; “*Notwithstanding anything to the contrary, no summons issued by any Court of*

*the United Republic or outside the United Republic in the exercise of its civil jurisdiction shall be served or executed within the precinct of the Assembly while the Assembly is sitting, or through the Speaker or any other officer of the Assembly, nor shall any member be arrested on civil process, save by the Leave of the Speaker first obtained, while he is within the precincts of the Assembly and while the Assembly is sitting.”*

Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Tafadhali hapo naomba ukae chini. Naomba ukae. Hiki ndiyo kifungu cha 47(1) kinasema jambo la dharura lililotokea sasa hivi na lenye maslahi muhimu kwa umma. Sasa kama wewe mwenzetu umekuwa *saved*, hili ni suala ambalo tungeenda kuongea ofisini, tukatafuta utaratibu wa kuwaeleza hao kwamba Mbunge katika shughuli zake anafanya nini. Sasa kweli kabisa kuna maslahi ya umma kwa sababu umekuwa *saved and noticed?* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Livingstone Lusinde, tafadhili endelea.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ambayo nimeisubiri kwa muda mrefu sana na nitakuomba Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanivumilie kwa sababu kama kujaa Roho Mtakatifu nimejaa muda mrefu sana lakini nimechelewa kupata hii nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa ajili ya wapigakura wa Jimbo la Mtera kwa kura nyingi walizonipatia na kuniwezesha kuingia hapa, lakini zaidi nimshukuru mke wangu mama Edina Lusinde kwa namna alivyokuwa akinituliza nilipokuwa nikipandwa na jazba wakati wa kampeni za uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake alifafanua mambo makubwa ambayo Serikali imefanya na mambo ambayo inategemea kuyafanya na ndani ya hotuba yake alizungumza kwa kirefu sana juu ya masuala ya msingi yanayogusa amani, mshikamano na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, inavyoonekana kwenye suala la amani ninavyotazama mimi ni kama vile wengine tumechoka. Wamechoka, tumeshiba sana neno hili sasa tunataka ivurugike na ndiyo maana tunaweza kuona baadhi ya viashiria vinatokea. Kwa bahati mbaya sana mimi kama Mbunge kwenye suala la amani sioni kama kuna umuhimu sana waku-*provoke* jamii yetu ili iumie, isipokuwa kama kweli tunadhani tunayo nafasi ya kuvuruga amani ni vyema tungeanza kuvuruga humu kwanza.

Mheshimiwa Spika, hebu siku moja tupigane wenyewe humu ili watu wajue kwamba kweli hawa wanaotaka imani ivurugike na wao wana uwezo huo. Sio kwenda kuwasakizia watu waumie halafu sisi tuko salama tunataka umaarufu kupitia damu za watu wengine. Hili halikubaliki.

Kwa hiyo, ni vyema kama kuna Mbunge anaona anaweza haya akaanzisha humu na mimi Lusinde niko tayari tukafunga mlango tukapigana humu halafu tukatoka tukawaambie wananchi jamani madhara ya haya ni haya tuliyoyaona kuliko kwenda kuwatumia watu wengine wafe, wengine waumie, halafu sisi tuwe maarufu kisiasa. Naona hili si sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, halafu jambo la pili, Serikali ya Awamu ya Nne wamekuwa wavumilivu mno. Imefika mahala wanapakwa matope ambayo si ya kweli. Mtu anatamka hadharani kwamba Serikali hii imetupiga mabomu. Mimi mwenyewe katika maisha yangu nimepata kupigwa na gesi za machozi nikiwa upande wa upinzani na Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema akiwa Waziri. Lakini sikuita bomu kwamba kwa bahati mbaya sasa Serikali inapakwa matope kwamba inapiga wananchi mabomu.

Mimi nataka niseme Serikali ya Tanzania haijawahi kupiga wananchi mabomu, bomu si jambo la mchezo. Kwa bahati mbaya sana mabomu yalilipuka pale Mbagala, yale ndiyo mabomu kwa wale ambao hawayajui mabomu yale ya Mbagala ndiyo mabomu. Bomu likilipuka halina masihara. Hizi zingine ni gesi za machozi si bomu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka niweke sawa hilo kwamba ndani ya nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijapata kutokea Serikali ikatumia mabomu dhidi ya raia wake kwa sababu bomu si kitu cha masihara. Nampongeza sana Rais kwa uvumilivu, amekuwa mvumilivu sana, wapo watu wamepitiliza mipaka sana, wametufikisha mahali ambapo mimi mpaka najiuliza hivi Kikwete uanajeshi wake kumbe haujamuathiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais yule hajaathiriwa na uanajeshi, yule ni mwanajeshi, lakini amevumilia, amepitiliza mpaka imefika mahali watu wanamtoa kikatuni, wanamweka kwenye mtandao wanafanya vitu vibaya kabisa ambapo viongozi wengine wasingeweza kuvumilia. Lakini yeye ameendelea kuvumilia, tunataka tuchukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya za kukuza demokrasia kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi yamezungumzwa na wenzangu, kwenye suala la kilimo tunahitaji kulitazama upya. Sisi wengine tulioingia humu ni watoto wa wakulima kweli kweli na tushukuru sana Serikali kwa Sheria ile ya Rushwa imesababisha hata akina Lusinde tumekuwa Wabunge tunawashukuruni sana kwa sababu tusingeweza kudhibiti hata kidogo na Ubunge sisi wengine tungeusikia kwenye ndoto, maana mkitaja watoto wa maskini waliongia humu msiponitaja mimi wote mtachomwa moto nyie, maana mimi ni miongoni mwa watoto hawa maskini kabisa wa nchi hii ambaye nimefanikiwa kuwa Mbunge kwa Sheria hii. Kwa hiyo, suala la kilimo ni suala la kufa na kupona. Hatuwezi kila siku tunazungumzia njaa, tunazungumzia kilimo.

Ningeishauri Serikali hivi tunawezaje kupeleka maboksi ya kura kila kona ya kijiji lakini tunashindwa kupeleka mbolea kila kona ya kijiji? Hebu tupeleke mbolea

karibu na wananchi na ikiwezekana tujikusulu kujitoa mhanga. Tuweke nchi yetu katika kanda za kilimo, tuwape mbolea bure, kuna shida gani ili tuondoe tatizo la njaa? Kwa hiyo, mimi nina maoni hayo kwenye suala la kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo nataka nimpongeze Rais na kwa hili nataka nipongeze Serikali ya Awamu ya Nne. Nimpongeze Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu aliyepita Mheshimiwa Edward Lowassa kwa shule za sekondari za Kata. Mmefanya kazi nzuri sana. Myonge mnyongeni haki yake mpeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Edward Lowassa umefanya kazi nzuri sana pamoja na wenzako, sisi tunawapongezeni sana pamoja na changamoto zilizopo. Changamoto nyingine na sisi wenyewe Wabunge lazima tujifunze, tumepata Waziri Mkuu aliyejiuzuru mwenyewe, kuwajibika kwa ajili ya makosa ya watendaji wake. Wengine hapa hata kujiuzuru kwa makosa ya chama tu hawawezi, wengine hata kujiuzuru kwa timu kufungwa hawawezi, lakini wakisimama hapa hadharani wanazungumzia demokrasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo Bunge lako Tukufu limefanya kazi ambayo haikutakiwa kufanywa. Wabunge wa CCM wanastahili pongezi kwa kuinusuru Kambi ya Upinzani iwe timu mmoja. Tungewaacha wavurugane, lakini leo tumekaa hapa tumewatengeneza wawe kitu kimoja bado wanatuona sisi wabaya. Ndugu zangu nataka niwaambie viongozi katika nchi yetu asiyekubali kuongozwa hata yeye kuongoza hafai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha bado ni ndefu sana lakini nilifikiria niwaelekeze kuna kazi ambayo tunapaswa kufanya. Nimeshabandika majina ya Kamati kwenye *notice board* pale kwenye Jengo la Utawala. Sasa ni vizuri mkaona zile Kamati kwa sababu kesho tutaingia kuchagua Wenyeviti wa Kamati hizo.

Kwa hiyo, mtaona kwamba katika uteuzi wa Kamati hizo na mtakumbuka kuwa katika Mkutano ule wa Kwanza mlipewa fomu na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kuomba kuteuliwa katika Kamati mojawapo ya Kudumu ya Bunge kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 113. Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni hiyo, naomba kutoa taarifa kuwa zoezi hilo limekamili na mkienda kule nje mtaona majina yenu. (*Makofi*)

Sasa kwa utaratibu uliofanywa na Katibu wa Bunge ni kwamba tumeangalia nyaraka zifuatazo, maombi yaliyowasilishwa na Wabunge, maelezo binafsi ya Wabunge yaliyokuwepo ndani ya CV zenu, vigezo vilivyoanishwa katika Kanuni ya 113(5) na matokeo ya uchambuzi wa awali wa maombi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati mchakato wa kupitia maombi ulipofanyika ilibainika kuwa Wabunge wengi walikuwa wamejitokeza kuomba Kamati fulani fulani na hivyo kufanya baadhi ya Kamati kuwa na waombaji wachache na nyingine kukosa kabisa waombaji.

Aidha, ilionekana kuwa baadhi ya Wabunge wenye ujuzi maalum wamejazana kwenye baadhi ya Kamati na hivyo kuzifanya Kamati nyingine kukosa Wabunge wenye taaluma zinazohusika. Kwa kuzingatia upungufu huo niliona ni busara kufanya uteuzi kwa kutilia maanani masharti na vigezo vilivyoelezwa katika Kanuni ya 113(5) kama ifuatavyo:-

(a) Kuteua idadi inayolingana kwa kila Kamati isipokuwa kama Kamati imeelezwa hivyo katika Kanuni kwa mfano Kamati zile za *watchdog* ni 15.

(b) Kuzingatia aina zote za Wabunge na kuwateua Wabunge mbalimbali akiongozwa na kigezo cha asilimia ya Wabunge hao iliyoko hapa Bungeni.

(c) Kwa kadri ilivyowezekana kuyapa kipaumbele matakwa ya Wabunge wenyewe lakini kutolazimika kutosheleza matakwa hayo au malengo hayo.

(d) Kuzingatia hoja ya haja kwa kila Kamati kuwa na Wabunge wenye uzoefu na ujuzi maalum kuhusu kazi za Kamati inayohusika.

Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia idadi ya Wabunge wa Chama Tawala na Kambi ya Upinzani, jinsia, ujuzi maalum wa Wabunge mbalimbali ya wakati uliopo katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia, siasa na demokrasia nimefanya uteuzi katika Kamati mbalimbali pengine tofauti na matarajio ya wengine wenu. (*Makofi*)

Pamoja na vigezo vilivyotumika, napenda nikiri kuwa zoezi hili lilikuwa gumu, lengo kubwa lilikuwa ni kuboresha na kuleta ufanisi katika utendaji kazi za Kamati. Naomba sote tuelewe na kuikubali hali hiyo na nina imani kuwa tutafanya kazi vizuri na kufahamiana zaidi kwa kipindi chote cha miaka miwili na nusu ya sehemu ya kwanza ya uhai wa Kamati hizi.

Waheshimiwa Wabunge, nimeona niseme haya ili kuwajulisha mambo ya msingi niliyoyazingatia katika uteuzi niliufanya kwa mujibu wa Kanuni 113(5). Kwa hiyo basi, kutokana na hili kesho tutafanya uchaguzi wa Wenyeviti wa Kamati hizo.

Kwa hiyo, mnaombwa mkaangalie majina yenu wale wenye nia ya kutaka kugombea vyeo katika hizo Kamati wanaweza kupita na kuomba kura na kesho tunafanya uchaguzi huo kusudi tuanze kuendelea na mfumo mwingine wa kazi zinazofuata. Kuna Kamati zingine tunashindwa kuchagua wale Wenyeviti kwa sababu Kamati hazijaundwa. Kamati ya Uongozi haikai kwa sababu Kamati hazijaundwa bado. Kwa hiyo, nawasihi mkienda huko mpate muda wa kuweza kuangalia majina yenu yapo wapi. Sasa rufaa msinikatie mimi tena sina rufaa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo nina matangazo machache. Katibu wa Kamati ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jenista Mhagama baada ya kuahirishwa kikao hiki anaomba Wabunge wa CCM wakutane kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine, napenda kesho kwa sababu orodha yetu ni kubwa tutaendelea na mjadala kama tulivyopanga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.30 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,  
Tarehe 9 Februari, 2011 saa tatu asubuhi)*